# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

Verbatim Report of

# DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, TAITA TAVETA CONSTITUENCY

# AT VOI C.C. HALL

ON

17 OCTOBER 2002

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, VOI CONSTITUENCY, HELD AT VOI C.C. HALL ON 7TH OCTOBER 2002**

**Present:**

1. Zein Abubakar Zein - Commissioner

**Secretariat Staff in Attendance**

1. Nickson Ogira - Programme Officer

The meeting started at 10.00 am.

**Speaker:** Watu wote na wanakamati ambao wemekuja kwa mkutano huu ambao umekuwa kwa mambo ya Katiba, lakini sasa ningetaka Reverend Ilo aje atufungulie mkutano huu kwa maombi tafadhali.

**Reverend Ilo: (Prayer)** Basi tuombe Mungu ili aongoze kikao hiki, na tuombe. Mungu wetu iliye hai mwenye uwezo, mwenye nguvu, mwenye ushindi, twakushukuru kwa kuwa umetuwezesha tukae katika mkutano huu basi namweka Chairman wenu na Speaker na wote ambao wamezungumza habari hii ya Katiba, twaomba Baba utangulie ili kila jambo liwe la mfano wako. Kwa Kristo Bwana wetu.

**Audience:** Amin.

**Committee Chairman – Voi:** Bwana Coordinator, Madam Frida Coordinator wetu na wanakamati wenzangu. Karibu katika mkutano huu, hii ni mara ya pili ama ya tatu kukutanana hapa. Jambo la kwanza tulipokutana hapa tulikuja kutoa mawazo yetu ili Katiba iandikwe kulingana na maoni yetu ambayo tuliyatoa wakati huo, ingawa wakati huu ni kusikiliza yale yalioandikwa kulingana na mawazo ambayo tuliyatoa. Sasa yatakayosemwa na Bwana Commissioner ni yale ambayo sisi tuliyatoa na kama kuna jambo lolote ambalo unafikiri tuliacha unaweza kusema. Kama umesikia maneno yoyote ambayo wewe unafikiri hukusema, hii ni chance yako ya kuibadili. Mengi sina, lakini ninataka kuanza sasa. Sasa ningetaka kumpa Frida Mwadime ambaye ni coordinator wetu atuonyeshe agents na wanakamati wetu.

**Frida Mwadime (Coordinator):** Asante sana Bwana Mwenyekiti wa Constituency ya Voi. Wananchi wa Voi, akina mama, wazee, vijana na walemavu, hamjambo?

**Audience:** Hatujambo.

**Frida Mwadime:** Kama alivyowaambia Rukia, majina yangu ni Mrs. Frida Mwadime na aliyeshirikishi wa mambo ya Katiba katika wilaya ya hii location. Nafikiri kabla hatujataja zaidi ningetaka umgeukie mwenzako tu umwambie pongezi.

**Audience:** ***(Laughter and murmur at the background).***

**Frida Mwadime:** Asanteni sana. Ni kwa nini nimesema mpeane pongezi ni kwa sababu wale ambao walikuwa hapa wakati wa civic education, tukiwa na Commissioner Abubakar Zein ambaye ameketi mbele yetu leo alituambia kwamba wao hawana maoni yao, maoni lazima yatoke kwa nani?

**Audience:** Kwa wananchi.

**Frida Mwadime:** Na wakati ambapo waliwasili wakachukua maoni na leo tuna ushahidi kwamba maoni ya wananchi wa Kenya kutoka sehemu ya wakilishi Bunge ya Voi yametiliwa maanani kutokana na repoti hii ambayo tunasoma hapa leo. Tutachambua hiki kitabu bado hasa, katika location level na katika sub location. Kwa hivyo leo tutajumuika pamoja nanyi and that is fair kwa sababu hatuwezi kutoa vyote hapa na tukienda Kavirago ama Changara, hata sehemu ya juu……(Inaudible) na wananchi repoti inayotokana na maoni ambayo wananchi wametoa.

Jambo lingine ni kwamba, ilikuwa inaonekana ya kweli constituency ya hapa maoni yote ambao wananchi wa Voi walitoa katika mahali hapa na …..Commission imeyanakili na kuyaandika katika kitabu hiki na nimesema kwamba itapewa kila nakala

katika kila location ya Voi Constitutency. Ili kwamba tukienda sehemu ya location na sub location wananchi wataangaliaje yale maoni tulitoa Voi na Karuga yalitiliwa maanani. Kwa sababu hatuna budi tujipongeze zaidi sana ni kwamba ni tayari na ni kweli kwamba hata sisi nasi ambao tulipewa jukumu la kufanya jambo hili kwa kweli tumejitolea kwa nafsi, kwa mali na kwa hali kuona kwamba la swala yote ya wananchi walitoa pendekezo yametiliwa maanani.

Jambo la pili ningesema wakati huu, hiyo ribbon umevaa ni rangi gani?

**Audience:** Yellow.

**Frida Mwadime:** Jambo la kwanza ni kuwa la kuungana na wale wenzetu ambao ni wanasheria katika marekebisho ya Katiba kuhusu wale ambao wanajaribu kupinga mjadala muhimu wa Katiba. Pili, nafikiri sasa tumetafsiri.

**Audience:** Ndio.

**Frida Mwadime:** Tumefika mahali ambapo kuna taabu fulani, si hivyo? Rangi ya kwanza ni ipi? Red si ndio? Inakuabia simama usiondoke. Rangi ya pili, yellow ambayo inakuambia nini?

**Speaker:** Kaa tayari kuvuka.

**Frida Mwadime:** Kwa hivyo leo tuko tayari kuvuka, kama ningekuwa katika Kanisa ningesema "Amen". Ama si hivyo, tuko tayari kuvuka si hivyo?

**Audience:** Ndio.

**Frida Mwadime:** Na kama tunavuka lazima tuvuke na jambo jipya hata wale Waisraeli walikuwa tu wanavuka bahari ya Shamu kwenda nchi ya ahadi. Walikuwa na Katiba ambayo ni amri kuu ya itavukwa ama vipi?

**Audience:** Ndio.

**Frida Mwadime:** Kwa hivyo tunahitaji watu waungane vile tulifanya wakati wa civic education, few good men and women. Kama uliangalia katika Biblia kati ya watu kumi na wawili waliotumwa na Musa wawili ndio walisema ikiwa Mungu yuko upande wetu ile nchi ya ahadi hatutaichagua, si hivyo? Wale wengine kumi walisema haiwezekani kuna majitu, kuna ….lakini Joshua na Caleb walisema ikiwa Mungu ametupatia tutavuka na wale wengine walikataa. Leo nasi tutavuka. ***(Laughter*)** Asanteni.

Na kwa sababu nii nimekupeleka kwa hiari na tukumbuke tuko tayari kuvuka na si kuvuka kwa fujo bali hata tukipigwa na sisi tutavuka kwa sababu tuko na Katiba mpya ambayo huyu Commissioner anaeleza kwa moyo wake wote. Naye amezunguka Kenya nzima na anajua vile Wakenya wanavyoishi, maisha vile yalivyo kulingana na watu mbali mbali na makabila mbali mbali katika nchi ya Kenya lakini leo katika Katiba mpya tunasema sisi Wakenya. Hatujajigawanya vile ilivyokuwa kwa watu hapo awali na kwa sababu hiyo ningependa kumjulisheni kwenu kwa mara nyingine, kwa hivyo mjulisheni kwetu halafu atatujulisha wale ambao pia amekuja nao halafu tutaendelea na Katiba yetu siku ya leo.

Kile nitakachowaomba Wakenya ni kwamba the light of Kenya kwa sababu sote ni Wakenya ijapokuwa tu ni makabila mbali mbali, dini mbali mbali na madhehebu mbali mbali. Ni kwamba tunahitaji kupokea siku ya leo kupigia halali, kusoma yale ambao Wa-Commissioners wamependekeza na hali …(Inaudible) halafu mwishowe Wakenya ndio wataamua pia. Si Ma-Commissioners, wamefanya kazi yao nyinyi ndio mtaamua pia. Je, mnapenda kukaa vile tulivyo ama muwe tayari kuvuka? Tuko pamoja, kwa hivyo mbele yenu ni Commissioner Abubakar Zein nitampa nafasi awasalimu kisha atawajulisha maofisa ambao wameandamana naye, wale committee members wa hapa Voi kutoka kila mahali na sehemu nyingine. Kwa hivyo atatujulisha yule amekuja naye halafu tutaendea kutoka hapo. Nashukuru kwamba Mayor amefika na hatakuwa tu Mayor wa Voi lakini pia ni Mwanakamati wa Committeee ya Marekebisho ya Katiba ya Voi. Karibu Mayor, Commissioner Zein.

**Bwana Mayor:** Habari ya asubuhi?

**Audience:** Mzuri.

**Frida Mwadime:** Ni Programme Officer Bwana Ogira. Ogira, salamia wananchi wa Voi.

**Nickson Ogira:** Hamjambo wananchi wa Voi.

**Audience:** Hatujambo.

**Frida Mwadime:** Aliyeketi kule na pia ambaye tunamfahamu sana. Nafikiri kwa wakati huu anaweze kuwasalimia pia, Ahmed.

**Ahmed:** Hamjambo. Sorry, sorry.

**Com. Zein Abubakar**: Hamjambo wananchi wa Voi.

**Frida Mwadime:** Pole pole.

**Com. Zein Abubakar:** Haisikiki pale kwa hivyo mtu akitaka kusema aje hapa.

**Frida Mwadime:** Asante tuna pia marafiki wetu ambao wameketi pale pengine mmoja wao asalimie wananchi kwa niaba ya yule mwenzake. Asante karibu

**Salim Mwangune:** Hamjambo?

**Audience:** Hatujambo.

**Salim Mwangune:** Nimeleta salamu nyingi sana kutoka watu wengi wa Nairobi ambao wanategemea Wataita wanasema nini?

**Audience:** Na Jina Lake?

**Frida Mwadime:** Jina lake ni Salim Mwangune.

**Salim Mwangune:** Kwa hivyo tunaposema Mwangune nafikiri wale ambao wanamjua Mzee Mwalimu Ogola na mtaenda kulinganisha.

**Frida Mwadime:** Nafikiri sasa tutaanza na Katiba yetu ya leo na nitapeana vifaa hivi kwa Commissioner Zein ingawa anasema sauti yake ni kubwa sana lakini kwa sababu ya wananchi wa Kenya wale walioko hapa Commissioner nafikiria utatumia vifaa hivi.

**Com. Zein Abubakar:** Asante sana Mrs. Mwadime. Mayor wetu, Mwenyekiti, Mwalimu wangu Mzee Mawaziri, Coordinator Mrs. Mwadime, wanachama wa 3C's, viongozi mbali mbali mliofika hapa. Kwa heshima zangu kubwa mimi nasimama kwenu kuzungumza na nyinyi tena. Na leo ninafuraha kubwa kuwa nanyi sio tu kwamba ninafuraha kwamba Mrs. Mwadimi ni mchokozi na saa ingine kutupaka mafuta. Ninafuraha kwamba kuwa niko pamoja na nyinyi kwa sababu salaah.

La kwanza kabisa, ni kwamba mimi ni mtumishi wenu na mimi ni mwakilishi wa Tume ya Marekebisho la Katiba ya Kenya. Ninafuraha kwamba nimefika hapa ili kuwaletea kazi mlilotuma sisi ili tuweze kuitikia pamoja na turudi kuangalia na kuhakikisha kwamba mambo yaliyoko ndani ni yale mliotuambia. Jambo lingine ambalo limenipa furaha kubwa ni kwamba nimeona mahali ya watu ambao sasa wamekuwa marafiki zangu kwa sababu tulipokutana kutoka siku ya kwanza tulianza kubadilishana mawazo kwa kubadilishana fikra na baadaye tukatoka nje tukimaliza mkutano hapo tunatoka nje tunaendelea kubishana hapo nje na mpaka sasa wamekuwa marafiki zangu.

Tatu, ninafuraha kubwa kwa viongozi, wengi maanake ninyi wote mlioko hapa ni viongozi. Viongozi wengi wamejitokeza

katika mkutano huu na kuhudhuria kwenu katika mkutano huu hakuna maana tu kwamba nyinyi mnapata kufuatilia mambo haya na kujua yameelekea wapi na hatua zilizobakia ni zipi. Lakini pia mmejitokeza ili mtakapopata habari hizi mrudi kule mnapotoka na kuzisambaza, kuwapa wengine na kuwaeleza kwamba yalio muhimu ni haya wala msikasirike kwa kuwa kiongozi wa kesho ameamua kujifanyia mazoezi yake yakifua?. (***Laughter)*** Akiendelea namna hiyo ni kwamba na sisi tutakuwa hatututatambua kwamba yeye pia yuko nasi jambo nzuri kwamba kiongozi wa kesho pia yeye yuko hapa.

La mwisho ambalo ni muhimu sana ambalo ninataka kuwapasha nyinyi, ni kwamba vizazi tofauti vimefika hapa. Tuna wazee, wanaume kwa wanawake, tuna watu wa makamu, tuna vijana na niliona watoto kama watatu au wanne na mmoja wao mdogo kabisa ndiye aliyekuwa akipiga kelele sasa hivi. Pengine si kupiga kelele ni kusema yupo.

Sasa mimi, kazi yangu fupi sana, ningeweza kuja niseme sina la kusema na naomba mnipe hii fursa nikae chini niwasikize nyinyi, lakini nadhani pengine hayo hayangewafurahisha wengi kwa sababu pengine mnataka kujua kwa undani zaidi. Kazi hii baada ya sisi kupokea maoni yenu, tulikwenda tukaifanya namna gani. Nadhani tungeanzia hapo halafu tuende katika eneo lingine ambalo ni kusema je, ikiwa kuna maoni ambayo hayamo katika mswada wa Katiba yatapatikana wapi? Je, yamepotea au yalichujwa na kama yalichujwa, yalichujwa kutumia mansisi gani? Halafu pengine tuangalie pia hii repoti fupi ambayo tumeitangaza na kuieneza, ambayo tumekuwa tukielezea watu maanake ni nini ? Halafu niwaelezee habari ya ripoti ndefu maanake ikiwa kuna ripoti fupi lazima fupi yanafanywa na mengi, sio?

**Audience:** Ndio.

**Com. Zein Abubakar:** Nikisema kuna fupi lazima kuwepo na ndefu. Sasa tofauti ya fupi na ndefu ni nini? Halafu mwisho pengine, tufanye haraka tupitie mswada huu hata wewe unaona mwenyewe pia umebeba kitabu kama hivi kwamba mswada huu ambao tunaupendekeza bado uko jikoni unachapishwa na ukishachapishwa kama alivyosema dada yangu mshirikisha wa hapa Bi. Mwadime tutawaletea na kwamba pia mtakapokuwa mkizunguka pia bado mtapata kwenye tarafa, mkifika kwenye tarafa mtapata. Mwenye kujipatia***…(Applause***) Wala msiwe na wasi wasi ama neno aliyekuwa nayo angesema. ***(Murmurs***).

Tusione vibaya wala tusilieboa sisi wa kweli wa Mombasa tunasema tuyaongoa mwenzako kwa kitabu wewe ujasiri. Vitabu hivi tutavitambaza na wakati tukivipata tunavitawanya kwa hivyo mpaka sisi ni kusema vitabu vichache tulivyovipata kutoka kwa mtu anayezichapisha, tuvigawanye sawa sawa ili katika kuzigawanya kila Wakenya wapate fursa sawa. Lakini ningependa kusema kwamba pengine nilifanya kosa kidogo kwa sababu mimi nimewaletea zaidi kidogo kuwashinda Wakenya wengine kwa sababu nyinyi mlibaandika kwamba sisi tunatumia Kiswahili na wengi hawapendi vitabu vya Kiswahili. Tukasema vile vilivyosalia vya Kiswahili ni kwetu sisi, (*Laughter*), ndio tusigawanye.

Sasa nianze pale nilipoanzia, mwisho nilisema kwamba tutakubali ….nilisema himla tutatoa ruhusa kwa watu kutoa maoni yao, kuuliza maswali na kadhalika. Ikiwa mpaka sasa tuko sawa tunaandamana pamoja, tuko sawa?

**Audience:** …(Inaudible)

**Com. Zein Abubakar:** Tuko sawa. Mnajua faida yetu ikiwa hamuitikii sijui mmeelewa au hamkuelewa. Tuko sawa?

**Audience:** Sawa.

**Com. Zein Abubakar:** Asanteni. Tulipomaliza kukusanya maoni, tulitembea mkoa hadi mkoa, wilaya hadi wilaya na tukazambaa katika kila sehemu ya uwakilishaji Bungeni nchi nzima. Sehemu mia moja na kumi, mia mbili na kumi mtanisamehe. Mia mbili na kumi. Juu ya hayo, tukawa tumepata kupitia barua na kupitia vikao maalumu vilivyowekwa katika mikoa pamoja na katika vilaya yetu kuu mjini Nairobi. Makundi na watu mbali mbali waliokuja kutuletea maoni yao either kwa maandishi ama kwa mazungumzo. Na nyinyi mmesajili kwamba tulikuja hapa au nasema uwongo mimi?

**Audience:** Ukweli.

**Com. Zein Abubakar:** Kwamba tulikuja hapa tukakaa siku mbili na baadhi yenu mlipoona pengine fursa mliopata Voi haikutosha mkatufuata Mwatate, tukakutana pia Mwatate. Au nasema uwongo?

**Audience:** Ni kweli.

**Speaker:** Hata Mbololo.

**Com. Zein Abubakar:** Hata Mbololo, Ndugu Mwangecha sijamsahau unajua hivyo. (murmurs). Tukakusanya haya maoni, tulivyomaliza kukusanya maoni kila tulipokuwa tukiyakusanya iliyofuatia tulikuwa tukiyatuma maoni haya Nairobi katika ofisi zetu kuu. Na maoni haya Mwenyezi Mungu alitusaidia tukapata ufahamu wa kuyarekodi. Sijuhi Mungu nini? Tukayarekodi ili baadaye kusije kukatokea jambo kama ilivyotokea baadhi wetu watu wa Kenya wakasema, hii Katiba mmetoa wapi? Lakini ukija Nairobi ukiwa unataka nani aliyezungumza tunarekodi yetu. Kama leo tulivyozambaza karatasi ya kusema aliyeudhurua aandike jina lake, mtu aliyekuja kutoa maoni kwanza alikuwa akijiandikisha mlango au hakuwa ajiandikishe?

**Audience:** Alijiandikisha.

**Com. Zein Abubakar:** Akishakaa ndani kulingana na alivyojiandikisha pale anaenda kuitwa kutoa maoni kwamba wewe umejiandikisha unataka kutoa maoni. Halafu ukishamaliza kutoa moani ulikuwa ukienda kwenye register yetu ukitia sahihi kwamba mimi nimetoa maoni haya bila kulazimishwa au kusulughwa na mtu, au haikiwa hivyo?

**Audience:** Ilikuwa hivyo.

**Com. Zein Abubakar:** Kwa hivyo maoni hayo yote tumeyahifadhi na kutokana na kazi yetu sisi tumelazimika kuwa ni watu ambao wamepewa jukumu la kuhifadhi maoni ya watu wa Kenya ambayo ni matakwa yao, ni maoni yao, ni ndoto zao, ni masaibu yao wanavyotaka wao au nasema uwongo?

**Audience:** Ni kweli.

**Com. Zein Abubakar:** Sisi tulipomaliza kuyakusanya tu tuliyatuma Nairobi, Nairobi yakaanza kushugulikiwa na mmoja wa watu waliokuwa wakiyashugulikia maoni hayo ni huyu ndugu yangu Bwana Ogira ambaye amekaa hapa ambaye anatufanyia kazi huko makao makuu. Akiyapokea tu uchukuliwa yakapelekwa idara tofauti, yale yaliosemwa kwa kauri, kwa kinywa, kwa mazungumzo yakapelekwa kwa watu wakaweka vizikizi vyao wakaanza kuandika kila neno linalosemwa mle. Yale ya maandishi yakapelekwa idara nyingine yakaanza kuangaliwa, mtu huyu aliyetoa maoni haya jina lake nani, ni mtu wa aina gani, ni mwanamme au mwanamke, ni mzee au kijana, amepitia kiwango gani cha elimu. Habari zote hizo tunazo, kwa hivyo wewe ukishaweka kwa mfano, kujua watu waliokuwa na wanawake kutoka Voi walikuwa wanataka nini, ni sisi kuingina kwenye computer yetu, tukaangalia wanawake, tukishaangalia wanawake tukakueleza wanawake wa Voi walisema mambo haya. Na kuna baadhi yenu mliofika mapema hapa kuiweza kupitia pitia kwa ufupi. Hii ni repoti kuhusu Voi kwa ufupi lakini tuna repoti kubwa zaidi zinazolingana na matakwa unaotaka wewe.

Kwa mfano ukitaka kubwa ni hii. Ukitaka nyingine utapata kubwa kulingana na mahitaji yako, ukiwa unataka kujua kila mtu neno alilosema Voi utapata file yako kubwa namna hii. Nadhani mpaka sasa tuko pamoja, tulipomaliza kufanya hivyo tuliweza kuanza kuchambua habari mlizotupa. Kwangu sasa tuanze pamoja na ….kuhusu jambo lenyewe, mambo gani, mambo yanayohusu na nadhani nitakuwa sisemi uwongo nikisema hapa wewe ndio watu waliokusanya hapa wakisema wanataka mabadiliko.

**Audience:** Ni kweli.

**Com. Zein Abubakar:** Mzee wangu mwenye kofia pale, yeye ndiye amepiga swali lake mpaka likasikika kwenye kila microphone. Sasa mambo ambayo yanayohusu jinsi serikali inavyotungwa tumeyaweka pamoja, kuhusu mahakama tukaweka pamoja, kuhusu watoto tukaweka pamoja, kuhusu haki za binadamu tukaweka pamoja lakini juu ya hayo tukagawanya pia katika haki za binadamu tukaweka pamoja. Lakini juu ya hayo tukagawanya pia katika hakii za binadamu, kuhusu wazee tukaweka pamoja, kuhusu wanawake tukaweka pamoja, kuhusu watoto tukaweka pamoja, kuhusu mazingira tukaweka pamoja. Kwa hivyo ukitaka kujua wewe kwa undani zaidi iwapo unapozungumzia haki, wanazungumzia katika mipaka gani pia unaweza kupata hayo.

Halafu, tukaenda Mombasa na nadhani nyinyi wengi mlifuatilia mambo haya kupitia vituo vya habari kwamba tulifika Mombasa. Na wengi wenu mnajua tulikwenda Leisure Lodge na kuna mswahili mmoja wa gazeti ambaye anaitwa Malibongo akachora vibongo vibongo kuhusu kazi yetu huko wengine wetu tumewekwa chini ya mnazi, chini wa dafu. Professor Ghai anasoma kitabu cha kibozo, mwingine anazama majini kwa sababu hajui kuogelea. Lakini nataka kutoa mfano kwa sababu juu ya kwamba tulikwenda katika hoteli ambayo ina starehe nyingi sisi hatukupumzika wala kula starehe hata siku moja. Tulifanya kazi usiku na mchana, hayawi hayawi mwisho ya kawu na waliokuwa wakisema hamtamaliza nini? Sasa tumemaliza kwa sababu watu wengi kwa wingi wao Kenya nzima walisema malizeni kwa haraka mambo haya si ya kufanyiwa taratibu Bwana. Baadhi ya wati waliokuwa wanasema sisi kwa kupenda mishahara minono minono na kuzoea kukaa katika magari yenye vono, magari makubwa makubwa tukajaribu kufanya kazi hii iende taratibu. Wanasema maswahili anayezoea nundu aachi kunona.

**Speaker:** ...(Inaudible)

**Com. Zein Abubakar:** Eeeh, namna hiyo. Akizoea atakaa tu hataki kufanya kazi. Lakini baadhi yetu tunafikiria aah, au watu wememaliza haraka kwa hivyo hawakufanya kazi hii, ni ndoto. Kabla sijaondoka hapa nitawauliza nyinyi kama ndugu zangu, kama wazazi wangu. Mwisho kabisa sitaki msema sawa. Mwisho kabisa baada ya kupitia kila jambo unieleze je, mapendekezo haya yalitoka kwenu? Usijibu sasa. Tuyajibu mwisho baada ya kuangalia mapendekezo haya yanasema nini. Tulipokuwa kikao Mombasa tulikuwa tukianza kazi asubuhi saa mbili tukimaliza kazi kawaida saa sita usiku na tulipokuwa tunakaribia kumalizia ili kupiga msako sehemu ya taarifa zetu, tukawa tukimalizia kama saa nane, saa tisa hivi. Tuliporudi Nairobi tulikuwa tukakaa usiku kucha tunapokezana … Watu wanafanya kazi, wangine wanakimbia nyumbani walale saa kama moja au mbili halafu warudi kazini. Hakuna wakati taa zetu zilizimwa ofisini, hakuna wakati computer zetu zilizimwa kazini na nasema haya ili mujue kazi kazi tulizofanya hatutaki kusifiwa sisi. Wakenya wengi sana walifanya kazi hizi mmoja wao akiwa ni huyu Bwana aliyekaa karibu na mimi mkono wa kushoto, mwingine ni huyu Bibi aliyekaa na mimi mkono wa kulia na mwenyekiti na nyinyi wote mlioko hapa. Mlikereketwa na kufanya kazi zingine tofauti isipokuwa hukuja kufanya kazi hizi. Nakomea hapo kupitia kuhusu maoni. Kama kuna mtu anataka kujua mambo mengine kuhusu kazi zetu ikiwa kwa mfano je wasaliti wako na ni akina nani. Hayo ni mambo ambayo singependa kuyaanzia, tuende hatua ya pili.

Hatua ya pili, kwa nini sisi tukachapisha taarifa kama hii inayoitwa toleo fupi? Kwanza kabisa, sheria inatulizimu sisi tuandike ripoti ndefu, katika ripoti hii ndefu tumegawanya juu zingine four volume, juu nne ambavyo zinazungumzia mambo tofauti. Kwanza tunazungumzia historia, vipi tulikuja sisi kama nchi katika mambo haya ya kubadilisha Katiba. Halafu tunazungumzia njia za kubadilisha Katiba ambako tunaozungumzia ile sheria, matakwa yake na maadhiri yeke. Kisha tunazungumzia historia ya Katiba ya zamani, halafu tunazungumzia kuchagua maoni ya Wakenya na tunatambua kongamano la mikutano tuliyoyafanya na wajuzi wa mambo ya Katiba ambayo tulifanya mengi. Tulifanya na wanaohusu wanawake, tulifanya inaohusu haki za kibinadamu, tulifnaya mkutano unaohusu majimbo pamoja na federalism na pia tulikuwa tumealika watu tofauti wenye uzoefu mkubwa katika kazi za kuandika Katiba kutoka nchi mbali mbali kuja Kenya na kufanya mazungumzo na Wakenya.

Tunatambua pia maoni hayo ili kuyafafanua Wakenya wanataka nini halafu tunaeleza katika repoti hiyo ndefu kwa nini tumeamua sisi kuunda au kubuni Katiba kutumia mtindo tuliyobuni Katiba. Halafu tunaeleza ikiwa kuna mambo yameachwa nje kwa nini yaliachwa nje, tunaeleza pia kwa ufupi kwa kila jambo kuhusu maoni ya watu, msimamo wa Tume na maamuzi yetu, inaenda hivyo. Maoni ya watu, uchagumbuzi wetu na masimamoi wetu pamoja na mambo yaliokubaliwa.

Lakini tukasema ni heri kuchapisha kwa ufupi kwa sababu ukimwambia Mkenya akae chini asome kurasa mia nane, itakuwa kama ni njama ya kumfanya kutokufahamu mnayopendekeza au si sawa hivyo?

**Audience:** Ni sawa.

**Com. Zein Abubakar:** Tukasema tuyaandike kwa ufupi katika kurasa zilizo, either mia au chini ya mia. Ukifungua kitabu hiki utaona kurasa ya mwisho inasema sabini na mbili. Kwa hivyo, tuliweza kufanya chini ya mia na tukasema ukiyafanya hivi kwa lugha fupi, lugha rahisi na kama itawezekana lugha tamu utawafanya wananchi waweze kusoma na kufahamu yale yaliokatika ile repoti lenu. Ya muhimu yote yalio katika repoti ndefu yako katika hii ripoti fupi sio fupi iwache muhimu, aah, fupi ni ya kufupisha mambo, tunaelewana?

**Audience:** Tunaelewana.

**Com. Zein Abubakar:** Sasa sawa na ripoti hii yenu ya uwakilishaji Wabunge wa Voi, fupi ndio ukikaa kama dakika ishirini unaweza ukaipitia kwa haraka na kusoma na kufahamu. Sasa nirudi katika mambo tuliyoyasikia tulipokuwa tukizunguka Kenya.

Kwanza kabisa mimi ninaamini jambo muhimu sana tulielezwa na Wakenya ni kwamba sisi tunataka kuwa taifa moja, sisi kama Wakenya tunataka kuwa taifa moja. Juu ya tofauti zetu za kikabila, za kidini, za kiika, la kihali za maisha tunataka kuwa taifa moja na kuhakikishia ya kwamba hatukwenda mahali popote Kenya, tukaambiwa sisi tunataka kujimeza tuwe kanchi ketu kadogo tofauti na nyinyi. Kila mahali tulipokwenda, tuliambiwa sisi tunataka kuwa taifa moja. Mahali pamoja tu karibu tufikie hapa eneo karibu tufikie hapo, lakini waliowasema kwa adhabu waliokuwa nazo, walituambia hivi. Tukiendelea kuonewa tunaweza kuharinia na fikra kama hizo zilikuwa zinazipenya penya katika sehemu zilozowatu wa nyuma kimaendeleo nchini na katika sehemu ambapo watu walikuwa hawaamini kwamba wao wanafaminia kama wanavyofaminia watu wengine. Wakasema, mkiendelea kutuonea tunaweza kuharinia kwa hivyo sisi tuliwauliza, kwa hivyo mnataka nini, wakatuambia. Tunataka tuwe taifa moja lakini katika taifa hili moja kila Mkenya, kila jamii ya Wakenya iwe na haki sawa ama hamkutuambia hivyo. (Applause). Hamkusema hivyo nyinyi, eeh?

**Audience:** Tulisema hivyo.

**Com. Zein Abubakar:** Wakatuambuia katika ugawaji wa rasilimali za nchi hatutaki wengine walale njaa na wengine walale katika uruo wa kualika mbwa zoa kwa nyama ya kilo kilo. (***Applause and Laughter)*** Wakasema hawataka taifa ambalo litakuwa na mamilioni ya maskini na watu wachache mamilionare. Wakatuambia, katika ugawanaji wa rasilimali watu wanaoishi sehemu fulani wawe na madaraka ya kujiamulia wao wenyewe wanataka kutumia rasilimali zao vipi. ***(Applause)*** Na sisemi hayo kuwachochea, wala sisemi haya ya kuwatia moto, wala sisemi haya kwamba ni uwongo. Wakatuambia tunataka jamii ya taifa jipya Kenya mpya ambayo itajengwa katika msingi ya haki ya kila mtu. Lakini watoto wote wawe na haki ya kuenda shule angalau elimu ya mwanzo iwe si sawa mtoto yoyote kutokuwa na uwezo wa kuenda shule kwa sababu mzazi wake hana kitu cha kumfanya aende shuleni. Sasa katika Katiba hii mpya tumesema shule ya mwanzo ambayo tunaitafsiri sisi mpaka kumaliza primary iwe ya lazima kwa kila mtoto na iwe ya bure. ***(Applause)*** Na sisemi hayo ili muzidi kunukiwa mseme mana-support Katiba hii mpya. Nasema haya kwa sababu haya tuliyapokea kutoka kwenu.

Wakatuambia, katika Katiba mpya muongoze ile sehemu inayosimamia haki za kibinadamu isizungumzie tu, kwamba haki za kimsingi lakini izungumzie haki za kimsingi ikiwemo haki za kiuchumi, haki za kijamii pamoja na haki zingine tutakazoweza kumfanya kila Mkenya aishi. Najua Mzee wangu unasema aishi je, uko Kenya. Asante kwa kunisaidia lakini wacha niendelee. ***(Laughter***) Kila Mkenya aweze kujipatia mahitaji yake ya kimsingi ya kupata mlo, ya kuweza kupata mahali ambapo ametenga kitu cha kujizuia na kukiwa na jua ama mvua pamoja, akiwa mgonjwa aweze kuenda hospitali bure. (Applause). Wala sifanyi siasa mimi, …(Inaudible)Wangeka wacha uchokozi hapa. ***(Laughter)***

Wanasema kuwa kenya kweli uhalifu umezidi, lakini Kenya kusiwe kuna haki ya kumtoa mtu hongo. Wanasema kweli uaalifu umezidi lakini mwalifu awe na haki zake hata kama umefungwa haina maana wewe utazuiwa kufanya ibada au haina budi iwe hivyo? Kwamba umefungwa usiruhusiwe hata kuabudu Mungu ndani ya jela, ni sawa hivyo?

**Audience:** Si sawa.

**Com. Zein Abubakar:** Kwa hivyo ukichunguza zaidi utaona mfungwa akapewa haki za ibada, mfungwa akapewa haki za kufanywa kama binadamu na adhabu yoyote atakapopewa mfungwa isiwe adhabu ya kupita mipaka. Ikawa mtu anayesimamia jela anakuwa kama "Mungu" …nasema Mungu anisamehe sisemi hivyo mimi lakini, mtu akiwa jela wale waliofika waliopata taabu ya kuwa jela wanajua. Ukiwa umeingia jela wewe yule mkubwa wa jela ndiye anaamua kila kitu kuhusu maisha yako.

**Speaker:** Ni kweli.

**Com. Zein Abubakar:** Sasa unapofungwa tunasema mtu akiwa atashikwa na polisi ashikwe katika mipaka fulani. Sasa tofauti kubwa kati ya Katiba hii ya sasa tunaopendekeza na Katiba ya zamani ni nini? Nataka mnisikize kwa makini. Tofauti kubwa iliyoko kati ya Katiba ya sasa iliyoko sasa ambayo unaishika mimi hapa ambayo inaelezo mia moja ishirini na saba na Katiba tunayopendekeza sisi ambayo inavitengo mia mbili tisini na nne tofauti yake ni nini? Tofauti zake ni hizi nitapokueleza sasa.

Kwanza kabisa, tumesema taifa ni watu.  Taifa ni watu.  Madaraka yote katika taifa yanatokana na nani?

**Audience:** Na watu.

**Com. Zein Abubakar:** Tumesema hivi, Katiba ya zamani haisemi hivyo ndio maana ukawa kwamba kuna utatanishi saa ingine kati ya watu na viongozi au sio?

**Audience:** Ndio.

**Com. Zein Abubakar:** Katiba inaanza na utangulizi, tofauti hiyo.  Hii ya sasa haina utangulizi inaanza tu, pu!  Inakuanzia inasema Kenya is a sovereign republic.  Pu! Inapoanzia, Kenya ni nchi huru, nani asiyejua hivyo?  Haya mapendekezo mliotoa nyinyi mjisifu jamani, kama sifa wanafaa kupewa wapewe watu.  Tunasema, 'we the people of Kenya', "sisi watu wa Kenya, aware of our ethnic cultural and religious diversity and determined to live in peace and unity as one indivisible sovereign nation. Inasema "sisi watu wa Kenya, kwamba tunafahamu tofauti zetu tulizonazo sisi za kikabila, za kitamaduni, za kidini lakini tumeamua kuishi pamoja kwa amani na umoja kama nchi moja ambayo haiwezi kumegwa megwa vipande vipande."  Inasema pia, utangulizi huu unasema "tunajitolea kuthibiti" wale waliona nakali hizi hayo magazeti mlionayo haya tuende sambamba. Mko mahali ambapo inasema preamble, isije ikawa najisemea tu mimi mwenyewe.  Jamani, mtumishi ikiwa hujapata baadaye tutakufatutia.  Mtumishi  hauawi au anauawa?

**Audience:** Hauawi.

**Com. Zein Abubakar:** Haya mambo yameandikwa kwa Kiingereza na mimi najaribu kutafsiri kwa kusimama sijafiria kitafsi kwa hivyo nikiteleza kidogo utafahamu.  Inasema, "committed to naturing and protecting the well being of the individual, the family and the community within our nation."  Tunajitolea kuhifadhi, kuendeleza na kustawisha mtu mmoja Kenya kumpa nafsi yake, familia na jamii zote Kenya.  Inasema, "recognizing the aspiration of our women and men for a government based on the essential values of freedom, democracy, social justice and the rule of law."  And there is a reason why wanawake wamewekwa mbele.  Kwa sababu katika historia yetu na katika Katiba iliyopita wanawake walituambia Kenya nzima tumeachwa nyuma, au sio hivyo wanawake?

**Women:** Ndio.

**Com. Zein Abubakar:** Nataka kusikia sauti zenu.

**Women:** Ndio.

**Com. Zein Abubakar:** Sasa katika utangulizi wanawake wamewekwa mbele.

**Women:** (*Applause from women)*

**Com. Zein Abubakar:** Haki zenu na wanaume mnapewa sawa. Tunasema tunataka kuweka matarajio ya wanawake na wanaume ambao wataweka utawala na serikali ambayo itakuwa imetiliwa msingi na kujengwa katika uhuru, demokrasia, haki na udumishaji wa sheria. Inasema, "exercising our sovereign and inalianable rights to determine the form of governance of our country and having fully participated in the Constitution making process do adopt, enact and give to ourselves and to the future generation this Constitution." Inasema hivi, kwamba, kwa sababu tuna haki yetu sisi na madaraka kama watu ambao haki hii haiwezi kuchukuliwa na mtu tunajiamulia wenyewe tutaweka utawala wa haina gani kwa sababu sisi ndio tuliounda Katiba hii kwa kuhusika katika mfumo wa kurekebisha Katiba. Na tunajichukulia Katiba hii na kujipa wenyewe Katiba hii. Na mwisho kabisa, ambao ndio mwanzo wa Katiba, mwisho wa utangulizi ndio mwanzo wa Katiba tunasema, Ewe Mwenyezi Mungu tunaomba uibariki Kenya na wanasema Wakenya wengi wao katika utangulizi wekeni mnaoweka lakini msisahahu kumtaja Mwenyezi Mungu. Au hamkusema hivyo?

**Audience:** Tulisema.

**Com. Zein Abubakar:** Sasa huo ni utangulizi, wengine Waswahili wachokozi wanaweza kukuambia ni kionjo. (*Laughter*) Lakini utangulizi huu lazima uangaliwe kama dira mnajua ile chombo kidogo kinachomwelekeza mtu safari anapokwenda, sio? Mwongozi huu katika utangulizi uangaliwe kama dhiraa ya kutuonyesha njia za kufuata katika kuweka Katiba mpya. Mtanisamea, naomba kwamba mtachoka lakini bado.

**Speaker:** Tutazoea.

**Com. Zein Abubakar:** Asante mzee wangu. Mtaitimea namwambie endelea.

Sura ya kwanza, jamani mtaniwia radhi pengine sikuwaambia na nyinyi wengine…..

**Speaker:** Ninaelewa mimi.

**Com. Zein Abubakar:** Tunakwenda pamoja, nitakuelekeza ninavyosema. Unaniamini, sio?

**Audience:** Sawa.

**Com. Zein Abubakar:** Sawa Bwana. Sura ya kwanza ya Katiba ya zamani kama nilivyokwambia inavitengo vitatu, moja, mbili, tatu. Ya kwanza inahusu Kenya is a sovereign republic, nilikuambia hiyo? Tukasema kama hujatambua jamhuri, watu wetu walivyotuambia muundo mpya utambue wapi, au si sawa hivyo?

**Audience:** Sawa.

**Com. Zein Abubakar:** Kwa hivyo sura ya kwanza ya Katiba mpya ambao mnafungua, mufungue hapo tuende zambamba. Ukiwa na hiyo gazeti inasema, chapter one. Usonge tena dada, songa mbele chapter one. Uko chapter one, ndio hiyo haya.

Inasema sovereignty of the people and the supremacy of the Constitution. Sasa pengine nikuambie tu kwa ufupi muundo tuliotumia sisi kuunda Katiba hili. Katiba hii imeweza kugawanywa katika mafungu manne, mafungu mangapi?

**Audience:** Manne.

**Com. Zein Abubakar:** Mafungu manne, tunajaribu kuifanya iwe rahisi. Mafungu hayo manne unaweza kuyagawana hivi. Fungu la kwanza inawahusu watu, linahusu jamhuiri wanaotaka kuweka watu wa Kenya, linahusu raia wa Kenya na haki zao, inahusu pia maadhili, misingi na nguzo tunazoweka zitakazosimamia watu hawa halafu tunazungumzia haki zao. Ukianza hivyo unasema fungu hilo la saba linatoka sura ya kwanza hadi sura ya tano. Refer to the first chapter to the fifth chapter you will deal with all these facts I am talking about. All of them have to do with who are the people of Kenya, the nature of the republic that we are establishing, what kind of values we have and what kind of duties and rights the citizen would have in this republic. Ukiingia wewe sura ya sita, na sisemi hivi kujigamba, utaingia katika sehemu, vipi mwananchi atajitawala na atahusika katika kuchagua viongozi. Ukitoka hapo utapita katika hali ya Ubunge, ukitoka hapo utafika katika hali ya serikali kuu na viongozi wao, ukitoka hapo utakwenda mahakama. Najua wengi wenu mnataka kuuliza swali hili la mahakama lakini tutafika huko. Baada ya hapo kutoka kwenye mahakama.

**Speaker:** Kadhi.

**Com. Zein Abubakar:** Hapana Bwana umekimbia Bwana. Ndio, uzambazaji na utawanaji wa madaraka katika sehemu mbali mbali nchini. Usipite hapo, ukipita hapo utakuwa umefanya mambo yote yanaohusu Mkenya, kuhusika kwake katika maisha, kuhusika kwake katika uongozi, uchaguzi na katika madaraka ya nchi pamoja na serikali. Halafu unaingia kwenye ardhi, ndio sasa umefika mahalii panafaa, baada ya ardhi ni nini? Mazingira na mali ya asili au si hivyo?

**Audience:** Ni hivyo.

**Com. Zein Abubakar:** Halafu public finance, halafu public service, halafu….sasa fika hapo ukishafika kwenye …..hilo ndio

kitengo cha tatu. Kitengo hicho cha tatu inahusu hizi mali zitakapogawanywa na itakapotumika pia kutoa huduma kwa wananchi na tarafa. Halafu yale yaliosalia yanahusu uwekaji wa tafsisi na njia za kuweza kutekeleza maadhili na mambo yote haya mengine tuliotaja na utekelezaji huu ni kwamba wakati wowote ijulikane kwamba Katiba inatumika. Sasa tuanze katika kitengo cha kwanza.

Kitengo cha kwanza, sura ya kwanza inasema madaraka yote katika taifa la Kenya yako mikononi mwa Wakenya. Na kwamba madaraka haya yatatumika nchini, taifa hili letu tukufu kwa kutumia Katiba, sasa tunazungumzia ukurasa mbili katika sehemu hii. Ukurasa ngapi?

**Audience:** Mbili.

**Com. Zein Abubakar:** Ya kwanza ni ukuu na umuhimu wa watu na madaraka yao, ya pili ni ukuu wa Katiba. Kwa nini tukafanya hivi? Kwa sababu Wakenya walituambia kwanza Katiba ya sasa inafanya viongozi kuwa mabwana za watu. Katiba ya sasa, it makes leaders be boses and masters of the people of Kenya. Na adhabu tunaopata sisi na hilo sawa ni kwamba viongozi wawe watumishi wa watu. (*Applause)* Hebu tulia kidogo uonje. Wanasema hivyo Wakenya na ndio tukasema lazima tutambue kama kitu cha kwanza katika Katiba ni ukuu na madaraka ya watu, ili baadaye wale walionania mbaya msije mkasema iliandikwa wazi. Ni hivyo mlituambia?

**Audience:** Ndio.

**Com. Zein Abubakar:** ….(Inaudible). Imeandikwa katika Katiba na ndio tutapewa katika kifungu ya pili. Ukuu wa Katiba, ikiwa imeandikwa kwenye Katiba lingine lote lisoloambatana na kuenda sambamba na Katiba hii halifai. Haijalishi limetoka kwa nani wala sisi tusiogope mtu huyo ana nguvu gani au mali gani ikiwa halimo kwenye Katiba halimo na halifahi kama mzee wangu anavyosema huko ndio na kutofaa huko utakuwa ni sawa na jambo hilo ambalo haliambatani. Ikiwa ni kipande kimoja kipande hicho nne, ikiwa vipande viwili vipande hivo nne, kwa hivyo tunasema nini? Mtu yeyote lazima awe chini ya sheria na …..lazima iwe chini ya?

**Audience:** Katiba.

**Com. Zein Abubakar:** Umepata Mwenyezi Mungu, mimi unasikia anasema mtu ninasababu zangu kutaja mtu, siko katika mambo ya kum-challenge Mwenyezi Mungu na wala sisemi kwamba maswada huu hauna dosari nitakuja hapo mwisho. Asiyena na dosari ni Mwenyezi Mungu peke yake au sio hivyo?

**Audience:** Hivyo.

**Com. Zein Abubakar:** Sasa sijui umezifahamu sana hizi. Sasa tumeongezea kwa juu kwamba ikiwa tutatafsiri Katiba, ukienda mahakamani au mahali popote kutafsiri Katiba. Katiba hii lazima itafsiriwe kwa kuendeleza maadhili, values zilizomo humo ndani ya Katiba, sijuhi mwanielewa. Na kuhusu utekelezaji wa Katiba hii Wakenya walituambia Katiba ya zamani mimi ningeona msifu tukisia kunaharibiwa na wahuni na mtaniwia radhi kutumia lugha kama hiyo maanake watu wanafyeka fyeka misitu hivyo ni wahuni. Mtaniwia radhi. Ikiwa ni wahuni wanafyeka fyeka misitu nikikimbia mahakamani kusema si sawa misitu unaofadhili jamii mzima kuchukuliwa na mtu mmoja au watu wachache kuifyeka fyeka na kufanya wanavyotaka wao, mahakama itanijibu. Wewe huna haki ya kuzungumza hayo unayozungumza kama nani. Wakenya wakatuambia Katiba mpya inipe mimi madaraka kama Mkenya, niende mahakamani kutekeleza Katiba him kitengo hicho ukiwa unasoma aangalia kitengo nambari sita katika sura ya kwanza.

Tusome pamoja, 'because a person or any authority interpreting the Constitution. Sio hii, angalia cha tatu, asante Bwana. Tatu kwanza, enforcement of the Constitution. 'A person may bring an action in the Court on the grounds that an enactment or anything contained in or done under enactment is inconsistent with or is in the contravention of the Constitution for declaration to that effect'. Halafu, kitengo kinachofuatia kinasema mahakama itatoa maamuzi kulingana na maombi hayo.

Kabla sijaenda mbele sana nikuambie kwa vile tumetaja mahakama hapa, Wakenya walikuwa naofu sana wanasema mahakama ilivyo sasa hata ukiandika hivi ukaenda mahakama, ukisema haki ni hii mahakama wana haki zao kwa hivyo pia lazima mahakama ipigwe msaha au si sawa?

**Audience:** Ni sawa.

**Com. Zein Abubakar:** Halafu kuna sehemu inaosema kulinda Katiba. Inasema kulinda Katiba kwa nini? Mtu yeyote, watu wowote, chama chochote, taasisi yoyote itakao ikifanya mambo yao ili kuweka mambo chini tofauti na mambo yaliondani ya Katiba watakuwa wamevunja Katiba na wamevunja sheria na watachukuliwa hatua. Na haki ya kulinda Katiba imepewa kila Mkenya, ukiangalia ambalo anapozungumzia majukumu ya raia na hiyo ni tofauti ingine kati yetu na Katiba ya sasa. Najukumu ya raia moja wao ni kwamba utalazimika wewe kulinda Katiba, ukimwona mtu au watu wanaoitengua tengua una haki ya kuenda mahakamani na kuilinda wewe. Naomba muda unakwenda pia nikimbie katika sura ya pili.

Sura ya pili hiyo tunazungumzia jamhuri si tumetoka kwa watu na watu ndio huwa na jamhuri ndio kwa hivyo mansiki inasema ukitoka kwa watu unaingia kwenye jamhuri. Katiba ya sasa sura ya pili inazungumzia uwongozi, the Executive tofauti na hili. Watu wametuambia tuitaje jamhuri sasa hufanana fafana kidogo ikiwa kuna jambo nziri katika Katiba ya zamani ….Tunaanza na kusema Kenya is a sovereign republic walivyoanza wao. Halafu tunasema the Republic is divided to the districts and several sections set out in the second schedule. Unajua Katiba ya majimbo hiyo tulikuwa nayo mwaka wa sitini na tatu ilikuwa na ufafanuzi kabisa, wilaya ni gani, mikao ni ipi, au sio?

**Audience:** Hivyo.

**Com. Zein Abubakar:** Lakini Katiba ya sasa haina mambo hayo, kwa hivyo tukasema lazima tutaje wilaya ni ipi mikoa ni ipi. Imetajwa katika second schedule halafu umuhimu kabisa ni madhumuni ya jamhuri hii, ukiangalia kitengo cha sita nambari mbili inasema the Republic of Kenya is founded on the republican principles of good governance through multi party democracy, participatory governance, transparency, accountability, separation of powers, respect of human rights, fundamental freedoms and the rule of law. Na hayo ndio madhumuni ya jamhuri hii, kwamba katika jamhuri hii kutakuwa na demokrasia, kutakuwa na demokrasia ya kushirikisha watu katika utawala, kutakuweko wazi au utenda wazi, kutakuwako na uwajibikaji, accountability principles na kutakuwako na kuheshimu kwa haki za kibinadamu na uhuru pamoja na kuweka au kudumisha sheria. Hiyo ndio madhumuni ya jamhuri, kwa sasa hatuna katika Katiba ya sasa au si madhumuni mazuri hayo? Lakini katika kutaja mikoa na wilaya nimewaguzia kwa sababu hiyo inawahusu watu wa Lamu. Na amini usiamini Katiba ya sasa haitaji mipaka yetu, mipaka yetu ya kimataifa Katiba ya sasa haitaji na sisi tumekata mipaka yetu in details. Ukifungua schedule huku utaona tumeweka details za mipaka yetu, au si sawa hivyo?

**Audience:** Ni sawa.

**Com. Zein Abubakar:** Tumesema pia haki zetu sisi kama Wakenya, kumiliki mipaka yetu hii ya kimataifa pamoja na mipaka yetu ya ndani hakuna mtu yoyote anayeweza kuiondoa isipokuwa kwa mujibu wa sheria za kimataifa pamoja na Katiba hii. Halafu, ukiangalia kitengo cha nne kinasema every citizen has the right and duty to defend the republic against any person who threaten the political independence, territorial intergrity or Constitutional order of the republic by unconstitutional means. Sijuhi mwanielewa?

**Audience:** Tunaelewa.

**Com. Zein Abubakar:** Haya. Na haya mengine ni madogo madogo. Amini usiamini, Katiba ya sasa haitaji hata mjii Mkuu wetu ni nini lakini sisi tumetaja kwamba miji wetu mkuu ni Nairobi. Unajua kwa nini tumeweka pale, kwa sababu tunataka kuipa mji mkuu huu kazi, inatakiwa kufanya nini? Kumpa mji mkuu huu kazi inayostahili na kama rasilimali za nchi nzima zilitumika kujenga mji huu lazima upewe hali ya kitaifa isije ikiwa na watu wachache wanasema mji huu ni wetu si ya watu wa Kenya au si sawa hivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Zein Abubakar:** Halafu tunasema katika kitengo kinachofuatia kuhusu mji mkuu. Najua mna hamu ya hayo.

**Speaker:** Ndio.

**Com. Zein Abubakar:** Haya wacha nimpe fursa azigawe hizo. Watu wa nje maskini huwa wanasahauliwa. Watu wa nchi suburini huko yaja yaja, subiri pahali ulipo. Ngoja, akipata mmoja katika na wewe lazima mu-share jamani. Someni wawili wawili ama watatu watatu.

**Speaker:** Watu wa nje mmepata?

**Com. Zein Abubakar:** Nakuambia ukweli mtu wa nje ingekuwa wewe hata nisipopata nitatega sikio. Naomba munipe fursa niendelee. Jamani tunafanya bidii kuzigawa hizi zitakuja lakini mtusikilize. Mzee wangu, wacha nikuambie mambo ya haki, kwanza haki huanzia nyumbani. Aliyefika hapa asubuhi mapema ndio aliyepata fursa ya kwanza kujigawia na wewe pia ulihusika katika kuzigawa. Watu wa hapa Voi ndio walizigawa au si kweli?

**Audience:** Kweli.

**Com. Zein Abubakar:** Sasa tuendelee. Amini usiamini, Katiba yetu haizungumuzii lugha. Sisi tunasema katika Katiba hii mpya, mapendekezo yetu kulingana na maoni yenu kwamba lugha rasmi ziwe mbili, Kiswahili na Kiingereza. Kwa nini tumesema hivyo? kwa sababu Wakenya wametuambia ingawa Kiswahili ndio lugha yetu, ukienda maofisini mwa serikali na katika ofisi na katika rekodi za Bunge, hupati maandishi ya Kiswahili na Mbunge wako akaamua aseme Kiswahili ndio aweke maneno yake yatatafsiriwa kwa Kiingereza kulingana na Katiba ya sasa na je tunasema hivi kuanzia sasa ni nyaraka yoyote iliyo rasmi sijuhi mnanielewa?

**Audience:** Ndio.

**Com. Zein Abubakar:** Ni nyaraka yoyote iliyo rasmi lazima iwe kwa Kiingereza mara ya pili. Kwanza lazima iwe kwa Kiswahili, ndio nakuambia mara ya pili Kiingereza ningekuwa nyuma. Kwa sababu ningesema vizuri sana Kiswahili. Ukisema pia…. Wewe unaweza kujisomea kwanza kwa Kiswahili kinasema nini halafu ndio Kiingereza kipya. Kama Kiswahili kilianza humu humu, kilichokuja na meli lazima kiwe nambari mbili, au si sawa?

**Audience:** Sawa.

**Com. Zein Abubakar:** Tukaona kwamba hali hii ya Kiswahili haijatosha tukasema endelea, tukaendelea tukasema Kiswahili kiwe lugha ya taifa. *(Applause)* Halafu tukaona hapo pia hautoshi, ukiangalia katika lugha kitengo cha nambari tisa sisi siku hizi tunaita articles na section. Kitengo cha nambari tisa sehemu ya tatu kinasema, the State shall respect and protect the diversity of language of the people of Kenya and shall promote the development and use of Kiswahili, indigenous languages, sign language and Braille, mnaelewa? Lugha zote za Wakenya zinalindwa kikatiba na dora inajukumu ya kujiendeleza na kuzihifadhi

ikiwemo lugha ya ishara. Imekuwa kwamba wenzetu ambao hawasikii akienda mahakamani ana……(Inaudible).

Tunamjua mwengine amefungiwa tu akawa hajuhi wanafungiwa makosa gani? Kwa hivyo ikiwa wewe husikii, utasomewa shtaka lako kwa ishara, ni haki yako ya kikatiba. Najua kweli utapewa Braille. Tukiwazungumzia haki au hamkisikia watu walemavu wakituambia hivyo?

**Audience:** Tulisikia.

**Com. Zein Abubakar:** Halafu tunaingia kuhusu dini na dola. State and religion si dini na dora za kimarekani, dola maanake ni State. Tunasema dora na dini zitawekwa tofauti, sijuhi mnanielewa?

**Audience:** Tunaelewa.

**Com. Zein Abubakar:** Wakenya walituambia Bwana tukizunguka, kuna mwingine anasema Bwana mimi nafanya ibada yangu siku ya Sabato au hamkuwasikia nyinyi?

**Audience:** Oh, yes.

**Com. Zein Abubakar:** Sisi tunafanya dini yetu siku ya Sabato, Mwenyezi Mungu alituambia tuitenge siku hiyo kwa minajili ya kuabudu yeye halafu kuna watu wanawasumbua walikuwa kadikadi kwa kufanya ibada zetu. Kwa hivyo, tumesema dini na dora ziwekwe mbali mbali na hakuna mtu atakayelazimisha mwenzake kufuata dini fulani na kwamba kutakuwa dola yetu itakuwa haina dini maalum. Lakini ukienda mbele usione tumekunyima haki yako una haki za kidini, kuna haki za kidini tumezitenga vizuri kila mtu awe na haki ya kuabudi ya kufuata ibada zake lakini usiniulize je, wakitaka kuabudi shetani, haikubaliwi katika Katiba hii.

Sasa tukimbie tuenda chapter three, hebu niambie saa ngapi? Jamani naoni hizi mbio tunataka, je mnaniruhusu niende mbio zaidi?

**Audience:** Ndio.

**Com. Zein Abubakar:** Nikate kate sasa kidogo?

**Audience:** Sawa.

**Com. Zein Abubakar:** Haya. Ningemwomba Chief Shabaan aende kumuona Bwana D.O. Chief Shabani kama yuko hapa

Bwana DO anakuhitaji.

Tukimbie tuende katika mambo yanayohusu maadhili. Ukianza kitengo cha maadili nataka uangalie kumi na nne, national goals, values and principles. Uangalie kitengo nambari tatu, hapo ndio mambo inaanzia hapo. Kitengo hichi kinasema the republic shall recognize the diversity of its people as per the cultures of its community, sawa?

**Audience:** Sawa.

**Com. Zein Abubakar:** Inasema, " the republic is based on principles of democracy and shall promote the participation of people in public affairs to facilitate the sharing and devolution of powers", sawa?

**Audience:** Sawa.

**Com. Zein Abubakar:** Halafu mnaenda hivyo, tunazungumzia katika maadhili haya kuhusu haki za wananchi na sababu za wananchi kuhusika katika mambo ya uma na vipi dola inalazimika kutambua tofauti zetu na kuheshimu makabila yote. Lakini katika mambo muhimu katika sehemu hiyo, nakuomba usome kitengo nambari kumi na mbili. Kinasema hivi, "the State shall impliment the principles that one third of the members of all elective and appointive bodies shall be women." (*Applause from women)* Inaambiwa dola kwamba hakuna kura itakuwa halaki, mtambue watu isipokuwa katika hawa waliochaguliwa theluthi moja kati ya tatu, theluthi moja wawe wanawake lazima na hakuna taswishi yoyote itakaoundwa za dola au na serikali au na …ambayo theluthi moja haitakuwa wanawake. Unajua kwengine watu wengine wanasema ikiwa hesabu za Wakenya zinaonyesha kwamba wanawake ni wengi zaidi kidogo kuliko wanaume sisi tunawapa theluthi moja. Tunasema hii hatua ya mwanzo sijuhi kama mnanifahamu. Haya tuendelee.

Ukiangalia kitengo nambari kumi na saba, samahani tuanzie kitengo cha nambari kumi na sita. "The republic shall recognize its responsibilities to future generations of Kenya by persuing politicis for the sustainable management of the environment." Tunasema si sawa tu kizazi kimoja kuwa na haki kati ya kizazi hicho, lazima wakati wowote vizazi vyote viwe vinafikiria hivi vizazi vya siku zinazokuja. Na katika utumishi wetu wa rasilimali na mali ya asili tuwe tunayalinda ili vizazi vinavyokuja pia wapate kuwa na faida katika mambo haya kama tunavyopata sisi. Kwa hivyo tumeenda mbali zaidi tunasema nini, si haki tu baina yetu lakini haki ya yule mtoto aliyekuwa akilia hapa na haki ambao pia wale waliotajwa na Mwenyezi Mungu lakini hawajazaliwa, au hamkuamini hivyo?

Halafu, tuseme katika hicho kitengo cha kumi na saba, hicho kitengo cha kumi na saba kinasema the republic shall be a good citizen of Africa and the world. Haja ya sisi kuwa raia wema tu Kenya, lakini nchi yetu isidharauliwe tena katika mikutano ya kimataifa. Afrika na katika mataifa halafu ukiangalia kitengo nambari kumi na nane tunampa Rais wajibu sijui umeshakiona?

**Audience:** Ndio.

**Com. Zein Abubakar:** Madaraka mara moja, kila mwaka. Kila mwaka lazima Rais aje aitubue taifa kupitia Bunge. Aende Bungeni kwenye wawakilishi wa watu aeleze tumesikia wapi ili kutekeleza maadili haya kama taifa. Haifai tu kuyaandika lakini kila mwaka, kwa hivyo itahitajika mara moja kule katika Bunge ili kueleza tumefika wapi. Ka nini tumesema hivyo, kwa sababu mnajua mambo haya mengine hayajafanyika kwa siku moja, huu ni msingi. Tutahitaji muda ili kuingiza Katiba hii itendeka na itufanyie haki wote lakini kila mwaka Rais anawajibu kuja kueleza tumefikia wapi halafu mambo yanayofuatia ni wajibu wa raia. Kwanza kabisa raia anawajibu kuifahamu Katiba yake au hamkusema hivyo nyinyi?

**Audience:** Tulisema.

**Com. Zein Abubakar:** Na tumesema kwamba Katiba itafunzwa shuleni. Halafu tunasema anawajibu wa kuitii Katiba na kuilinda Katiba halafu, awe na haki ya kupiga kura na wajibu huo, ukiwemo wajibu wa kuhusika katika mambo mengine yanayohusu siasa. Awe na wajibu wa kuhusika katika kufanya kazi, tumeelezwa na Wakenya wengine hatutaki Wakenya wazembe, hatutaki Wakenya wavivu. Ikiwa kila mtu atafanyiwa kazi, Wakenya wanataka kufanya kazi. Awe na wajibu wa kufanya kazi, wajibu wa kutunza familia yao au si sawa hivyo?

**Audience:** Sawa.

**Com. Zein Abubakar:** Akina mama wametuambia Kenya mzima, siku hizi na akina baba muniwie radhi sisemi haya kwa kutokuwa na nidhamu lakini akina mama wanasema kuna wazazi wengine wakiume wanaterekesha familia zao na hawaangalii watoto.

**Audience:** Ni kweli.

**Com. Zein Abubakar:** Kwa hivyo hiyo ni wajibu wa kila raia kuchunga familia zao. Halafu, ukiendelea kuna mambo mengine ya kufanya tuwe nchi moja, kuendeleza umoja, halafu ukiangalia sana utaona pia kila raia ana wajibu wa kulipa kodi au si sawa hiyo?

**Audience:** Ni sawa.

**Com. Zein Abubakar:** Kama tunataka kujenga taifa nzuri si kila raia alipe kodi?

**Audience:** Ndio.

**Com. Zein Abubakar:** Naona watu wengine wakianza kutetemeka na kuanza kufikiria tuaanza kuwafuata kikoloni vile zamani, watu waanze kuulizwa wewe unasema umelipa kodi ama huyu angelipa kodi. Ukiwa ukinunua kitu hata ukinunu pakiti wako ya unga wa pembe unalipa kodi au si hii si kodi?

**Audience:** Tunalipa.

**Com. Zein Abubakar:** Nafahamu Bwana. Tunasema kodi ukiangalia katika public finance kule, na hali ya kutoza kodi tumewawekwa mipaka na hili ni jambo muhimu kufahamu wewe. Hakuna ofisi tuliyoiweka ambayo haikuwekea mipaka, sijuhi mnanifahamu? Hakuna haki iliyotolewa bila kuwekewa na majukumu, haki bila majukumi ni uwanja wa fujo na hakuna kiongozi au ofisi ya kiongozi tuliyoweka bila kumwekea malengo na sababu ya yeye kuwekwa pale na utumishi wake na mipaka yake.

Ukikimbia katika sura ya nne inahusu uraia, hiyo inaendelea mpaka kitengo cha ishirini na nane. Mambo muhimu ya mimi kusema katika uraia ni nini? Kwanza tumeondoa maonevu waliowakifanyiwa wanawake kuhusu uraia. Wanawake walilalamika kwamba katika Katiba ile ya zamani, mwanamme akioa mwanamke ambaye si Mkenya mwanamke yule an haki ya kuwa Mkenya, lakini mwanamke Mkenya akiolewa na mtu ambaye si Mkenya mtu huyo hana haki ya kuwa Mkenya. Kwa hivyo sisi tumesema haki sawa, ikiwa mwanamme anaweza kumpa mkewa ambaye si Mkenya haki ya kuwa Mkenya hata mwanamke Mkenya ambaye ataolewa na mwaname ambaye si Mkenya ana haki ya kumpa. (***Applause)***

Tumesema pia, mwanamke Mkenya katika Katiba ya sasa, akiolewa akiwa nje akapata mtoto, mtoto yule akija naye hapa hatasimamishwa na kuambiwa wewe si Mkenya lakini sasa hakuna tena hayo. Ukiwa na mtoto wako wewe kama mzazi moja tu Mkenya mtoto wako anaweza kuwa Mkenya, sijuhi mnanielewa? Halafu, nikuelezee kitu kidogo kuhusu mambo ya uraia, mambo mawili. Mtoto ambaye wewe utasema huyu hukumzawe lakini unataka awe Mkenya awe mtoto wako wa kulea….

**Speaker:** Hebu tulia kidogo tafadhali.

**Com. Zein Abubakar:** Asante Bwana. Nasema wewe Mkenya wewe unataka kumlea mtoto ambaye si Mkenya awe mtoto wako mlezi ambaye hajapita miaka kumi na nane, inalo wazi watu …… una haki hiyo kama Mkenya bora awe chini ya miaka ya kumi na nane. Pia tumesema katika mazingira haya ukiwa kuna mtoto ambaye hajulikani watu wake, watu wake hawawezi kutambulika na anaonekana kama ana miaka minane na ikiwa mtoto huyu hana uraia mwingine wa nchi nyingine, mtoto huyo atakuwa Mkenya. Tuna haja ya kukataza mtoto huyu?

**Audience:** Hatuna ni sawa.

**Com. Zein Abubakar:** Na sababu ya kusema akiwa anaonekana ana miaka kama minane ni kwamba kwa sababu akishatimiza miaka saba mtoto anahitajika kuenda wapi?

**Audience:** Shule.

**Com. Zein Abubakar:** Akiwa hana mtu wake tunamchukua tunampeleka shule sisi kama taifa. Halafu lingine ambalo linafaa mjue kuhusu uraia kuanzia sasa ikiwa mapendekezo haya mtakubali kwamba ni maoni yenu na yanafaa kwa Katiba mpya hakuna mtu wala kasisi au chama, au group lolote lanaweza kunyang'anya mtu uraia wake. No one can take away your citizenship, the only way your citizenship can be taken away is if while you were applying for your citizenship you used fraudlent means. Njia moja tu ndio unaweza kutumika kukunyanganya uraia wewe. Ikiwa unapotuma maombi yako ya kuwa raia ulitumia uwongo, udanganyifu, ukadanganya wewe ni Mkenya na kumbe si Mkenya tunaweza kukunyanganya Ukenya. Lakini ukiwa Mkenya wewe mzaliwa hakuna mtu anaweza kukunyang'anya Ukenya wako. Uniulize mimi swali, je wewe ukaenda Waswahili wa Mombasa wanasema kutarasa kutafuta riziki unaenda kutarasa katika nchi ya nje kutafuta riziki, halafu kuwe kuna vijana wengi ambao ni watoto wenu wameenda Amerikani na wengine wako Wingereza, Ulaya kutafuta riziki atatumbukiwa kupewa uraia kule anapoonda uraia huo utafanya mishahara yangu iwe minono na nitapata faida fulani ndani yake. Ikiwa yeye alifanya hivyo na nchi hiyo inasema lazima uwache Ukenya wako ndio uwe raia wa huko yeye akitoka na huko akitaka kurudi Kenya atazuiwa, la hasha. Je, Mkenya akizaliwa mpaka atakapokufa.

Ingine tunasema nini? Tunaruhusu kuwa raia wa nchi zaidi ya moja ukiwa wewe ni Mkenya lakini katika mipaka fulani tutakaokuweka na Bunge ili wewe ukiwa mtoto wako ameenda kusoma nje na amepata funzo ya vyoo ukiwa wewe ni raia wa huko na kwenu utapunguziwa kitu hiki na hiki unaruhusiwa kuwe kule, raia wa nchi mbili. Lakini tunasema ukiwa Mkenya wa nchi mbili unapewa haki lakini unapewa na majukumu na unaweza kunyimwa haki kidogo si nyingi. Hamuwezi kukubali ili Rais wa Kenya awe raia wa nchi mbili au mtakubali hivyo?

**Audience:** La.

**Com. Zein Abubakar:** Au kiongozi wa hali ya juu awe ni Mkenya na ni Mganda na tunasema ukiwa unataka kuwa dual citizenship kuna mambo mengine kidogo ambayo yatakubumbuzi wewe lakini uyakubali mwafaka unataka kuwa wa nchi mbili na najua bahadhi yetu tuna ndugu zetu hapa jimbo hapa Taveta kwa kwanza au pili?

**Audience:** Ndio.

**Com. Zein Abubakar:** Unaweza kuwa na haki ya kuwa Mtanzania na Mkenya , sijuhi mnanielewa?

**Audience:** Ndio.

**Speaker:** Na ukitaka ku-renounce...(Inaudible)

**Com. Zein Abubakar:** Inasema hivyo, ukitaka ku-denounce wewe useme mimi sitaki tena kuwa Mkenya nani atakulazimisha, tutakufunga kamba au vipi? Lakini kwa vile sisi ni watu wenye, sisemi sisi kama Tume sisi Wakenya. Nikuambie sisi Wakenya ni watu wenye roho safi tunasema juu ya wewe kuchagua kutokuwa Mkenya ukaenda kule dunia ikakupiga kibodo ukataka kurudi kuwa Mkenya uzuiliwi hivyo. (*Laughter)*

Sasa mimi namba kwa vile wewe pia umeomba sana nifanye mbio zaidi. Kwanza tumeamua kulingana na maoni ya Wakenya kugawanya uongozi wa taifa, tuanze na mkodo wa Bunge. Bunge tumeligawanya mara mbili, sawa jamani?

**Audience:** Sawa.

**Com. Zein Abubakar:** Bunge tumeligawanywa mara mbili kuna Bunge la juu na Bunge la chini. Si kusema wa juu ni bora kuliko wa chini, ni sawa tu ni katika njia ya kutofautisha. Bunge la chini ambalo tunalita National Assembly tunasema Parliament, the way we define Parliament. Parliament will consist of the National Assembly ambayo tunaita Lower House and the National Council ambayo tunaita Upper House. Na nitakueleza kwa nini tumefanya sababu ya kugawanya Bunge mara mbili, lakini kabla ya kuenda hapo tuanze na Bunge moja. Sehemu ya uwakilisha wa watu, sehemu ya chini. Tumesema hivi katika kuwateuwa hawa Wabunge tutatumia sehemu zilizoko sasa za uwakilishaji Bungeni, sawa.

**Audience:** Sawa.

**Com. Zein Abubakar:** Sehemu ya uwakilishaji bungeni ziko ngapi?

**Audience:** Mia mbili na kumi.

**Com. Zein Abubakar:** Mia mbili na kumi lakini tuna.

TAITA TAVETA TAPE II

**Com. Zein Abubakar:** Ngoja Bwana mambo ya ………..(Inaudible) yatakuja, lakini Bwana haongoji anasema je anasema ana uwezo wa kuongoza waziri mkuu? Anaweza kupendekeza tu huko bungeni, bunge litapiga kura. Bunge likikataa kumfuta, Waziri Mkuu anaendelea.

**Audience:** Eeh.

**Com. Zein Abubakar:** ……………….(Inaudible).

**Audience:** Eeh.

**Com. Zein Abubakar:** Tumpe nguzu na ujitoe kidogo, tumpe………..(Inaudible) mambo yalivyokuwa katika zamani. Hata huyo Waziri Mkuu ametoa vikapu. Sasa Wazari Mkuu ndiye atakaendesha serikali. Kwa nini Waziri Mkuu? Kwa sababu bungeni ndio kuliko wanakilishi wa watu, mmenielewa?

**Audience:** Eeh.

**Com. Zein Abubakar:** Waakilishi wa watu wako bungeni, sio?

**Audience:** Yeah.

**Com. Zein Abubakar:** Waziri Mkuu yuko bungeni akiwa anafanya mambo yake, wawakilishi wa watu watamuuliza haya mambo unayafanya kivipi? Kwa nini? Kwa sababu gani? Kumfaidi nani? Mambo yale ataulizwa bungeni, hivi leo Rais anaweza kumuuliza mambo hayo?

**Audience:** Hapana, wanamwogopa.

**Com. Zein Abubakar:** Na ukisema Rais tumesema Rais kwa vile tunafanya ni Rais na awe ni ishara ya utaifa wetu, the symbol of our nationalism our nation the uniting symbol of our nation, ukimfanya yeye kwamba ni anawakilisha utaifa wetu, halafu umsikie tena kwenye siasa za kurugana, ni sawa hivyo?

**Audience:** Hapana.

**Com. Zein Abubakar:** Na anatupaka matope.

**Audience:** ……………(Inaudible).

**Com. Zein Abubakar:** Ni nani atamueshimu. Ndio tukasema as a national symbol, madaraka yako ni haya, lakini undeshaji wa serikali lazima urudi kwa waakilishi wa watu ili watu waweze kuhojiwa, unafanya haya kivipi? Kwa nini? Kwa faida ya nani? Ya taifa au ya watu binafsi? Ya watu wengi au watu wachache? Halafu tunasema nini? Tunasema hivi kwamba, huyu Waziri Mkuu atakuwa na Waziri Wakuu wawili wadogo wasaidizi wawili, mmoja atashughulikia mambo ya serikali na mmoja atashughulikia mambo ya bunge, sawa?

**Audience:** Sawa.

**Com. Zein Abubakar:** Halafu tunasema huyu Rais atakuwa na Makamu wa Rais, na Makamu huyo wa Rais lazima awe mgombea mwenza, sijui kama mnanielewa?

**Audience:** Tunakuelewa.

**Com. Zein Abubakar:** Mgombea mwenza, maanake nini? Maanake you will be a running mate, sijui atakupokuja kuchaguliwa kuwa Rais, atakuja kwako na kukuomba …………..(Inaudible) amejikata mkono na makamu wake, ndio muangalie vizuri, hawa wanafaa au hawafai.

**Audience:** Ndio.

**Com. Zein Abubakar:** Na ukishamchagua Makamu wa Rais, Rais hana haki ya kumfuta, kwa hivyo nasema Rais achunge, aifikiri kwa muda mrefu na kama anaamini Mungu ambayo inafaa, amuombe Mungu kwa mda mrefu kabla hajamchagua mgombezi mwenza. Manaake tukishamchagua ………..(Inaudible) haki ya kumchagua ama haki kumnyanganya. Tunasema ni haki sio?

**Audience:** …………………(Inaudible).

***(A lot of noise from the audience).***

**Com. Zein Abubakar:** Ndugu yangu ngoja, ngoja ndugu yangu, ngoja ndugu yangu, najua wawe, sikiza ndugu yangu, najua wewe unataka kwenda na mimi nyo, nyo, ngoja, ngoja, na hamuwezi kwenda nyo, nyo, nyo, unayotaka wewe kwa sababu nyinyi haya nimekwama katika kuyaunda, sasa nitakupa fursa pengine unataka kuuliza nitakachosema sasa hivi ngoja tu. Lakini ikiwa nimekupoteza kabisa nikuunge mkono then nitapiga fulstop, nifunge breki halafu nirudi nyuma nijue nimekuwa sawa. Sawa?

**Audience:** …(Inaudible).

**Com. Zein Abubakar:** Sasa, sasa niende kwenye baraza la Mawaziri na najua hiyo, hilo niliongea na wengine. Tunasema Waziri Mkuu atateua baraza la Mawaziri ambalo lazima liithirishwe na bunge. Na tunasema hana haki ya kuchagua Mawaziri kutoka bungeni, na kwa sababu nyinyi niwaambia kwamba tatizo kubwa lililoko sasa kuhusu baraza la Mawaziri ni mambo haya yafuatayo:-

1. Kwamba Mawaziri hawachaguliwi kutokana na uzoefu wao wa kazi, elimu yao au ujuzi wa mambo, au hamkusema hivyo jamani? ***(Clapping from the audience).***

**Audience:** Tulisema.

**Com. Zein Abubakar:** Mkasema mnataka Mawaziri wenye uzoefu wa kazi, elimu inayoambatana na kazi anayopewa. Sio Mwalimu kufanywa ndio wanasimamia madaktari, au Madaktari kusimamia Waalimu. Tunasema mtu anayefahamu mambo anayoyesimamia.

**Audience:** Kweli.

**Com. Zein Abubakar:** Hilo ni jambo la kwanza, mkasema ni tatizo hilo.

**Audience:** Kubwa.

**Com. Zein Abubakar:** Pili mkasema watu wanachaguliwa sababu either ya kuwafuata unyounyo, uviongozi na kuwaokota kama wale, mnajua kuna tofauti wa mbwa na mtaniwia radhi kutumi tafsiri hii. Kuna tofauti wa mbwa, mnajua vile vijibwa vidogo vile vina vinavyozaliwa ambavyo havina elimu ya kufanya mambo yako bila kujua, akisha zaliwa hajui ni paka, sio? Ndio mkaweza kumwekea vipaka, sasa kile kijimbwa kidogo kinakufuata kila mahali sio? Sasa wanasema viongozi wanaochaguliwa Mawaziri ni wale wanaowalamba viatu viongozi. ***(Laughter from the audience).*** Sycophants kwamba unachaguliwa kulingana na wewe ndio unajua kuimba sifa za kiongozi au hujui. Kuna watu wasiochaguliwa ……………(Inaudible) si semi mimi bwana, mkitaka ripoti tutawawekea msikie kwa masikio yenu na wengine kulisikia ndipo kuwa mmekaa, kwamba achaguliwa mtu hata kusoma hajui, anambiwa Mzee tia sahihi hapa, hajui hati kutia sahihi kujifunga au kujifungua.

***(Laughter from the audience).***

**Com. Zein Abubakar:** Zingine mliotuambia nyinyi, mnasema akiteuliwa mtu kuwa waziri hatumuoni tena katika sehemu ya uakilishaji bungeni. Na pia tumuuliza mbona hatukuoni tena? Unasema bwana nina madaraka mengi mimi taifa linanitegemea kama waziri.

Tena mmumetuambia nyinyi, kwamba siku zote……….(Inaudible) na maendeleo ikiwa maendeleo yatafika mahali basi, Waziri huyu anatumia uaziri wake vibaya kuyaondoa mendeleo sehemu ingine ili kuyaleta pale, ili aweke mandeleo kwake kwa kutumia njia za ufisadi, nyinyi ndio mmetuambia.

**Speaker:** Ndio sababu barabara wanasema heka ngapi?

***(Laughter from the audience).***

**Com. Zein Abubakar:** Kuna kujana hapa, anataka niingie kwenye siasa lakini nakataa. ***(Laugher from the audience).*** Ninaposema mimi sio mwanasiasa Bwana.

**Speaker:** Ni ukweli.

**Com. Zein Abubakar:** Siasa unakumbuka tukizingumza hayo niwaambia siasa, mimi nasema ya sadfa yaliyo na uhakika . ***(A lot of noise from the audience).*** Sasa ngoja, ngoja ……………(Inaudible) mnajua tutakaa hapa siku nzima mda unakwenda ……(Inaudible). Nasema hivi, mmetuambia hivi pia, kwamba saa ingine mtu akiteuliwa Waziri, hasa kama yeye ni kiongozi vibaya, kutumia madaraka ya uaziri kuangamiza watu wanaopinga yeye.

**Speaker:** Eeh…………(Inaudible).

**Com. Zein Abubakar:** Ukiinua sauti anakuitia polisi, au sio? Basi tukasema kulingana na maoni haya ya wenge wa Kenya, wacha mawaziri wasio wabunge. Mawaziri wateuliwe kutoka inje, na mawaziri watueliwe kulingana na uongozi wao wa kazi lakini sio uramali wake.

Halafu tukasema hivi, wala si jambo la kwanza hivi kwangu. Watu wanasema ni jambo la kigeni, je Mkuu wa sheria wa sasa, ni Waziri?

**Audience:** Hapana.

**Com. Zein Abubakar:** Lakini anakaa bunge hakai?

**Audience:** Anakaa.

**Com. Zein Abubakar:** Kwa nini anakaa bunge? Ile aulize maswali, na hawa watakaoteuliwa kuwa mawaziri watakaa bunge, na kuitwa na wabunge, na kuitwa makamati za bunge ili kuhojiwa wanaendesha vipi kazi zao.

**Audience:** Ndio.

**Com. Zein Abubakar:** Wakiteleza wataitwa na waulizwe maswali wakishindwa kuyajibu watahukumiwa. Mtoto urudi bado

mchanga Bwana. Na akifanya makosa makubwa bunge linaweza kumwuondoa. Mimi nina haki ya kumpigia kura tusipokuwa na imani ya waziri huyo, au ikiwa waziri huyo amepiga mipaka ambayo Waziri Mkuu aliyeruhusu pia Waziri Mkuu utampigia kura ya kutokuwa na imani na yeye, mkamwondoa. Halafu tumeambiwa na Wakenya, hili ni jambo muhimu sana, ili kufanya siasa za bunge, parliamentary politics, lazima kuwe na tofauti kati ya serikali na wabunge. Hivyo sasa ada na desturi na historia yetu inatufunza, Rais anaweza kuteua mazawaziri atakavyo, thelathini, arubaini, hamsini, sitini na wao wasivuke tisini maanake ni, ukichagua Mawaziri, Mawaziri thelathini na wafuasi wao wawili wawili, maanake tisini, sio?

**Audience:** Ndio.

**Com. Zein Abubakar:** Na wote mawaziri. Sasa ukileta kura ya ya kutokuwa na imani na serikali, waziri huyo anaweza kuipigia serikali, kuikataa ama atawapinga nyinyi mnaopinga nyinyi serikali.

**Audience:** ……………………..(Inaudible).

**Com. Zein Abubakar:** Ndio sababu ingine muhimu ya kutokusanya, Mawaziri wawe wabunge, kwa sababu wabunge wanatakiwa wao, wawe waziri ni wa watu. Sasa moyo waka umetawanyika kati ya kulinda watu na kulinda serikali utakuwa umelinda watu kweli?

Tumesema kikatiba Waziri Mkuu yeyote hawezi kuchagua mawaziri zaidi ya kumi na tano. Nchi yetu maskini jemani.

**Audience:** Jameni.

**Com. Zein Abubakar:** Fedha za kuchezea hatuna hapa. Kwa hivyo wasizidi kumi na tano, akitaka kuchagua watano hiyo ni jukumu lake, na akishindwa kufanya kazi tutamuondoa. Na asiwe na Naibu wa Waziri zaidi ya mmoja, zaidi ya mmoja kwa nini? Haya tuliyapata ya kwanza kwa watu, halafu kuhusu kazi za hizi bunge mbili, nirudi back.

Kazi za hizi bunge mbili, kwanza kabisa Wakenya wametuambia hawataki kuweka viongozi ambao hawawezi kuwaondoa, …………..(Inaudible).

**Audience:** Ndio.

**Com. Zein Abubakar:** Wengine walisema we must have a right to recall, sio?

**Audience:** Eeh.

**Com. Zein Abubakar:** Ikiwa mtu amechaguliwa na ni mzembe, ikiwa mtu amechaguliwa na akahama mji, ukamchagua akahamia Nairobi hataki kurudi tena. Akipita katika magari atawarushia mkono tu, kwa kwamba hakuna njia ya kumrudisha mtu huyo. Katika katiba mpya, watu waliopiga kura asilimia thelathini wanaweza kwenda kwenye tume na kuanzisha mashtaka yatakamwuondoa huyo. Tume itafanya uchunguzi na ikiwa uchungi wake una ahakika huyo mtu ataondolewa, kazi yake itafungwa. Lakini kufutwa kwa kazi hakuhusu kwa wabunge peke yao, tutafuta mpaka Waziri Mkuu, mpaka Rais. Kwa mfano, Rais akienda kinyume la kiapo alichokula cha kutengeneza wajibu wa Katiba tuna haki ya kuomwuondoa au hatuna?

**Audience:** …………………………(Inaudible).

**Com. Zein Abubakar:** Kama amerudi katika bunge hizi mbili na kazi zao. Ananikumbusha bunge la pili ni kutaja nani atakuwapo, na nilikuwa nitakuja ku.. msiwe na haraka.

Bunge la pili la juu, tutachagua waakilishi kutoka kila Wilaya, Tuko sawa?

**Speaker:** Tuko sawa.

**Com. Zein Abubakar:** Kila Wilaya. Tukisema ni kwa nini hawakuchagua wawakilishi kutoka kila Wilaya ni Wakilishi wangapi hao?

**Speaker:** Sabini.

**Com. Zein Abubakar:** Sabini, ziko Wilaya sabini kwa sasa. Tunasema halafu baada ya usabini, ikiwa mji wa Nairobi tutachukua kama Wilaya ni vigumu, tukishachukua mmoja mmoja tutaongeza na wanawake thelathini……………..(Inaudible) tunarudi kwenye ile..

**Audience:** One third.

**Com. Zein Abubakar:** One third na wanawake kuanzia sasa, one third mahali popote tukienda wanatuuliza one third yao kiko wapi. ***(Laughter from the audience).***

Kabla kuwa hajapigiwa tuna hakika kwamba katika bunge hii la juu kutakuwa kuna wanawake thelathini kati ya mia. Kila mkoa iko mikoa mingapi?

**Audience:** Nane.

**Com. Zein Abubakar:** Hapana, ni nane kweli, lakini katika mambo yetu tumesema mkoa, mkoa wa Nairobi, kila mkoa wanawake wanne, watakuja wangapi?

**Audience:** Ishirini na nane.

**Com. Zein Abubakar:** Halafu wawili watoke Nairobi.

**Speaker:** …………………..(Inaudible).

**Com. Zein Abubakar:** Kuongeza sabini, hao ndio wabunge wa bunge la juu.

**Speaker:** Jumba kuu.

**Com. Zein Abubakar:** Jumba kuu, Upper House. Na yule atakayetoka katika Wilaya, sababu kubwa ya yeye ni kuwakilisha nini? …………………..(Inaudible).

**Audience:** ……………………………(Inaudible).

**Com. Zein Abubakar:** ……………………(Inaudible).

**Audience:** …………………(Inaudible).

**Com. Zein Abubakar:** Wananchi gani?

**Audience:** Wa wilaya hiyo.

**Com. Zein Abubakar:** Wa wilaya hiyo. Na ukiangalia katika sura ya kumi, sura ya kumi tumezungumzia fikra ya kwamba, lazima kuweko na kutawanya kwa madaraka hadi chini, devolution. Wanatuambia majimbo e majimbo, lakini hatukupata ……….(Inaudible) ya kueleza kinagaubaga maana ya majimbo ni nini? Sisi tukasema utoaji wa madaraka ya watu kujinyakulia mambo yao chini aunzie chini kijijini, ukitoka kijijini uende katika tarafa. Ukitoka katika tarafa uende katika wilaya na serikali mkuu katika mashina itawekwa wilayani, kwa hivyo Taita Taveta District itajiamulia mambo yake yenyewe hapa, hapa. Kuhusu rasilimali, kuhusu ardhi, kuhusu utoaji wa kodi ni ya hapa. Kordi ya taifa itapozwa na taifa, lakini kodi ya itatozwa na nyinyi, ugawaji wa rasilimali itatozwa na nyinyi, uzimamizi wa ardhi ya Taita Taveta itasimamiwa Serikali ya Taita Taveta. Serikali ya Wilaya na ambao itawakilishwa kutoka kila tarafa.

Mtachagua mtua awe katika serikali ya wilaya na mchague district administrator, kiongozi wa wilaya, nyinyi ndio mtamchagua. Na kiongozi wa Wilaya atakuwa na haki ya kuwateua watu watakaofanya kazi na na yeye, haki ya kuwapa kazi na kuwafuta, lakini wale viongozi wengine mtakuja mtu akichaguliwa huyo amechaguliwa kufanya kazi hii. Wale viongozi kutoka kila tarafa katika wilaya watamweka chini kama inavyofanywa bunge, wamuhoji anafaa, afai?

Sijui mnaelewa?

**Audience:** Tunaelewa.

**Com. Zein Abubakar:** Kwa nini kuzungumzia kuhusu madaraka yanayosomwa na nchi katika wilaya? Kwa nini? Kwa sababu hili bunge la pili, kwa sababu litakuwa na wakilishi mnaochagua katika wilaya, litakuwa na haki ya kulinda imani hiyo, sijui mnanifahamu.

**Audience:** Eeh.

**Com. Zein Abubakar:** Ikiwa hakuna tafsisi inaolinda devolution, inaweza kupotea au haiwezi?

**Audience:** Inaweza.

**Com. Zein Abubakar:** Hiyo ni, hiyo ni…………. (Inaudible) iliyoko. Halafu kutakuwa kuna coordination katika mkoa, halafu ndio tufike kwenye taifa. Halafu kitu kingine ambapo mnafaa kujua ni muhimu sana, tumejaribu pia unapotoa uwajibu na madaraka lazima iwekewe viwango na mipaka, mlisema hivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Zein Abubakar:** Sasa tusema mfano, ukitaka kumwondoa Rais, amevunja sheria, amevunja katiba, mambo hayo tataanzia bunge la chini, tunasema si haki bunge moja kumsufuika mtu, wakubaliane, wamshtaki, wao ndio watoe malalamiko, wao ndio wamfanyie mashaka na wao ndio wanfanyie uamuzi, kama mashtaka inavyotaka kutufanyia sisi. Tunasema si sawa, bunge la chini ikiwa Rais atapita mipaka akavunja katiba na sheria, bunge la chini linaweza kutoa mashtaka, likisha toa mashataka, mashataka hayo lazima ipelekwe bunge la wapi?

**Audience:** La juu.

**Com. Zein Abubakar:** La juu. Ndio isianzie kusema kama kaonewa, sijui mnanifahamu?

**Audience:** Twaelewa.

**Com. Zein Abubakar:** Halafu bunge la juu litasikiza hayo mashtaka na litoe uamuzi. Likipiga kura kwa theluthi mbili kwamba akifanya makosa ataondolewa kama Raisi wetu. Na Rais akiondolewa au akitoka kwenye kiti, au akafa, au naposema kufa si dhambi, au ni dhambi.

**Audience:** Sio dhambi.

**Com. Zein Abubakar:** Maana ya kufa ni nini?

**Audience:** Kawaida.

**Com. Zein Abubakar:** Sio tu kawaida ni kwenda kukutana na muumba wako, kwa hivyo si jambo mbaya sio?

**Audience:** Eeh.

***(Laughter from the audience).***

**Com. Zein Abubakar:** Au kwenda kukutana na muumba wako ni jambo mbaya?

**Audience:** Hapana.

**Com. Zein Abubakar:** Ninaona ni kama watu wengine wanakunakuna. So, ingawa Rais hukaa kwa kiti hiki, nchi yetu haitakwenda tena kwenye uchaguzi kuanza kumchagua Rais, kwa sababu hakuna fedha hizo kila wakati kufanyafanya kura, kwa vile Rais na Makamu walienda pamoja kama wenza, na iwe makamu alijue madaraka aliyopewa Rais na tumesema kiwango cha elimu cha Rais ikiwe sawa na cha Makamu wa Rais, wote wawe na degree. Ukitaka kuwa Rais lazima uwe umesoma Bwana. Akifa, akatoka madarakani, ama akajiuzulu, au akaondolewa na taifa kwamba akakosea. Kulingana na mujibu wa katiba tutampa kiapo ili Bwana, Makamu wake awe Rais, naye achague mtu aendee nawe awe Makamu wake, lakini mtu huyu lazima aidhimishwe na bunge. Sijui tuko sawa sawa?

**Audience:** Ndio.

**Com. Zein Abubakar:** Kitu kingine muhimu sana ambacho najua kina wakera miguu ni kuhusu vyama vya kisiasa. Manake watakaokwenda kukiri mnafikiria lazima wachague ……….(Inaudible) yake sio? Tumesema tume ya uchaguzi itaipa madaraka sio tu ya kusimamia uchaguzi lakini tutaipa madaraka ya kusaidia yao kufuta vyama, mmenielewa?

**Audience:** Ndio.

**Com. Zein Abubakar:** Haki isiwe na Serikali, Serikali mara ingine huamua kujisajili chama au kuvuta chama fulani kwa kupenda kwao kama serikali, sio?

**Audience:** Ndio.

**Com. Zein Abubakar:** Wananchi wametuambia hivyo, kuwa tume huru kama inasimia uchaguzi, isimamie pia na vyama, sikusajili na kufuta vyama peke yake, lakini kusimamia pia vyama. Tumesema vyama lazima viundwe na kuendelezwa kwa mujibu wa taifa.

**Audience:** Taifa.

**Com. Zein Abubakar:** Kwa mfano tumesema, uchaguzi wowote nchini Kenya utafanywa kwa kura ya siri. ***(Clapping from the audience).*** Hapa hatufanyi siasa, nakueleza yaliyomo ndani katika mapendekezo ya kura hii, mapendekezo ya katiba hii inasema, kura zote katiba hii ni itakubalika hata ………..(Inaudible) itafanywa kwa siri, na zitafanywa katika maandishi ya ki-democracia, kwa vile una chama chako usione kwamba unaweza kufanya tu utakalo, na tumeweka mipaka ya vyama. Vyama lazima viundwe kwa utaifa, kabila mmoja haliwezi kuunda chama chake, dini mmoja haiwezi kuunda chama chake huwezi kuanzisha chama katika mipaka ya dini au mipaka ya kikabila, au mipaka ya kitabaka ukasema chama cha Banyenye.

***(Laughter from the audience).***

**Com. Zein Abubakar:** Mnajua kuna tabaka ya juu na chini, ya juu inaitwa nini?

**Audience:** Bwenyenye.

**Com. Zein Abubakar:** Walio……..(Inaudible) sio?

**Audience:** ………………(Inaudible).

**Com. Zein Abubakar:** Na wale wengine ni wa ……………(Inaudible). Kwanza hii tume itakishajili chama na itakuwa kuna usajili wa hatua mbinu, usajili wa hatua ngapi?

**Audience:** Mbini.

**Com. Zein Abubakar:** Hatua ya kwanza ni kwamba wewe unatuma maombi unataka usajili, halafu unapewa miezi kumi na mbili ili utakapokuwa unaenda kwa watu na kuombolea au kuwaelezea mwangaza cha chama chako au chama chenu ili mpate wafuasi, mtapewa hiyo miezi kumi na mbili mpate wafuasi Kenya nzima. Sawa?

**Audience:** Yeah, yeah.

**Com. Zein Abubakar:** Na kitendo cha, theluthi?

**Audience:** ……………………(Inaudible).

**Com. Zein Abubakar:** Wanawake ……….(Inaudible) mnafahamu?

**Audience:** ……………………..(Inaudible).

**Com. Zein Abubakar:** Katika ………..(Inaudible) mwezi mmoja, do you know? Tumesema tume ya uchaguzi, itasimamia uchaguzi pia. Kwa nini ninasema hivyo? Kwa sababu tunataka iwe huru, kura zitakuwa zikihesabiwa mahali zinazopigwa. Si sheria ni katiba inasema hivyo, au sio nyinyi mlisema hivyo?

**Audience:** Ni hiyo.

**Com. Zein Abubakar:** Wanasema mkiki mkiki na mipaka ya kubeba kura mara kura huongezeka au zikapunguka au zikabadilishwa vile mnasema, sawa?

***(Laughter from the audience).***

**Com. Zein Abubakar:** Sawa? Ndio zihesabiwe pale zinapopigwa, tunasema aundikishaji wa kura utaendelea siku zote daima dawamu. Au hamkusema hivyo nyie?

**Audience:** Tulisema.

**Com. Zein Abubakar:** Mkasema pia, kupiga kura ni haki ya Mkenya na nilishangaa vile mlianza mkazungumza kuhusu urai, hakuna mtu aliosema juu ya kitambulisho. Kitambulisho ni haki yako ya kikatiba, passport ni haki yako ya kikatiba. Katiba inasema hivi, wewe una haki ya kutoka katika jamhuri ya Kenya ikiwa wewe n raia, na unaweza kutoka bila paspoti, paspoti imekuja hapo pia na pia imesema hivi, kwa kuofia kwamba ukipewa haki ya kutoko, mtu anaweza kukunyima haki ya kurudi,

una haki ya kurudi katika jamhuri unapopenda. Kwa hivyo mambo ya kusema oh, huyu hakusajiliwa kwa kupiga kura kwa sababu hana kitambusho hakuna tena mambo hayo.

Kila Mkenya ana haki ya kupata kitambulisho, na mtu akikunyima anapelekwa mahakamani kwa kuvunja katiba. Lazima atamani peke yake, pengine tutaporudia hapa nikuambie …………(Inaudible) kupeleka malalamiko, ikiwa unaona mahakama bado havijitengeza vizuri bado tunaendelea kupiga mkasa na mda unachukua mda kuna taasisi mpya tunavyozitengeneza. Ikiwemo mahakama kuu ambayo itakuwa na majaji wapya, hakuna hata mmoja aliye kosa sasa kuingia mahakama kuu…. ***(Clapping from the audience).***

**Com. Zein Abubakar:** Hii ni tume huru ya kurekebisha katiba hatutaki ifanye siasa, kwa hivyo tumesema, vile uko siasa kubwa mno itapunguzwa. Lakini atakayechaguliwa kama mwanatume atalindwa kikatiba ili asiingiliwe katika kazi zao. Na mtu yeyote ni muhimu mbinu kukueleza hivi, mtu yeyote atakayepewa madaraka makubwa hatayachukua madaraka hayo mpaka atakapokwenda kukaa bungeni na wabunge wamuulize maswali, anafaa au hafai?

There will be a confirmation process and making of any person who is given National responsibility, akiwa ni tume kama hii yetu, ingekuwa ni tume umeanzishwa katika katiba mpya nisingesimama katika mbele yenu mpaka nikaenda kuhojiwa bungeni, ninafaa au sifai? ***(Laughter from the audience).*** Pengine hayo yangefanyika tungekuwa na wafanishi wachache. Kwa sababu katika kusimamia uchaguzi utuhitajika ama ni lazima uwe huru, watu wote lazima wapewe fursa sawa, hasa katika kutumia chombo cha taifa kama KBC ni katiba si kisheria, sio Katiba. Halafu kuna mambo mengine tumeweka ile kulinda watu kuleta fujo, au kuleta uhasa ama katika jamii. La pili lililo la murwa zaidi ambalo ni kuongea nyinyi.

Ukiwa mtu anataka kusimama bila kusimama na chama aruhusiwe, au hamkusema hivyo?

**Audience:** Tulisema.

**Com. Zein Abubakar:** Ikiwa mtu hataki kusimama mbunge kama mwanachama wa chama, asimame mtu binafsi aruhusiwe. Ikiwa anataka kusimama kama Rais, aruhusiwe lakini nitawawekea mipaka. Lazima wawekewe mipaka kwa sababu gani? Kwa sababu kila mtu atataka tu pengine kuna wakorofi ambao wanajua wazi hata watu wa kijijini chake hawawezi kumchagua Rais lakini anasema mimi nataka kujiteua kusimama kuwa Rais, ili aonekane kwenye picha za magazeti na hata kwa utangazaji, kwa hivyo tutaweka kiwango uwe na wafuasi kusaidia hekima hiki, kupitia njia ya heshima, ili wale wenye wenye wasisimame, wawe watu wa kushangilia. Mnajua kuna tofauti wa mshangiliaji na mtu aliye…….(Inaudible) sio? ***(Laughter from the audience).*** Sasa mniite kwenye jambo ambalo mnajua mnangojea kulishinda.

**Speaker:** Hapo hapo.

**Com. Zein Abubakar:** Na hapo hapo, nataka… ni saa ngapi sasa?

**Audience:** Saa saba kasorobo.

**Com. Zein Abubakar:** Saa saba kasorobo mtaniwia radhi nachukua mda mrefu, …………………….(Inaudible). Sasa niko kwenye mambo ya ardhi najua mnataka kujua hayo mambo ya ardhi.

**Audience:** Sana sana.

**Com. Zein Abubakar:** Hebu fungua sura ya kumi na moja, mmefika?

**Audience:** Bado.

**Com. Zein Abubakar:** Wewe unaona mambo ya ardhi yanafuata tu baada ya revolution sio?

**Audience:** Ndio.

**Com. Zein Abubakar:** Kwa sababu yanaenda pamoja, tumefika hapo. Sasa niwaambie kwa ujumla tu kwa kugusia kwamba kuhusu ardhi, watu wengi walitoa lawama zao, hata watu wa hapa walitupa lawama zao kuhusu ardhi. Wakasema vipi mtu anaweza kuambiwa ni mpangaji katika ardhi ya mababu na manyanya zake, au hamkusema hivyo?

**Audience:** Tulisema hivyo.

**Com. Zein Abubakar:** Wakapewa vipi watu wengine, anakimbia Nairobi anakuja na cheti chake hapa anasema nyinyi mliyokaa hapa miaka mia moja hameni, hamjulikani nyinyi, mnaitwa squatters, au hamkusema hivyo?

**Audience:** Tulisema.

**Com. Zein Abubakar:** Mnasema nyinyi vipi mtu atapewa mamlaka katika wilaya kugawanya ploti na anapoigawanya majina fulani fulani yameanza na majina fulani fulani peke yake ndiyo yanapata ploti na wenyeji hawana. Au hamkusema hivyo?

**Audience:** Tulisema.

**Com. Zein Abubakar:** Mkatuambia vipi mtu atakuwa na mahekari ya maelufu na wengine hawana hata ka heka kamoja, hamkusema hivyo?

**Audience:** Tulisema hivyo.

**Com. Zein Abubakar:** Na ndipo, mlisema vipi mtu ambaye sio Mkenya, ni mtu wa inje anakuwa na haki ya kuwa na ardhi na Mkenya mwenye haki hana ardhi, au hamkusema hivyo?

**Audience:** Tulisema.

**Com. Zein Abubakar:** Mlisema hivi pia, vipi mtu atapewa mashamba makubwa ambayo halitumii linamea kwetu na ……..(Inaudible) ya mimba na wengine wanaotafuta heka moja ya kujilimia mahindi hana, au hamukusema hivyo?

**Audience:** Tulisema.

**Com. Zein Abubakar:** ……..(Inaudible) mbona ndio mnasema mlisema hamkusema, kama mwanzo mwanzo. Mwanzo tunasema ikiwa wewe sio Mkenya huna haki ya kumiliki ardhi. ***(Clapping from the audience).*** Ikiwa wewe si Mkenya una haki tu ya kukodi ardhi, tena kwa vile sisi tusiwe tukaonekana na mapendeleo mengine tunafanya kuwaonea wengine, manake watu wanaamini sisi wa Afrika kazi yetu ni kuwaonea wengine tumesema ikiwa hivi leo wewe ni mgeni na una free ku-own title, Katiba mpya ikiingia ukapewa lease ya miaka tisini na tisa. Hizi lease ya tisini ya tisa ikiwa hii ilikuwa ardhi ya umma inarudi kwa umma, ikiwa ardhi hii ilikuwa ya serikali inarudi kwa serikali……….(Inaudible).

**Audience:** Serikali haina ardhi.

**Com. Zein Abubakar:** Sasa Mzee akamwambia serikali haina ardhi, wacha kifafanulie kitanzi. Katika Katiba mpya lazima tuyaandalie yaliyo ya zamani kwamba hivyo inaitwa Government land kwa sasa itakuwa inaushishwa kweli katika katiba. Tumegawanya katiba mpya sehemu tatu ya umilikaji wa ardhi. Sehemu ya kwanza tunasema ni public land, na public land will be heading first from the people of Kenya by the Government, ndio hapo sasa inaitwa serikali ya, hati serikali itajiunga itakuwa nini?

Ardhi ya umma, kama kuna kitembo cha pili, kitembo cha pili kinasema nini? Ardhi ya umma wenyeji ni some kwa tafsiri yangu kombokombo, inasema public land, halafu inasema common maana common ni nini inayomilikiwa na jamii kwani hakuna haki ya mababu zenu nyinyi wa Taita na wa Taveta ambao ni yenu, haiko?

**Audience:** Iko..

**Com. Zein Abubakar:** Hizo zitageuka zinaitwa common, si mtu mmoja anayeimiliki inadhirikiwa na jamii, sijui mnanielewa?

**Audience:** Tunakuelewa.

**Com. Zein Abubakar:** Sehemu ya tatu, ni ardhi inayoamilikiwa na mtu binafsi. Sijui tuko pamoja sasa, eh? Tunasema hii ya mtu binafsi itatumika bila kuwanyima watu umma au umma wenyeji haki zao.

Halafu mnasema ardhi yeyote ambayo haitatumika ipasavyo inavyosema sheria kwa mfano ardhi ambayo inaweza kulimiwa mahindi ikawachua imee magugu itakuwa hakuzwa kodi. Sijui mnanielewa?

**Audience:** Ndio.

**Com. Zein Abubakar:** Itakuzwa nini?

**Audience:** Kodi.

**Com. Zein Abubakar:** Mashamba makubwa makumbwa ambayo hayatumiki vizuri yatatozwa kodi ili wenyewe awe na uchungu aidha aanze kuajiri watu wafanye kazi, au akate aseme hii siwezi kuitumia. Kwa mkono wa watu. Halafu tumeweka msingi ya kwamba kila Mkenya ana haki ya kumiliki ardhi, ni misingi hiyo.

Halafu kulingana, nikisema hayo mengine mtakasirika jamani, msichukulie mimi nasema hayo kwa sababu mimi ni mtu wa Pwani, mnakumbuka wala sitaki kutukana mtu. Tumetenga kitengo, nataka uangalie kitengo mia mbili thelathini na tano. Mko hapo?

**Audience:** Yeah.

**Com. Zein Abubakar:** Mia mbili?

**Audience:** Thelathini na tano.

**Com. Zein Abubakar:** Thelathini na tano. Uende roman namba tisa, (ix) mko hapo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Zein Abubakar:** Mwende B1. B1 mmuipata B1?

**Audience:** Ndio.

**Com. Zein Abubakar:** Haya wacha nikusomee tusome pamoja. The review hii ina maana tunaanzia pale juu, inasema establish mechanisms for the review and assessment of all claims to unjust expropriation of land, invest, hebu msome na mimi nisikie.

**Audience:** In the Coast, North Eastern and Rift Valley.

**Com. Zein Abubakar:** In the Coast, North Eastern and Rift Valley provinces or elsewhere, whether arising from historical or other processess in order to establish their validity and how best they can be jostling, peacefully and equitably resolved…………..(Inaudible). Mko hapo?

**Audience:** Yes.

**Com. Zein Abubakar:** Inasema tunatambua katika mikoa mingapi ya nchi hii na pengine sehemu zingine, kulitokea mambo yanayohusu historia au mambo mengine ya kijanjajanja, kuwanyota, kuwapokonya, kuwadhulumu watu ardhi zao. Lazima katiba inasema, lazima kutengenezwe njia itakayochunguza mambo hayo, na ikishayachunguza iyafanyie mambo ili ardhi itendeke kwa amani na usawa, au sio sawa hivyo?

**Audience:** Ni sawa.

**Com. Zein Abubakar:** Au nyinyi hamna malalamiko ya kihistoria. Mara ya mwisho nilipokuja hapa, nilikuja nikazumza na nyinyi niliwaambia ………….(Inaudible) wenzetu sio, au sikusema hivyo?

**Audience:** Ulisema.

**Com. Zein Abubakar:** Na mimi nilifurahi sana na leo nina furaha kubwa na bado ninajigamba huko Nairobi kwamba nyinyi mlikuwa mnasema hamtatoa maoni je watu walitoa maoni ama hawakutoa maoni?

**Audience:** Walitoa.

**Com. Zein Abubakar:** Na msisema hivyo kwamba naenda kinyuma na kiapo changu nilichokula, kwa sababu yenyewe sio……………..(Inaudible) nilipoondoka mjini ………..(Inaudible) ondoka mjini?

**Audience:** ……………………(Inaudible).

**Com. Zein Abubakar:** Mkisengenya sicheki nie, nimewaambia ……….(Inaudible) aliposema, …………….(Inaudible) alisema nini, ukinisengenya nie sicheki, ukifinya sioni uchungu na ukinikata nie sitoki damu.

**Audience:** ………………….(Inaudible).

**Com. Zein Abubakar:** Basi niwacheni nikomee hapo, nimewaeleza mengine kwa kijuu juu na kufunga kitabu na kufunga kazi ili nipokee maswali. Kwanza ninasema hivi, tatizo mmoja kubwa, kumbwa sana tuliyolichambua kutokana na maoni ya watu, ni kwamba kwa katiba hii tuliyonao sasa ilikuwa haina njia, mnanisikiza, ilikuwa haina nini?

**Audience:** Njia.

**Com. Zein Abubakar:** Haina njia wala haina tahasisi, wala haina maadhili ya kuindeleza katiba, kuitekeleza katiba na kuhalalisha katiba wazi. Na ni mambo na ningependa kusema hivi kuhusu Mwalimu wangu Mzee Mwawanzi. Mwalimu wangu Mzee Mawanzi alinifundisha ……….(Inaudible). Ukiona jambo lolote zuri kutokana kwangu limetokana na yeye, na mkiona jambo lolote linalotokana kwangu limetokana na mimi halijatokana na yeye. ***(Laughter from the audience).***

Mwalimu wangu Mzee Mawanzi alikuwa akininongonezea hapa tulopokuwa tumekaa akiniambia kwa mujibu wa historia na nakubaliana na yeye, kwa mujibu wa historia katiba ya mwanzo iwe ya majimbo, ilisaidiwa kwa sababu ilikuwa hakuna njia ya kuiendeza na kuizimamisha hii katiba, na wale watakaojaribu kuiondoa iwapige vita. Kwanza hilo ndilo lilikuwa tatizo kubwa na mimi nakubaliana na yeye na mimi nakubali yakuwa inakutaja kwamba hayo ndio yalikuwa matatizo makuu. Na si vizuri kujiandikia mapendekezo mazuri mazuri tu bila kuwako na njia na tahasisi ya kuyatekeleza au ni si sawa hivyo, si sawa? ..

**Audience:** Sawa.

**Com. Zein Abubakar:** Kwa hivyo tumeona tahasisi na vyombo ambavyo vitatekeleza katiba hii. Kwa mfano, watu wengine walituambia kwamba ukiwa na Mkuu wa sheria, yuko bungeni, yuko kwenye baraza la Mawaziri na yeye ni mtu mwanasiasa ama mwanasiasa si mwanasiasa, halafu tena huyo huyo unampa na mamlaka ya kuamua atamshtaki nani, na asimeshtaki. Tumekuwa na matatizo nchini kwamba wanaofanya makosa, wanaojua watu wenye nguvu zao hawashika chini, wasiofanya makosa saa ingine lakini wanamruhusu mtu fulani mwenye nguvu zake wanashtakiwa, au sio kweli.

**Audience:** Kweli.

**Com. Zein Abubakar:** Kwa hivyo, wamesema mtawekee mtu atakayesimamia mashtaka awe kando na serikali, na awe na amesimamiwa na katiba in a constitutional office. ***(Clapping from the audience).*** Mtu anayemshataki mkubwa wa serikali,

mtu anayesimamia masharti atakuwa na haki za kikatiba kufanya kazi yake bila kuingiliwa na mtu, bila fikisho, bila uoga, bila upendeleo.

Naomba mniwie radhi, awe na haki ya kushtaki mtu anapoona yeye ni sawa. Lakini pia tumesema ikiwa utaweka mtu kushtaki watu, lazima uweke na mtu wa kuwalinda sio? Kwa hivyo tumetengeneza a public defender (ombudsman) Mwenye haki sawa zaidi yakushtaki. Sijui utashtakiwa kwa …….(Inaudible) kubwa kubwa ya kutisha tisha, serikali ina haki ya kufunga mtu wakutolinda haki hiyo na kukuwakilisha bungeni na kumtolea ………….(Inaudible) mahakamani, sawa?

**Audience:** Sawa.

**Com. Zein Abubakar:** Ili kulinda katiba hii, tumesema lazima tuakikishe kuwekwa mahakama huru, tumerudi kwenya mahakama, si niliwaambia nitarudi?

**Audience:** Ndio.

**Com. Zein Abubakar:** …………….(Inaudible) Mahakama huru, hivi hivi nanavyosema na wewe tunafuata elfu moja ngapi? Elfu moja mia nane na arubaini ya maneno ya Wakenya tuliyokusanya, katika haya miaka elfu moja mia nane arubaini hakuna jambo nzuri aliyopatwa nayo hata mmoja.

Maoni yote haya tumeyakusanya, one thousand eight hundred and forty pages, yanalalamika kuhusu kuzoea kwa muozo.

**Audience:** …………….(Inaudible).

**Com. Zein Abubakar:** …………..(Inaudible) nini kingine? Ufisadi, uzembe wa kwenda kazi katika mahakama, wanasema haki siku hizi inanunuliwa, au hamkusema hivyo?

**Audience:** Tulisema.

**Com. Zein Abubakar:** Ukiwa na senti zako wewe unakwenda kununua haki mahakamani, sio sisi tuliyosema hivyo jamani, waliosema hivyo ni Wakenya ambao watatumia mahakama leo na kesho, kila siku. Kwanza wanakwenda na wao ndio wanadhuluma. Na kusema kwamba Wakenya hawana imani na mahakama, nimesema mimi?

**Audience:** …………………(Inaudible).

**Com. Zein Abubakar:** Wamesema Wakenya. Wanasema lazima tutafute njia zingine ambazo zitafanya nini? Zitafanya

kwanza kabisa, mahakama yawe huru, yasiingiliwe na mtu. Wewe ukiwa ni mtu ambao umepewa cheo cha kuitwa jaji, usiende kumuuliza mtu mwingine jamani kesi hii ni ikate namna gani? Mahakama yote iwe huru, halafu Wakenya mmetuambia kuwekewa kesi miaka kumi na mbili maanake nini?

**Audience:** ………………..(Inaudible).

**Com. Zein Abubakar:** Nenda urudi, nenda urudi, nenda urudi, ikiwa nenda urudi hiyo inaendelea haki iko?

**Audience:** Hakuna.

**Com. Zein Abubakar:** Wametuambia tunataka mahakama ambazo hazitachukua mda mrefu kumkatia Jambo fulani. Wametuambia pia unaweza kwenda mahakamani ukapata hakimu ambaye hakutimia ki elimu. Mimi ndio nimesema hivyo?

**Audience:** Aah.

**Com. Zein Abubakar:** Wakenya wamesema hivyo, mmetuambia hawana elimu ya kutosha, kwa hivyo nasema uwawekee viwango vya elimu ya kutosha, mtu anayetaka mahakama kumkatia mtu shauri amfunge mtu huyu, ampokonye uhuru wake ambao amepewa na haki ya Katiba. Mtu kama huyo anafaa kukua mjanja wa elimu

**Audience:** Hapana.

**Com. Zein Abubakar:** Kama nitanyimwa haki mimi nisinyimwe haki kwa sababu ya uchache wa elimu, au sio sawa hivyo?

**Audience:** Sawa.

**Com. Zein Abubakar:** Kwa hivyo ikiwa tunataka sisi mahakama zetu siziwe za siasa za kikorofi, mtu akienda anapigiwa kelele au wanasema mambo kwa lugha ambayo ufahamu. Ni haki mtu kusema kuwa funguliwa mashtaka kwa lugha anayoyafahamu.

Ni haki ikiwa lugha usiyoifahamu unatumika kwa serikali, bora kumtafuta mkaremani anayefaa.

**Audience:** Ndio.

**Com. Zein Abubakar:** Na ni haki kwa Mkenya ikiwa unafungwa na mashtaka makubwa leteni mawakili wa serikali.

**Audience:** Ndio.

**Com. Zein Abubakar:** Hayo ni kwenye mahakama, tunasema nini tena katika mahakama tunasema iwe ikweko mahakama hivyo sasa, ukaweka mahakama kuu kabisa. Supreme Court, na Supreme Court hii itakuwa na original jurisdiction kwa kusikiza mambo ya kikatiba. Unaweza kutoka wewe leo hapa ukaenda kama Supreme Court ikiwa unaamini kwamba haki yangu za kikatiba zimefurugwa bila kupita vikoti vingine vingine vidogo vidogo. Muwe na haki hiyo, ikiwa huna imani na korti zingine uwe na njia moja kwa moja mpaka Supreme Court. Lakini ikiwa unataka kwenda High Court, isiwe huwa na haki hiyo ambapo utatuliwa jambao lako vibaya sana uwe na haki ya kukata rufani katika mahakama mkuu kabisa.

Lakini Wakenya walituambia, wale waliopendekeza tuweke mahakama kuu kabisa, je, ukimtoa hakimu au jaji ambaye Wakenya hawana imani na yeye sasa lipo sasa nipe madaraka zaidi, utakuwa umefanya nini?

**Audience:** …………….(Inaudible).

**Com. Zein Abubakar:** Watu wengi wanasema kazi bure, kazi bure eh, haitafua dafu kazi hiyo, wanasema tupeeni majaji wapya katika mahakama hii hayo hizi zingine mziwache lakini katika mahakama hii mpya tupeni majaji wapya ambai aidha hawajakumbwa na ufisadi au hakujatokea fununu kwamba ni mafisadi au watu hawana imani na yeye. Imetendeka hiyo katika mapendekezo yenu, ikiwa watu wametuambia hivi na sisi tukachukua hatua. Itakapokuja katiba mpya majaji wa sasa wasionewe kwa sababu ya mnongono wa watu hii, wape fursa ya ku-retire kimya kingi bila kuulizwa maswali, na sisi tumekubali hii Kenya mpya kwamba ikiwa wewe ni jaji sasa na pengine una wasi wasi wa maswali yatakayokuja baadaye Katiba mpya itakapoanza kutendeka hata kama umetimiza miaka ya ku-retire una haki ya kusema Bwana mimi naomba ku-retire, utasema haki hayo uende ukapumzike nyumbani, na wale waliojiamini pengine hakuna mnongono mpya hizo wa kutosha vijao wakitaka kuendelea tumekubaliana hivyo waendele katiba vibaka hii, lazima watimize masharti ya nidhamu ya uongozi.

Masharti haya ya nidhamu ya uongozi, tunawafanyia kila mtu anayeitisha kiongozi. Kwa mfano, ni masharti gani yaliyomo ndani ya masharti ya uongozi, kwanza kabisa utataka utueleze wewe mali ulizo nazo, au sio sawa hivyo?

**Audience:** Sawa.

**Com. Zein Abubakar:** Kwa vile tunajua changu ni changu na cha mke wangu ni changu na changu ni cha mke wangu, tafuta mali ya mkewe utatakiwa utaje, au si sawa?

**Audience:** Sawa.

**Com. Zein Abubakar:** Na kama ni jaji mwanamke, ya mumewe umtaje. Halafu sharti mengine hakuna tena kufanya hilo sharti, au sio sawa hivyo?

**Audience:** Sawa.

**Com. Zein Abubakar:** Ikiwa wewe unataka kufanyia kazi umma, umma utakulipa vizuri lakini sahau mambo ya kufanya biashara, kama ni jaji, kama ni kiongozi usahau, ukiwa mtumizi wa umma biashara sahau, mishaahara utalipwa tosha wewe, hivyo basi ………………(Inaudible) lakini hawataruhusiwa kufanya biashara, maanake majaji wakifanya biashara, haki pia itakuwa ni dhambi au si hivyo?

**Audience:** Ni hivyo.

***(A lot of noise from the audience).***

**Com. Zein Abubakar:** Tunasema hivi, katika mtenda kazi wangu wewe kama jaji utafanya kazi bila upendeleo au sio?.

**Audience:** Ni kweli.

**Com. Zein Abubakar:** Bila maumivu, bila chuki au bila kuchukua amri kutoka kwa mtu mwingine ……………(Inaudible) kama wewe. Halafu tunasema hivi unajua ukifanya mwaka mmoja tu, atafanya miaka moja halafu anze kulipiza mali kila baada ya mda mtaangalia mali zangu zimefika wapi. Na ikiwa haziambatani na mishahara yako utasema umetoa wapi? Halafu tumesema hivi, jaji yeyote ambaye kuna malalamiko dhidi yake kupitia chama cha wanasheria wa Kenya au kupitia mahakama. Atafunguliwa mashataka, itawekwa independent tribunal na hii kufanya tribunal na hii iwe independent tutatumia majaji kutoka ndugu zetu wa Tanzania au Uganda au sio sawa hivyo?

**Audience:** Ni sawa.

**Com. Zein Abubakar:** Wakasema ukweli …………………………(Inaudible) lakini, hatutamfunga idhini tutaleta majaji kutoka Tanzania wataweka tribunal wamchunguze yule, wamchunge, wamwangalia ameingia mipakani au ametoka, akiwa ametoka yeye afungwe ndani. Na akiwa amevunja sheria amevunja sheria ya kikatiba. Sasa wale tunasema, ikiwa wewe Bwana hutaki kuingizwa katika maisha haya kuchunguzwa chunguzwa basi ni heri uchukue haki yako uende ukapumzike.

***(Clapping from the audience).***

**Com. Zein Abubakar:** Au sio sawa hivyo.

**Audience:** Ni sawa.

**Com. Zein Abubakar:** Huyu Bwana amevaa kofia nzuri ananiambia aah ndio maana mtapelekwa kortini, anasema yeye si mimi. Kwa sababu tunasema sisi …………….(Inaudible) msitushike, tumesema hivi, sisi tunatekeleza kazi yetu kwa mujibu ya sheria, sio?

**Audience:** Eeh.

**Com. Zein Abubakar:** Nikitoka Nyanza kuja hapa Taita/Taveta ………….(Inaudible) mnaniona mimi kama mtu muoga muoga hivi?

**Audience:** La hapana.

**Com. Zein Abubakar:** ……………………..(Inaudible) hulisifu mwanawe, maanake nikianza kuwahurumia tena shauri yetu ……….(Inaudible) sikunyetei. Tunasema hivi tunatekeleza kazi zetu kulingana na mujibu wa sheria lililowekwa na bunge, na kitengo ishirini na tano yakielelezwe bunge inasema, katika utekelezaji wetu wa kazi hakuna mtu anayeweza kutufungulia mashtaka, isipokuwa ikiwa tumevunja sheria, hakuna mtu aliyevunja sheria. Tunayachunguza mambo ya watu wasiofaa kusikiza fikra ya maoni ya Wakenya ni kuunda sheria huko?

**Audience:** Hapana.

**Com. Zein Abubakar:** Kutimiza wajibu wa sheria na kusema sisi tuandike na kuchunguza upya kazi zote………………………..(Inaudible) kumbukumbu ni ………….(Inaudible)?

**Audience:** Hapana.

**Com. Zein Abubakar:** Ikiwa wana imani kwamba sisi tunavunja sheria wanahaki ya kutufungulia mashtaka, sisi tumesema na hatusemi hayo kwa ukarimu naomba mnisikize vizuri ndugu zangu, hatusemi haya kwa ukarimu, wala hatusemi haya kwa utovu wa nidhamu na kukosa haya, tunasema haya kwa nyinyi kwamba tunaofanya la haki na tunaitii sheria. Na wa Kenya ndio waliotutuma wafanya watakalo, sisi tutaendelea na sheria tunawezayo, na tumesema hivi, ikiwa hayo mambo ni si yetu, hayo ni maoni ya watu, katika hayo niliyosema kuhusu mahakama naomba mtu anayefikiria ni mabaye ainue mkono. Yupo?

**Audience:** Hakuna.

**Com. Zein Abubakar:** Na kama yupo ningepiga kelele nikufikie. ……….(Inaudible) ikiwa unaona haya tunayosema hayakutoka kwa mtu, aliyesema mambo waliosema …………….(Inaudible) kama sio hapa mliotoka kwenye magazeti ainue

mkono, yuko?

**Audience:** Hayupo.

**Com. Zein Abubakar:** Wapi apige kelele. Pengine sisikii kelele pia inje hakuna. Sisi tunaposema jamani na mniwie radhi hii kusema haya. Nasema kwa kupenda kwangu, nina sema kwa sababu yananichoma moyoni, sisi mtu anasema hamna haki hata kufikiri, sitimizi, kwa nini sitimizi? Hata mnyama anafikiri, mimi sifikiri pengine …………….(Inaudible) isiyojulikana pengine ………………..(Inaudible) kama kiumbe cha ……………………………(Inaudible). Lakini sisi mtu atasema wa Kenya wasikifiri hayo ni ya kutengeneza au ndio kuaribu?

**Audience:** Kuharibu.

**Com. Zein Abubakar:** Hayo ni ya maana au matusi?

**Audience:** Matusi.

**Com. Zein Abubakar:** Sisi sikujua tunaumbwa na Mwenyezi Mungu na kipowa cha kufikiri tusifikiri, na tukifikiri atatufanya nini?

**Audience:** ……………………(Inaudible),

**Com. Zein Abubakar:** Nauliza mimi?

**Audience:** Atafanya nini?

**Com. Zein Abubakar:** Atatufanya nini sisi, na ana uwezo gani wa kujua sisi tumefikiria, anaende kuingia katika kinywa lakini huku amejua watu wamefikiri, hayo ndio mambo ambayo tunataka kuyawacha, tunafaa kurudi nyuma au kwenda mbele?

**Audience:** Kwenda mbele.

**Com. Zein Abubakar:** Vipi mtu atasema ukivaa hii ribbon ya yellow kama hii unanishtua, kwa nini usikitumie kama unafaa kushtuliwa?

***(Clapping from the audience).***

**Com. Zein Abubakar:** Ikiwa wewe unafikira hizo, inamaana umesha…….(Inaudible) au sio?

**Audience:** Ndio.

**Com. Zein Abubakar:** Haji kijitambaa ...(Inaudible), hebu tuelewane……………(Inaudible) nidhamu, kama kuna watu………..(Inaudible)

Sasa kuhusu haki za binadamu ananikumbusha nizungumzia kuhusu Kadhi court, waislamu walisema tunataka Kadhis Court ziendelee au hawakusema hivyo waislamu?

**Audience:** Walisema.

**Com. Zein Abubakar:** Wakasema haina maana kuwa na Kadhis court, halafu mtu akitaka kukata rufani aende kwa korti ambayo sio ya Kadhi au hawakusema hivyo? Wanataka Kadhis court iwe na njia zake zaku-appeal za kukata rufani au hamkusema hivyo?

**Audience:** Tulisema.

**Com. Zein Abubakar:** Lakini Kadhi court inahusiana tu na sheria ya waislamu kuhusu haki zao za kibinadamu za kidini yaani huwa katika familia, kuoa, ndoa kuwachana au kufa katika ………(Inaudible) katika ………..(Inaudible) hivyo tu……………(Inaudible) umeona watu waongezee pia ikiwa atafanyana ……….(Inaudible) ambapo ikiwa pesa sio nyingi kazi pia hasa ikuwe hivyo au waislamu hawakusema hivyo?

**Audience:** Walisema.

**Com. Zein Abubakar:** Wakasema kuna mali zile za umma za watu, kukiwa kuna ubishi kuhusu kutumia mali ya watu kazi ………..(Inaudible) au hamkusema hivyo?

**Audience:** Tulisema.

**Com. Zein Abubakar:** Wakasema makazi wawe wa kutosha. Wakasema pai katika ofisi ya Kadhi uwe kuna mwanamke anaijua sheria ya kiislamu ili wasaidie wanawake ikiwa wana mambo yao ya kusema hawawezi kusema mbele ya Kadhi, au hamkusema hivyo?

**Audience:** Ni kweli.

**Com. Zein Abubakar:** Hayo yote yametekelezwa. Ukisoma Kadhis' court utaona hayo yote yametekelezwa. Je nitakimbia, nirudi katika haki za kibinadamu na kabla kufika hapo nimesema tumetengeneza tume ya haki za kibinadamu na kuendeleza mashtaka watu kikatiba, tumetengeneza tume au mlinzi wa taifa, the ombudsman, mnataka hivyo sio?

**Audience:** Eeh.

**Com. Zein Abubakar:** Ikiwa kuna mtu anaona lengo lake anaona hataki kuyapeleka kortini yatafanyiwa mambo mambo atakayeweka kwenye mlamishi huyu wa taifa. Katika hapo hapo pia kuna kitendo ambapo kinashughulikia mashlaha ya wanawake na kuhusu jinsi wanawake wanaweza kuingizwa katika mambo ya kitaifa ka kuzikishwa.

Pia, kuna tume itakayosimamia devolution, ikiwa utatengeneza devolution na hakuna tahasisi ya kufuatilia devolution ifanye kazi itawapa ………(Inaudible) hivyo hivyo, kuna tume hiyo. Kuna tume nyingi na ofisi nyingi ambazo tumezitengeneza ili kulinda haki za wa Kenya. Lakini tuangalie tu kwa haraka kumi na tano kama tunaweza kurudi nyuma kwa kumalizia.

Ningependa kusema kwamba, na sisemi haya kwa majivuno, mapendekezo haya ka katiba yanahaki za kibinadamu zilitiliwa mkazo kushinda nchi nyingi sana. Sasa utaona kwamba tunaanza kitengo, ningependa tuanze na kitengo namba thelathini na mbili, right to life, mmeona hiyo? Haki ya uhai mmeona?

**Audience:** Ndio.

**Com. Zein Abubakar:** Inasema everyone has the right to life, angalia kitengo kinachofuatia, the death penalty is abolished, sawa?

**Audience:** Eeh.

**Com. Zein Abubakar:** Angalia hiyo yenye inafuata inasema nini? Usawa, mmeona usawa eh?

**Audience:** Ndio.

**Com. Zein Abubakar:** Halafu freedom from discrimination mmeona hiyo?

**Audience:** Eeh.

**Com. Zein Abubakar:** Halafu angalia katika kitengo thelathini na tano tumetengea nani hiyo?

**Audience:** Wanawake.

**Com. Zein Abubakar:** Nani huyo?

**Audience:** Wanawake.

**Com. Zein Abubakar:** Wanawake, katiba ya sasa katika kitengo cha wanawake peke yao eh, wanawake walituoambia hawana haki ya kurithi, wamepewa haki hiyo, hawana haki ya kukua na mali katika ndoa, angalieni vizuri katika kitengo hicho. Halafu kuna the older members of society mmeona hiyo?

**Audience:** Yes.

**Com. Zein Abubakar:** Haki za wazee, baada ya wezee tunakuja kwa nani?

**Audience:** Kwa watoto.

**Com. Zein Abubakar:** Kwa watoto,……….? (Inaudible) baada ya hapo tumepata nini?

**Audience:** Familia.

**Com. Zein Abubakar:** Familia, haki za familia…………? (Inaudible). Halafu inatokea nini?

**Audience:** Walemavu.

**Com. Zein Abubakar:** Walemavu. Halafu hizo zingine ni haki ambazo tutapea watu wa kuwaida, ningependa kukuonyeshea kwamba haki hizo upewa watu kawaida lakini angalia kitengo 45, privacy, every person has a right to privacy which includes the right not to have:-

a) Where person………………(Inaudible) mmeelewa hiyo wa Kenya walituambia polisi wanaanza kukuvuruga watakavyo wakiingiza mkono mifukoni wakikupata wewe, waingie wapige teke mlango wako ……………..(Inaudible) wako wengi, halafu inasema nini? There property rights there are professional rights, information relating to the family or private affairs unnecessarily are acquired or revealed of the privacy of the communication is invaded. Unaongea katika simu na kuna mtu anakusikiliza sio haki tena hivyo, hakuna hiyo sasa.
b) Freedom of religion, belief and opinion.
c) Freedom of expression. Na kuna waandishi wa habari hapa?

**Audience:** Wako.

**Com. Zein Abubakar:** Hebu angalia kitengo la 45, kitengo ambalo inasema every person has a right to freedom of expression which include the, freedom of the press and other media.

B, freedom to receive or publish information or ideas, C, freedom of artistic creativity, kuna wasanii hapa?

**Audience:** Ndio.

**Com. Zein Abubakar:** Mnaona hiyo? Academic freedom and freedom of statistic research okay, lakini waandishi wa habari angalieni hii 46, publication of opinion, freedom and independence of the electronic media ……….(Inaudible) and guarantee, mnaona hiyo? Lakini muangalie zaidi kuhusu mambo ya freedom to infromation kuwalinda nyinyi, angalia kitengo namba arubaini na sita 2B, mmeona imesema nini?

**Audience:** ………(Inaudible).

**Com. Zein Abubakar:** The state shall not hurt or penalise any such person for any editoral opinion or view or the content of any such publication au sio sawa hivyo?

**Audience:** Sawa.

**Com. Zein Abubakar:** Haki ya kuandamana ikiwa mmekasirrishwa na jambo imeangaliwa, angalia kitengo namba arubaini na tisa inasema, every person has the right to a peaceful demonstration without the requirement of prior permission to assemble, to demonstrate to ………..(Inaudible) and to present decision to public authority au sio sawa hivyo?

**Audience:** Sawa.

**Com. Zein Abubakar:** Siku hizi ukitaka kuandamana mpaka ukachukue katiba hii sio?

**Audience:** Eeh.

**Com. Zein Abubakar:** Nitaapa kusema machache, unaambiwa ukuwe calm wala usiwe unavunja imani. Ikiwa wewe unataka kuandamana mji mzima kuonyesha kwamba umekasirishwa na watu wanaovyogawanya ploti hapa, una haki hiyo. Lakini tunaomba haki hasa watu wa kidini angalieni haki ya kila mtu.

Angalia hamsini na moja every person has a freedom of movement lakini pia every person has a right to leave the republic angalia inayofuatia juu, every citizen is allowed to enter into, remain in and reside anywhere in the republic, sawa?

**Audience:** Sawa.

**Com. Zein Abubakar:** Fungalia kitendo namba sitini na tano kuhusu haki za wafanyikazi na vijana wa kazi. Mtu ana haki ya kulipwa mshahara wake mmeona hiyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Zein Abubakar:** Angalia health, security, education, housing, food, water, sanitation and Government, consumer rights lakini hii ya kufurahisha zaidi kuna polisi wowote hapa? Na kuna raia yeyote hapa? Nyinyi nyote raia?

**Audience:** Ndio.

**Com. Zein Abubakar:** Angalia sitini na sita, 66 inasema nini? Every person has a right not to obey unlawful instructions, hizi tunazopewa sisi na mahakama ni lawful or unlawful?

**Audience:** Unlawful.

**Com. Zein Abubakar:** Katiba mpya inasema una haja ya kuvunja. Hebu angalia kitengo tisini na nane, mnaona kitengo sitini na nane, the rights of arrested person, ukiwa umeshikwa wewe, unaona haki za kushikwa watu walioshikwa eh, every person who is arrested for ellegedly commiting an offense has the right:-

a) To remain silent.
b) To be informed promptly in a language they understand, one of the right to remain silent and two of the consequences of not remaining silent.
c) Not to be compelled to make any confession for that could be used as evidence against that person, aware any such person willingly chooses to make any confession such a compesion shall be made before a court or a magistrate.
d) To be held separately from persons who are serving sentence…………(Inaudible) watu siku hizi hushikwa na polisi akapekekwa akakae na watu waliohukumiwa. Angalia hii to be brought before a court as soon as he will report to and not later than 48 hours after being arrested, or not latter than the end of the first ………(Inaudible) after the departure of 48 hours if the 48 expires outside the ordinary court hours or for a day that is not an ordinary court day, or if some person is arrested from a court…………..(Inaudible) mnajua kuna watu wengine unaenda kushikwa mahali ambapo

mahakama iko pale ndio utapewa extention hizo. Halafu angalia mbinu, no person maybe remanded in custody for an offense if such offense is person…………..(Inaudible) or by a fine or imprisonment of not more than six months, okay.

Angalia pia on the rights of persons held held in custody, wanawake walituamilia kwamba wakati mwingine mwanamke anashikwa halafu anawekwa cell na wanaume, hakuna haki hapo………….(Inaudible). Haki ya kila mtu atawekwa katika cell kama ni mwanamke na wanawake wenzake, na wakongwe hawana haja kushikwa kuwekwa seli isipokuwa kwa jambo ambalo litamfanya mtu afikirie kwamba aidha ni kwa sababu ya yule analindwa au juu ya kubali anaweza kutokea ikiwa tutatumia hapa wengi.

La tatu uwe na sababu ya kutosha kuwekwa mtoto ndani. Halafu, angalia state of emergency hapo tulizoko, halafu application of the bill of right, mnoana hiyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Zein Abubakar:** Lakini kabla sijakaa chini, je na hii ni jambo ambalo wa Kenya wengi wameniuliza je, tutakapomaliza katiba nzuri ………(Inaudible) namna gani? Ni baadaye wanaenda kule wakaifikisha ………(Inaudible) wakaibadilisha katiba hilo. Naomba mwende kwenye chapter 18, ndio inazungumzia jinsi ya kubadilisha katiba, tumefika hapo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Zein Abubakar:** Ah, kitendo cha pili tusimamie, tumefika hapo?

**Audience:** Eeh.

**Com. Zein Abubakar:** Sasa tumetengeneza njia mbili za kubadilisha katiba. Njia ya kwanza ni ya kuhusu mambo ambayo ya inafaa kubadilishwa katiba hivi hivi bila kuwauliza watu, kwanza kabisa jambo hilo lazima ipitishwa na bunge zote mbili, kwa theluthi mbili, sijui mnanielewa?

**Audience:** Eeh.

**Com. Zein Abubakar:** Lazima ifikishwe na bunge zote mbili ikotoka bunge moja ipelekwe bunge ingine kwa theluthi mbili ya wa bunge wote, lakini pia utakapoweka mswada wa kubadilisha katiba lazima zipite siku tisini, siku ngapi?

**Audience:** Ninety.

**Com. Zein Abubakar:** Tisini kabla kwanza ule haujaanza kujadiliwa, kwa nini tukasema hivi? Ndio turuhusu………(Inaudible) siku tisini hizo, wakenya wajadili na ikiwa hawataki mabadiliko hayo wapige kelele na kuwaambia wabunge wao wasipitishe jambo hilo, halafu lipite kuandika bunge zote hizo mbili.

Na ikiwa mabadiliko haya hayaambatani na katiba ya sasa, yaani yanaharibu katiba ndio tukaweka njia ya pili ya kubadilisha katiba. Tunasema kuna mambo kadhaa ambayo ni muhimu sana, ikiwa yatabadilishwa lazima wananchi baada ya mswada huu kupita katika bunge sote mbili lazima kutakuwa na maoni ya wananchi ndio katiba ibadilishwe. Wanachi wapige kura wamekubali au wote wanakata jambo hilo. Mmekubali haya ambao ni muhimu ambao tumewatengea mkiwa wananchi wa ………….(Inaudible).

La kwanza, ni kuhusu mipaka yetu ya kitaifa tunasema itakuwa hata bunge haina haja ya kuuza hata kiti mmoja wa Kenya, ikiwa wewe unataka kubadilisha mipaka yenu, lazima urudi kwa wananchi wa Kenya waamue je, unataka kuuza ardhi yenu au si sawa hivyo?

**Audience:** Sawa.

**Com. Zein Abubakar:** Halafu, ukiangalia kitengo kinachofuatia ikiwa wanataka kubadilisha iwe sasa inaohusu madaraka ya wananchi, hawana haki hiyo mpaka irudi kwa nani?

**Audience:** Wananchi.

**Com. Zein Abubakar:** Halafu bunge likitaka kubadilisha the principles and values of the Republic, maadhili ya jamhuri hawana haki ya kubadilisha maadhili ya jamuhuri, hawana haki hiyo, hawana haki hiyo mpaka warudi kwa nani?

**Audience:** Wananchi.

**Com. Zein Abubakar:** Kama alivyozungumza mwambiwe mnakubali au mnakata? Halafu haki zilizowekwa katiba bill of rights, kile kitengo cha kahi za wa Kenya hawana haki ya kubadilisha hiyo mpaka irudi kwa nani?

**Audience:** Wananchi.

**Com. Zein Abubakar:** Wananchi, kisha kwa vile watu waliokuwa wakipendekeza devolution walituambui ile devolution ya mwaka sitini na tatu ilibadilishwa bila sisi kuuzishwa, ikiwa mtu anataka kubadilisha ……….(Inaudible) serikali za wilaya kujiambulia mambo yake lazima irudi kwa nani?

**Audience:** Wananchi.

**Com. Zein Abubakar:** Halafu kuhusu ……….(Inaudible) hawawezi kubadilisha sehemu ya isipokuwa kurudi kwa nani?

**Audience:** Wananchi.

**Com. Zein Abubakar:** Halafu tumesema ili wasiwe watu wa hilo walifanya ujanja hawezi kubadilisha kitengo hiki kinachohusiana na mambo haya. Mnajua anaweza kukiwa kufanya hivyo wanaweza kubadilisha kitengo hicho halafu wabadilishe, mmenielewa?

**Audience:** Ndio.

**Com. Zein Abubakar:** Hata kitengo hicho ona haki ya kubadilisha itakuwa ikirudi kwenu, sawa?

**Audience:** Sawa.

**Com. Zein Abubakar:** Sasa nitafanya kazi yangu ya mwisho ninaona sauti yangu inaanza kubweka, na mazungumzo hatujaanzia hapo, mazungumzo tuliyaanzia mbali na mazungumzo kama haya, utamwacha unaweza kuendelea kuongea utakaa hapa mpaka daima dawamu, kwa hivyo nitaifupisha kwa vile kusema hivi, nao kwa haki zenu mbele ya waraia wenzetu tuliyoka hapa na mbele ya Mungu mtu aniambie mapendekezo haya hayakutoka kwa wananchi wa Kenya, yuko?

**Audience:** Hakuna.

**Com. Zein Abubakar:** Wangapi wanaamini mapendekezo haya yametoka kwa wananchi wa Kenya na walitoka hapa kwenyu na yatatufaisha jamii yetu ya wa Kenya inueni mkono, mimi siinui mkono kwa sababu mimi nilikuwa shahidi. Inueni mikono, inje pigeni kelele nisikie. Kwanza mimi nimetimiza, nimetimiza kwamba leo nyinyi mmekuwa mahshidi na kuwacha nyinyi kwenye majukumu, majukumu gani haya? Kwamba ikiwa umesha………(?) ya uzaidi mbele ya watu wa Kenya na mbele ya Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu anaona nafsi zetu mbele yake au sivyo?

**Audience:** …(Inaudible).

**Com. Zein Abubakar:** Wale wanaosema mambo haya hayakufanywa na wa Kenya wana sababu gani? Sisi kama tume tumetimiza kazi mliotupa, mmetupa jukumu hakuna hata moja lililokushinda, sisemi kazi ilikuwa rahisi. Lakini tumeyatimiza kwa nguvu ya Mwenyezi Mungu na kwa usaidizi wenu kwa sababu nyinyi ndio mmefanya kazi. Kazi yetu ilikuwa ni kupokea maoni. Sasa nasema hivi, kuanzia leo, wengi wanafikiri kazi imekwisha anayefikiri hiyo hivyo nataka abadilishe maoni yake.

Niliwaambia mara ya pili nilikuja hapa, mwanzo wa ngoma ni wewe, sikusema hivyo na nyinyi mkasadiki mkasema mwanzo wa ngoma ni nyinyi, kweli walisema hivyo………...(Inaudible).

Na kazi imeanza sasa, sawa? Kazi imeanza saa ngapi?

**Audience:** Sasa.

**Com. Zein Abubakar:** Ikiwa una imani na mapendekezo haya, basi ni wajibu wako kuyalinda. Sina zaidi ya kusema, nawashukuru sana na ikiwa tunamkosea mmoja wetu hapa naomba mniwieradhi. Asanteni sana.

**Speaker**. Asante sana. Nadhani mumesikia hotuba yake. Commissioner Katiba ile ya kwanza ilibadilishwa ya Majimbo ilibadilishwa kimia kimia Bila sisi kujua sasa chungeni. Hii mimi nilipendekeza Majimbo. Nilipo isome sikuona neno moja la Majimbo lakini niliposoma katika magazeti nikona haina Majimbo nikaipenda kweli. Nikazungukazunguka nikaenda kwa mambo ingine nikasema jamani hii Katiba kweli ikweza kutumika tutajiona kweli tuko uhuru, uhuru kweli. Lakini kuna maono ati Katiba hii ni ya watu na hayo mimi nasema kwamba kutoka leo tutakuwa tukizungumza mpaka tarehe 28 wakati watakutana huko Bomas of Kenya katika lile kungamano ni wa jibu wetu kui-support haswa itakapo pitishwa tujitoe kabisa kabisa ku-support Katiba hii, kwa mfano katika District ni wananchi wanao ishi katika District ambayo watakuwa wamechaguliwa kuongoza Serikali ya Wilaya. Tusikubali mtu mwingine kuja kujiikeza hapo na kuanza ku-chokora chokora. Mali yetu tuta irinda kama sisi wenyewe tutajitoa kuendesha Serikali ile tunayo. Hii Katiba watu wengine wakiingia kutoka pahali pengine itaisha. Asanteni sana.

**Frida Mwadime**: Nafikiri tungemshukuru Commissioner kwa yale ambayo ametuelezia nafikiri tutaendelea kusema kwamba kitu ambacho mtaweka Katika hizia zenu ni kwamba huwa anazungumza na moyo wake wote. Na pia anasitahili pongezi.

**Audience**: Sana. Makofi.

**Frida Mwadime**: Haya tumpigie makofi. Mama mzee wa Commissioner wetu wa mambo ya Poverty Eradication, nasema makofi akisimama. Nafikiri tuna… kuna mmoja sijui atapata makofi. Hebu apate makofi ya kumshukuru.

**Speaker:** Basi kwa sababu nimepewa nafasi hii ninaongeza lakini nataka ile makofi ya mzee urrrrrrrr.
Makofi,urrrrrrrrrrrrr. Urrrrrrrrrrrrrrr. Asante sana.

**Frida Mwadime**: Asanteni sana. Ninajua maswali ni mengi lakini uenda tunapo uleza maswali tukasahau mambo matatu muhimu ambayo ningependa kutangaza kwa ajili ya wananchi wote ambayo wako hapo. Tangazo la kwanza ni kuhusu elimu hii na kuhusu keilelezo cha Katiba na reporti ya Katiba kwa wananchi Ma-Commissioners wa Tume wana adaa vitimbi katika

radio ya KBC siku ya Jumpili, idhaa ya kiswahili kuazia saa sita hadi saa saba. Watakuwa wana eleza kuhusu kielelezo cha Katiba na riporti za Katiba kwa minajili ya mwananchi aweze ku-fahamu na kuwa na ufahamu zaidi kwa hivyo muna ulizwa kusikiliza kipindi hicho ni ikiwezekana pia mpige simu kutaka kujua zaidi. Kama mahojiano vile ilivyo kuwa wakati wa elimu ya raia. Halafu, kingereza ni saa tisa hardi saa kumi, siku ya Ijumapili, na kama kuna swali kuhusiana na nyakati hizo na saa hizo nafikiri tutamuliza Commissioner baadaye.

Tangazo la pili ningependa kuwatangazia wananchi wote wa Voi constituency ni kwamba tuliweza kuchagua wale waakilishi wetu wa tatu wa wilaya katika National Constitutional Conference tarehe kumi na saba pale County Council Chambers. Na wale ambayo wamekuwa wakifuatilia mambo haya, moja ni Isabell a ambaye alikuwa …………… ni Town Council Councillors kwa sababu ki-sheria, ndiyo wanao akilisha Wilaya. Kwa hivyo tuliweza kupata viongozi wetu mashujaa wana elimu ya kutosha na uzoefu wa kazi ya kuhusu mambo ya uma na ikiwa ni lazima mmoja wao awe mwanamke tulimpata Mrs Mariama Mwagoko abaye ni Makelele graduate amekuwa academician kwa miaka mingi, na amekuwa kiongozi lakini sasa ni mfanya biashara pale Undanyi. Wa pili ni Councillor Joel Haji, nafikiri wengi wenyu mnamfahamu kwa sababu ni mwana siasa na pia ni Councillor. Wa tatu ni mzee Osomoni Omollo ambaye amefanya kazi katika mahakama na pia alikuwa ni Mbunge wa Taveta wakati ulio pita. Kwa hivyo hawa ndiyo walio chaguliwa na wale walioko pale watakubaliana na mimi kwamba hiyo kura ilipigwa bila utatanishi wo wote. Kama kuna swali mtauliza baadaye.

**Interjection:** murmuring.

Sawa. Tangazo la mwisho ni kuhusu mikutano ya Tarafa. Kuanzia pengine kesho ama kesho kutwa, mwana Kamati ambaye ana kazi pale pale kwa tarafa katika sehemu hii ya wakilishi Bunge watadaa mikutano ya ki-baraza kujadili zaidi na kama kuna wezekano wananchi kutoa mapendekezo zaidi kuhusu chelelezo cha Katiba basi ni sawa maana tumepewa siku thalathini na tulianza tarehe 27 mwezi wa tisa kwa hivo hizo siku sinaendelea. Asante.

**Speaker:** Nina swali moja kwa huyu madam na maswali mawili kwa Commissioner**.** Kwa Commissioner ni kwamba watu walio chaguliwa ku wakilisha watu wa Taita Taveta.

**Interjection:** Long silence.

**Speaker**: Huyu mtu hakuna maana kitu hicho twaomba kirekebishwe, watu wa Voi pia twapenda kuwakilishwa. Commissioner vile twapendelea kuna jambo limenipita la kwamba watoto wanao zaliwa katika nchi ya Kenya wanasitahili shule hiyo ya bure, wanasitahili wakipitisha umri miaka kuma nani wapate passporti na vitabulisho. Kuna kitu sasa nitaguzia, napendekeza kwamba lazima mtoto akifikisha umri wa miaka kumi nane ambaye ni mzaliwa wa Kenya, Serikali imuhakikishie ardhi.

Na la mwisho ni kwamba labda umezidikiwa ama labda sijafahamu je Waziri Mkuu na mdogo wake ni lazima wawe Wambunge au ni moja moja? Asante.

**Frida Mwadime:** Nafikiri ninge jibu hili na kwa kuwa tuko na Commissioner hapa ni swali rahisi sana. Ili tuweze kutoa wale watu watatu kulikuwa na sheria ya ki Katiba kulingana na cap. 3A na sheria hiyo, haikutaja kwamba kuwe na wakilishe sawa kwa sehemu za wakilisi Mbunge katika Wilaya that is one. Two, nisikilize basi baba. Nominations za watu waliotaka kuchaguliwa was free for all. Bila kuchagua wake ama wanaume na isitoshe wanawake walipewa nfasi ya kwanza kwa sabuli yao pekee yao ijapokuwa ni moja tu tulichague. Tatu, ilikuwa ni kwamba Wilaya ipeleke watu wa tatu kama wangetaka watu watoke Mwatete haingekuwa shida, Undanyi wa tatu haingekuwa shida, uchagunzi ulitegemea County Council Councillors. I have no role to play I was a mere as Returning Officer. Na mzee Bahati kama Mwenyekiti wangu wa Voi kama anaweza kutoa ushuhuda huyu. There is no way I could temper in this election.

**Com. Abubakar zeine Abubakar:** Na sema je, katika kutenda kazi kwake bi Madime katika utandaje kazi wake Bi Madime hajafanya makosa. Sheria ilitungwa na wana Mbunge yeye yuaitekeleza. Sio, kwamba katika utungaji wa sheria pengine si kila mtu akawa na furaha. Jambo ambalo lilikuwa likinifanya saa zingine mimi na gutuka usingizini na sema watakapo piga kura kule Taita Taveta, wapige kura wachague wote watatu wa Taita wasimtie Mtaveta mtakapo kwenda kule vita nitakavyo vipata mimi Mungu ndiyo anajua. Nilipo kuja mzee ndiye amechaguliwa nikasema nitakuwa lakini nilijua kuna maswali kama haya.

Ni nini muhimu kuhusu uakilishaji wenu? Si delegates hawaendi kukaa na muhimu mujue hivyo ni muhimu mueze kuzungumza nao sasa. Wasienede kule wakaenda wakajiwakilisha wenyewe. Halafu tatu, ni vigumu sana kupata kila mtu mwenye ujuzi mwajua wengi wenu mliyuko hapa mlikuwa masitahili kuwa katika mkutano huo lakini si rahisi ilikuwa ni tharura kila wilaya watu wa tatu kwa hivyo mfahamu tusitiwe baridi tukupali mambo haya. Isipo kuwa ikiwa una imani kabisa kwamba waliochaguliwa hawafai kwa sababu hawana elimu kama inavyo takikana walichaguliwa kwa kupitia njia zizo sahihi mna haki kutuandikia sisi na kutupa tia maoni sawa.

Halafu, tulichagua sisi County Council iwe ndio kitengo cha kuchagua watu hao kwa sababu katika kila wilaya nchi nzima kuna County Council lakini mji wa wenye hadhi kama huyu wa Voi, unaweza kuwa kuna wananchi tofauti lakini kuna miji mingine mdogo mdogo haina Municipal Council. Kwa hivyo ukiamua Muncipal Council ndiyo zichague basi itakuwa Wilaya zingine hazina watu wa kuwachagua. Kwa hivyo ikachaguliwa County Council kwa sababu it is common in ……. in the District si kudharao Muncipal Council ambazo sina hadhi au jiji kama la Nairobi sasa Nairobi walisema mara ya kwanza walipo ambiwa wachague watu wakasema sisi hatuchague kwa sababu nyinyi mnatudhara kwa nini mwatumpa watu watatu kama watu wengine. Tukawambia sheria ni sheria ni msimano wa kata mbele na nyuma. Watu watatu mwachague chagueni hamuna sheria pia imetupa sisi mamulaka kuteua mkikataa tutateua watu wa tatu kutoka Nairobi.

Halafu swali lako kuhusu Waziri Mkuu. Wale waasidizi wa Waziri mkuu, Makamu wake. The two Deputies Prime Ministers

lazima wawe Wabunge. Pengine ni ngepokea maswali ya watu watatu au wa nne halafu ni yajibu kwa upesi.

**Richard Mwakeka**: Asante Commissioner Abubakar Zein na wote mlio kuja. Mimi ni na swali lakini si swali. Jina naitwa Richard Mwakeka. Wakati ulipo kuwa ukiongea ni kama uli kuwa ukiongea kwa sababu Commission hii imehudhiwa na nikapatwa na ugonjwa upia. Lakini kusema ukweli, ikiwa ni kiongozi wa nchi anasema ati hii Katiba haifai Kenya inafaa Ulaya tutamwelewa je? Sasa ndiyo tunajua shida na wananchi wa Kenya yeye ndiyo Rais wa Kenya. Lakini ulivyo zungumza wewe ni kwamba tufuate Katiba hii sisi ndiyo tulitoa maoni yetu kwa hivyo mimi pia ninge kutia moyo si swali. Kwa sababu tumeelewa haki zetu sasa ni kwamba tunakushukuru. Tena kuna mahala ambapo kidogo nilikuwa nataka kulegelezwa. Ningetaka Katiba hii muongeze kitu kidogo ndani kwamba hii mambo ya burial permit, mpaka mgeni akiwa burial permit inaweza kubukwa hiyo iondolewe. Kutakuwa na njia ya kutengenezwa.

Langu la mwisho ni kwamba mambo ambayo yanaendelea na Wabunge ama na hawa ndugu zetu wengine wa mahakama, mimi nina pinga singependelea waendelee. Thank you.

**Sulemani Ramadhani**: Kwa majina naitwa Sulemani Ramadhani. Swali langu ni kuhusu kitengo 105. Zamani nilipo kuwa mdogo niliuliza habari ya Katiba niliambiwa ni ya majimbo. Nilipo uliza kwa nini Majimbo zilikufa nikaambiwa Kenya haikuwa na pesa na sasa nauliza tena, je Kenya itaweza kuwa na hizi nyumba?

**Jemimah…**: Asante Commissioner na wanzake jina langu naitwa Jemimah… Umetuzungumzia mengi natumefurahi isipokuwa mwisho mwisho umetwambia sasa kazi ndio inaaza sasa swali langu liko hivi Je hiyo general election inayo kuja itafanyawa na Katiba mpya ama twa ngojea? Labda itatumika ile ya zamani? Hilo ndilo swali langu.

**Christopher Kayanda**: Bwana Commissioner na viongozi walioko mbele hapa, mimi naitwa Christopher Kayanda. Ni lazima tuseme mawili kwa sababu tulikuwa tuna fikiri tumefuga paka kumbe tumefuga shiba ndani ya nyumba na inatutarua. Ni wananchi walio piga kalele hii Tume itengezwe. Kiongozi wa nchi hii akakubali leo atwambia haitambui kwa sababu hakutoa maoni yake na haitafanya uchaguzi. Mimi kwa niamba ya Wanakereketwa mimi na wale wana ukatili rohoni nasema bila Katiba hii hakuna uchaguzi. Kwa sababu Katiba hii ita mwakilisha munova, kiwete, kiziw na wale ambao hawa jafikia kiwango cha kule juu cha kufunga tai. Kwa hivyo wewe peleka ujumbe kwamba Wataita wanasema bila Katiba mpya, hakuna uchaguzi.

Kisha tunaomba Bunge lililoko limzuie kabisa asitumie nguvu za kusema yeye ana prerogative. Hiyo ni ya kuumiza kwa sababu tumeona waliotoa maoni yao kwamba hawataki Uhuru Project wamenyanyaswa. Kina Saitoti na wale wengine. Sisi wengine hatuna uongo ukinitambulisha hapo nitakushukuru.

Kipengele kingine ambacho nilikisikia na ningekuomba ni kwamba tumepata habari ya Serikali ya Wilaya, lakini Serikali za Mitaa kama Municipality hatujajua katika Katiba mmizeweka wapi? Na kama ziko zitachaguana ki-Muncipal au itakuwa ni

katika Wilaya?  Hilo ndilo swala langu.

Mwenye kiti nina kushukuru sana naona umesha tuarika tumechukua haya.  Na kushukuru vile nakuona wewe ni bingwa kweli.  Na kwambia kabisa wewe ni bingwa usipitishe

**Interjection**:  Noise.

**Com. Abubakar Zeine Abubakar**:  Vile nilikuwa nasema naomba ni yajibu hayo yenye mmeuliza halafu niende mengine.  Kwanza kabisa napenda kuwashukuru watu ambao pengine wananipaka mafuta kidogo.  Ninge omba tuende kwenye kazi.  Kwanza nilianza kwa kusema sifanyi siasa mimi sijui mlisikia hivyo?  Kwa hivyo ningewaomba mambo yanao guzia siasa ni si yaajibu au si sawa hiyo?  Kwa sababu kiapo changu cha kazi haki ni ruhusu mimi kuzungumzia siasa.  Sasa ningejibu swali hili la kwanza.  Sasa naenda kwa Bwana Makeka  swali lako kuhusu habari ya burial permit.

Nadhani ni muhimu sisi kufahamu si mambo yote tunaweza kuyaweka kwenye nini?   Kwenye Katiba.  Kuna mambo mingine yataenda kwenya sheria sitakazo tungwa na Bunge, na mambo ingine itaenda katika sera za Serikali za Ki-taifa? na zile za Wilaya na sehemu zingine.  Kwa hivyo nyinyi hapa wenyewe maweza kujiamulia njia ya kutoa permit.  Sidhani permit ni kitu kibaya maanake ukiwa unasema hatutajua nani amekufa, mmenielewa?  Kwa hivyo lakini mta tumia njia za kurahisisa mambo hapa hapa wilayani mtajeamlia njia gani ndiyo rahisi kweli.

Halafu kuhusu swali hilo liliulizwa kuhusu kitengo 105, linalo husu Bunge mbili.  Anasema kwamba aliambiwa alipo kuwa akikuwa kwamba sababu ya kufungwa kwa kumbi kumbi la pili ya Mbungi ilikuwa ni ukosefu wa pesa.  Sidhani hiyo ndiyo ilikuwa sababu.  Yule aliyekwambia ungemwabia akueleze vizuri.  Pengine alikuwa anataka nataka kukueleza kuwa, Serikali Kuu ya Taifa ilizua pesa hizi ili kuziua.  Au na sema uongo mimi?  Sio pesa zilikuwa hakuna, fedha zili zuiwa na si ngependa kusema sana.

Sasa viongozi wanazungumzia kuhusu Katiba hii tunayoipendekeza pamoja na uchaguzi.  Ukisoma ukaraza wa 75 wa hiki kitabu chetu na usione na weza kutaja bila kukiangalia kwa sababu sisi wenyewe ndio tulikiandika kwa hivo tunajua tumeandika nini wapi.  Kitabu hiki ukikiangalia ukaranza 75 unazungumzia mahali panapo sema conclusion, tume eleza musimamo wetu kama Tume kuhusu Katiba. Tunasema ya kwamba ingekuwa ni jambo la heri na manufaa hapa nchini kwetu ikiwa tunaweza kuepuka kufanya uchaguzi December. Tutakuwa hatujafunja Katiba yeyote au kufunja kipindi cha sasa cha Bunge. Kipindi cha sasa cha Bunge kita isha ikiwa hili Bunge halitafujwa mapema na Rais ambaye ana uwezo huyu na si mulaumu Rais.  Katiba ya sasa imempa uwezo huo.  Ikiwa atatumia uwezo wake wa kufuja Bunge kabla hapa ni jambo lingine. Lakini ikiwachea tu Bunge liendelee kwa muda wake mpaka kipindi chake kitakapo isha, kipindi cha Bunge hili kitakuisha Februari tarehe nne.  Kwa sababu waliapishwa Februari terehe 5 mwaka wa 98 miaka mitano kutoka Februari tarehe 5 mwaka 98 ni Februari mwaka ujao tarehe 4 ndio kipindi chao kina isha.  Na sisi kama Tume tukasema kwamba kufikia Februari nne tutakwa tumesha ikiwa

kuna nia ya kutimiza Katiba hii. December Katiba hii itakuwa isha kubaliwa. Ikiweko nia.

Kwa sababu tumepanga kuita mkutano wa kitaifa tarehe 28 na kwa majadilio yetu ambayo tumeyafanya. Sisi tuliongea tukasema wakati huu tutawaletea Katiba? si hiyo na Gitumeileta.
Mtuamini kidogo pia kwamba, ikifikia tarehe 28 tukianza mkutano, ikifika tarehe 27 November tutakuwa tumethibitisha Katiba hiyo katika mkutano halafu itachukua wiki mjo kupitishwa Bungeni. January na February tutumie wakati wa kutengeneza seheme za Katiba zinazo taka kutekelezwa haraka. Bunge likufunjwa Februari italazimika Bunge lingine likutane baada ya siku 90. Sijui mwanielewa? Kutokia Februari siku 90 kwa hivo tuna muda wa kutosha lakini ikweko nini? Nia Nadhani nia inahusu mambo zaidi ambayo mimi naenda kuyashughulikia. Nadhani ni hayo tu. Kuna swali ambalo si jajibu? Eh. Ume uliza swali kuhusu vyama via politices. Zitakuweku isipokuwa hazi takwako katika County Council mbele. Kwa sababu ukiwa tuna Serikali ya Wilaya hatutahitaji County Council. Tutakuwa na Serikali ya Wilaya halafu tutakuwa na Serikali zinazo simamia miji. Mahali ambapo miji na Serikali ya Wilaya imeingia za sambamba tutatoa special status for that town, sijui kama mna nifahamu? Sawa.

**Elias Mwachika**: Swali lingine, hamjambo? Mimi kitu ambacho ninaweza kuwaambia na ninawaomba, majina yangu ninaitwa Elias Mwachika Mbere. Mimi na waomba kama nyinyi mulioko hapa na wengine walio nje. Katiba hii muwe mikijua kuwa ni draft na this is one word tulisema kuwa hii Katiba hatujaisoma vizuri tuka ielewa ndani yake. Tafadhalini nina waomba muelewe na ndio tuseme hii Katiba tuwataka kwa sababu jua kuna kubadilisha na kuongeza si ndiyo? Kwa hivyo tuielewe tafadhali. Hili ni jambo muhimu sana, kwa sababu mwingine atasema mimi na elewa na mwingine kule nyumbani bado hajaielewa na hao walioandika hii Katiba ni sisi tuliwatuma na muwe mkijua pia hao ni binadamu. Pia wao walikuwa na makosa wakiandika haiwezekane ati walikuwa right kwa kila kitu. Mimi nisha ongea na ma lawyer fulani Nairobi wakaniapia hapo ndani pia kuna mambo ingine si ya kweli si ya kurekebishwa. Kwa hivyo tusije tukasema ati ni nzuri ama pia tuisomeni tuielewe tafadhali, tafadhalini.

**Com. Abubakar Zein Abubakar**: Ngoja ngoja alisema huyu Bwana ni jambo muhimu sana. Kwanza mimi nilianza kwa kusema kwmba sisi hatusemi hatuna dosari. Siku sema hivyo. Kisha na sababu ya sisi kutoa nakala hizi ndiyo msisome mzielewe muhakikishe mambo hayo yamo ni yenu ya na yanawafaa najua kuna dosari hapa.

Kitu ningependa kumkosoa Ndugu yangu usisikia watu wana kwambia mimi lawyer kuna mambo yanayofaa kuondolewa. Mueleze yapi? Mambo haya ni onyeshe na yapi ambao unataka tutoe. Ama si uvume umo. Ama hakuna Uvumi? Kukosoa si kusema hiki ni kitu kibaya hiki ama kitu kizuri. Sema uzuri wake na ubaya wake? Wame kuambia kuna ubaya wakuonyeshe. Wamekuonyesha? Nionyeshe na mimi basi, eh hayo ndiyo ukimuliza mwenzako ndio tuzungumze. Hili ni jambo la uma kuna siri? Ingekuwa kuna siri tunge kucha kugawanya makaratasi hivi tuzungumze? Tuna piga mangoma sisi ….someni weeee………someni……. Mimi. Ngoma twa zipiga na ni muhimu kusoma ni kasema nini? Somani na muende mkawabie wali watu wanao wakilisha matakapo fika kwenye mkutano wa kitaifa semeni hivi, semeni hivi, haya twa yakubali, haya

hatuyakubali. Hapa kumepunguwa hiki ongezeni hiki hatukatai sisi haya ni yeni si yetu sisi. Sijui muna ni elewa?

Na kama huyu ndugu yangu anavyozungumza hapa ana haki ya kuzungumza na aliyo sema si mbaya na angekuwa amesema mabaya ninge mwambia pia ana haki ya kuyasema. Sio vizuri akisema jambo ambalo pengine watu wengi hawalikubali niseme ametumwa huyu sio vizuri. Kitu kingine cha ni furahisha mimi ni kusema haki ya kusema haki zenu. Mua haki ya kusema lakini hapa anaambiwa ayaseme sawa? Na ngesema hivi naona kuna watu wanaenda wakirudi. Naona kama watu wame anza kuchoka. Ukiwa una swali muhimu uliza swali mara moja. Ukiwa una jambo la kusema kuhusu Katiba hii useme mara moja. Nitachukua mengine matano. Tueze na huyu mzee.

**Patrick Masese**: Nashukuru Bwana Commissioner. Majina yangu ni Patrick Masese. Mimi nina swali moja ingawa limeulizwa na wananchi. Wananchi wanalalamika kuna Katiba ya sasa inawanyanyasa sana. Maana anajenga nyumba yake anamaliza pesa kabisa nyumba ina ingiliwa, mpangaji ana haki ule mwenye nyumba hana haki atalala njaa na nyumba inalala na mtu akifunga hiyo nyumba kidogo anashikwa anapelekwa Police anaenda kuhukumia ni si mkusaji. Sasa hii iko upande gani?

**Omari Kilabu:** Nafikiri mimi kwa majina naitwa Omari Kilabu wa Kinango. Swali ninalo taka kuuliza hapa ni kwamba, la kwanza ni la huyu mama na ni msichana wetu amesema ameandika wetu Taveta kwa hiyo Tume kwa mambo ya hii Katiba. Ukiwa unataka kwa majina kwanza ni Judge. Ni mama mwenye elimu sana, nifikiri ata yeye alihusika kwa uchaguzi huo

La pili hapa Taita Taveta watu wengi wame poteza maisha wameuawa na ndovu hii sheria hakuna watu hawalipwi, yangu ni hayo tu.

**Jacob Munyalo**: Mimi naitwa Jacob Munyalo. Mimi natoka kwa sirikisho la waifanya kazi, mimi ndiye niliwakilisha hiyo riporti katika Wilaya ya Taita Taveta. Swali langu nina zungumzia kifungu namba 55 inayo husiana na mambo ya ufanya kazi. Nilikuwa nataka niseme ama niulize ama nimeonelea kwamba, wangapi wamesikia Waziri wa Labour akisema huu mugomo ni halali au si halali. Hapa kifungu namba D cha 55 kinasema. Kiko silent bado sijapeta fahamu kwamba tumepatiwa uwezo wa kugoma ama tukiwa tumegoma tumefanya makosa? Hilo ndilo tu ndilo jambo nili lo taka kuuliza.

**Speaker:** Commissioner na wananchi mlioko hapa. Hamjambo? Basi Bwana Commissioner nina swali moja ambalo sija lipata kuhusu mambo ya Insurance. Kuhusu mambo ya Insurance kwa mfano kama mtu amepata ajali bara barani halafu wakili anafuatilia hizo kesi kudai kulipa yule Bwana aliyepata ajali, kama ni mama au mtoto lakini hizo pesa uwa hazifikii wale watu walio husika na ajali. Sijui umeweka Kifungu gani kusudi wale watu walio umia wapate hizo pesa zinatoka na hazifikii hawa wenye kudai?

**Manyara**: mimi ni kuhusu. Jina langu naitwa Manyara kuhusu saa za kipindi. Kuwa hicho kipindi ni siku ambapo watu wengi sana hawaendi kazini. Lakini watu wengi wako busy kwa mambo ya ibada, kwa hizo saa za muchana kwa maoni yangu na

wale wengi ambayo nao jua ama naongea hapa kwa niaba ya wengi. Katika Kenya watu wengi watakua wanashugulika na mambo ya ibada na shughuli za ibada. Kamati au Committee naomba kama hicho kipindi kingekuwa usiku ungekuwa vizuri sana.

Pia kuhusu kazi. Katiba kama itakuwa imepitishwa na sijui itakuwa vipi mwananchi ataipata na mna gani maanake kama saa ingine ningelifanya ikawa ni biashara itabidi niwe nimeisoma Katiba vizuri kwa sababu nina weza kuwa nafanya mambo mengine kube mwananchi mwingine hakuyaona ni manzuri akanipeleka kortini. Sasa nauliza tutaipata vipi hiyo Katiba ili kusudi ni ipitiye ndiyo maanake kwamba ninapo fanya mambo yangu nisije nikashtakiwa?

Jambo lingine ni kuhusu, kwa mfano ma-Judge. Judge analipwa mshara wa kutosha ame elezea mali zake. Kwa hivyo haruhusiwi kuchukua hongo na sasa hiyo itakuwa ni kipimo cha ku hakikisha kwamba hachukui hongo kwa sababu mali zake tunasijua kwa kiasi. Lakini nje akiamua kutumia kwa njia anasa labda aamue anaend akunyua Tanzania na ndege na anarudi jioni. Weekend anaende nchi ya mbali na anarudi kesho na ile ndege ya haraka na ile ni njia ya kutumia hizo pesa za hongo ndiyo ziisha haraka haraka.

**Ambrose John Nyangi:** Jina langu ni Ambrose Nyangi na mimi niko na maoni yangu juu ya proposals mbili katika Katiba. Katika Katiba mmesema munataka mu-abolish death peanulty. Tena mu-abolish nini copral punishement. Nadhani hiki ni kitu kikibwa sana kisichanganywe na mambo mingine ya Katiba. Kitu hiki tungezungmzia baadaye. Zile nchi ambazo zili-abolish death penulty walifanya referendum ilizungumzwa na watu wote halafu wakafanya referendum. Kwa hivyo ningeomba lisiingizwe katika Katiba sasa, lakini possibly liwe refered kwa ile Commission ya human rights. Hiyo na copral punishment. Kwa hivyo hii punishement kuondolewa, mimi naona ni makosa. Kwa sababu kwa mfano, juzi juzi hapa kulikuwa mtu moja alipiga bibi yake akamtoa macho sasa tukisema tutoe copral punishement mtu kama huyu apati kufanya hiyo makosa. Mtu kama huyo haitaji kiboko nadhani kuondoa hii copral punishment si vizuri. Yangu ni hayo, tu.

**Timothy Malwa:** Hamjambo wenzangu? Mimi ni Timothy Malwa. Swali langu nitawauliza tu, naona kama ile hali iliyoko sasa tunaelekwa uchaguzi lakini hatujui uchaguzi watakuwa tarehe ngapi? Sasa hiyo imekuwa ikitatiza Wakenya wengi kwa hivo mimi nilikuwa nauliza kwa Katiba hii imekuwa stipulated ki vipi? Nilikuwa nataka kujua tu, ikiwa tuta kuwa na five years term tujue mwaka wa 2004 December tarehe 22 ama kitu kama hicho, tutakuwa na uchaguzi kwa hivyo wananchi wote watakuwa wanajua kuwa uchagunzi ni siku fulani mwaka fulani ili kusiwe na mtu wakuweka wenzao katika hali abayo haijulikani kama vile tumewekwa sasa. Hatujui Bunge litafunjwa nini? Hatujui uchagunzi utakuwa nini? Imekuwa kama ni personal issue lakini tunataka iwe National Issue, kila mwananchi hata mtoto akizaliwa leo ajue kuwa uchaguzi utakuwa siku fulani, Bunge litafunjwa siku fulani ni kitu kama hicho.

**Victoria mwabuga:** Kwa jina naitwa Victoria mboi Mwabuga. Langu ni pendekezo tu, kama wananchi wakikubali. Pendekezo langu linapitia juu ya shule ya upili. Fungo la kumi na tatu. National days. Kwa sababu mazingira ya imeharibika

sana ningependekeza ya kwamba siku moja ya hiyo National days iwe ya mazingira tuende tukatengeneze mazingira lakini ni kama wananchi wakitaka sio yangu.

**Elijah Opore:** Jina langu ni Elijah Opore Utanisamehe sauti yangu ni mbaya kidogo. Langu ni, pendekezo. Pendekezo langu nikuwa nitazungumza kwa kifupi ndogo ndogo… ulale Friday, Saturday, Sunday, Monday. Nilikuwa naomba pendekezo langu tuko na holiday nyingi za kutosha. Langu ni hilo.

**Harman Mwalukuku:** Majina yangu ni Harman Malukuku na swali langu linahusu umilikaji wa ardhi. Tumejulishwa ya kwamba, mgeni hana haki ya kumiliki ardhi isipokuwa ana haki ya kukodi. Lakini swali langu ni kwamba tunaambiwa wale wageni ambao tayari wanamiliki ardhi nchini kwetu watapewa lease ya miaka 99. Sasa hiyo miaka 99 sioni si mapendekezo yetu sisi. Kwa hivyo naona kwamba kama kuna uzekano miaka hiyo ipunguzwe.

**Interjection**: Miaka mingi.

**Michael…**: Majina yangu ni Michael …… kitu ambacho nimekisikia na nikawa na maswali ni juu ya uraia. Yaani mgeni akioa Mwanakenya bibi yake anaweza kumfanya huyu bwana awe ni mwananchi wa Kenya na vile vile mwana Kenya kulingana na Katiba ana haki ya kurithi ardhi. Kwa hivyo huyu mgeni anaweza kuwa, aje Kenya aoe, awe mwanakenya na apate ardhi halafu, aachane na bibi yake. Watu kama hao kuna nafasi ya kuwatambua?

**Speaker:** Bwana Commissioner na wenzangu wote. Langu ni juu ya hawa watoto ambao wamepewa elimu ya bure ya kutoka std 1 mpaka 8. Hiyo niipongeza sana, lakini naona kwamba kwa sababu kuna yatima wengi wanao ongezeka. Serikali ingechukua wale ambayo wanaenda High school wanaenda, masomo ya university kama ni mtoto yatima Serikali ichukue hawa. Maanake watoto wakifika std 8 wasi-drop-out. Kwa sababu fees iko juu zaidi basi twaweza kupoteza Wanakenya wanzuri ambayo waki ongoza Kenya kesho. Kwa hivyo kipengele ungewekwa baada ya watoto kusoma bure mpaka 8 na wale ambao wamebahatika wana akili nyingi na ni watoto yatima wapewe uwezo wa kusoma. Serikali ichukue jukumu la kuwasomesha mpaka wamalize kwa sababu hizo bongo lao laweza fanyia Kenya kazi.

**Godffrey Mwandigo:** Bwana Commissioner na wote ambayo wako. Mimi naitwa Mwandigo. Swali langu ni moja tu. Nimesikia kwamba ukisema kuhusiana na maamuzi. Kwa mfano matumizi, yale ambayo yatatoka katika District kama hiyo. Ya takuwa yana amuria hapa hapa na yanafanywa hapa hapa na mkumbwa atakuwa ni District Administrator. Lakini huko juu naona kama kuna kivuli fulani maana kama ya kwamba kuna Serikali hii ya Wilaya bado kuna Serikali ingine. Sasa sijui kama hawa watakuwa ndiyo wana-recommend wanapeleka kwa wale wa-approval ama ikisha kuwa approved hapa ni kabisa. Kwa sababu huenda tukakubali labda ndio kuwe na hali kama hiyo. Lakini bado hiyo ni kwamba haikushugulikiwa Taita bado tena ikenda uko mbele kwa Serikali kuu inataka ipewe approval ndio mambo ifanyike. Kwa hivyo hapo sijui kwamba iko namna

gani? Swali langu ni hilo.

**Mohamed Ashra Abudi**: Kwa majina naitwa Mohamed Ashra Abudi. Swali langu ni moja kuhusiana na haki za kibinadamu. Kuna sheria moja iliyoko katika Katiba hii ya sasa kwamba kutojua si hatia. Sasa sijui ni wapi tumeweza kupatiwa nafasi ili mwanadamu achukue haki yake ya kutojua kwa sababu bado upeo wa kiwango cha elimu katika Kenya, hatujakipata kama vile tulikuwa twatarajia ili mtu akeweza kuiba pahali fulani hizi sheria za kanyanga kama vile upite pale katika Rail mama mzee hajui kusoma kibao kiko kimeandikwa trespass, yeye atafuka pengine asitakiwe kwa kutojua kwa hivo nilikwa provision hiyo iko wapi katika human rights katika Katiba hii yetu mpaya?

**Livingstone Mbori**: Jina langu naitwa Livingstone Mbori nami nilitaka tu kuliza juu ya hizi national Parks ambazo Taita Taveta ndiyo ni kama vile zimeruandikwa hapa. Unajua wakati wa ukoloni. Wabunge wameuliza hiyo, Wabunge hata nikiwa kijana zamani nilsikia Mbunge wangu aliuliza ati kwa nini hii Taita Taveta. …Na shida hapa tutakaa nayo mpaka nini kwa sababu Taita Taveta sisi ni wachache kweli lakini ikiwa kweli lakini kama kungekuwa mashamba ya kutosha si ingesaidia watoto wa Taita Taveta kwa elimu na mambo yote haya. Utanisamehe kama nimeenda sana pengine ni kavuka mpaka lakini langu ni hilo tu. Asante.

**Ezra:** Mandugu zaku mabibi na mabwana hii ngoa yetu ilitutoa. Mimi staki kusema mengi. Jina langu ni Ezra, swali lako ni kutoka draft hii. Nilisikia kuna kipengele ambacho nilikisahau, kuhusu Council zetu na wale watakao gombea hizo viti, kwa sababu tulipendekeza zigombewe na wazaliwa wa hapo. Na pia umilikaji wa ardhi, tungependa muweke vipengele ambavyo vinaeleza umilikaji wa ardhi. Sana sana kuhusu kiasi cha shamba ambalo mtu anafaa awe na kiasi gani?

**Com. Abubakar Zeine Abubakar**: Mzee Agaustine lako sitalijibu. Nadhani umesikia ujumbe wako umetoa, nadhani umesikia. Na penda kumuhakikishea mzee aliye sema mwisho kuhusu Buga za wanyama kwamba hajafuka mipaka. Katiba haina mipaka na nadhani wale walikuako hapo wakati tulipokuwa tukipokea maoni ya wa Kenya mulisikia wengi wa Kenya walizungumzia wanao ishi hapa kuhusu muingiliano wao na wanyama wa bori katika buga hii. Ndiyo maana ni kazungumzia kuhusu haki zenyu za kihistoria. Si hiyo ni moja inayo husu historia? Sio? Tutatengenza njia ya nini kupata frusa ya kuzungumzia vipi mtapata haki zenyu za kihistoria. Lakini juu ya hayo tumekubaliana kama kuzo, kama abili kwamba sehemu yoyote Kenya wapate manufaa kutokana ni rasirimali zilizoko karibu nawao. Kama Buga la wanyama iko na nyinyi kwa nini musipate rasilmali? Na nyinyi ndiyo mtaunda Serikali ya wilaya hapa hatutaki muwaue wanyama wote na mumeishi na hawa wanyama mpaka leo ikiwa hamjawaua mtaaza sasa. Kwa hiyo hayo yasiwatie shaka.

Lakini nitaanza na Patrick, kuniuliza mimi kuhusu haki za mwenye nyumba nadhani hatukuweza kutia haki za mwenye nyumba na haki za mpangaji ndani ya Katiba. Haki za mwenye nyumba na Mpangaji mtaziamua wenyewe kwenye Serikali zenyu huko chini. Nyinyi wenyewe muamue lakini huwezi kusema mwenye nyumba pekee yake ndiyo ana haki na mpangaji hana mtamua wenyewe chini kwenye Serikali zenu munataka haki yenu itekelezwe vipi?

Halafu kuhusu conflicts between animals and people Mzee Omari Kerabo nafikiri nimejibu hilo nitaishugulikia.

Kitengo 57 kuhusu strike Kutoka korti. Nadhani wale ndugu zetu wamekubali ya kwamba Katiba ya sasa haizungumzie mgomo. Haki ya mgomo kwa mfanyi kazi Katiba ya sasa haizungumze haki ya mgomo kwa mfanyi kazi. Katiba ya sasa haizungumzie napendekeza Katiba inayo kuja inasema wafanyi kazi wawe na haki ya mgomo hiyo ni haki yako ya kimusingi ya kikatiba na hakuna mtu anaweza kukunyaganya. Kitu ambacho kitafanywa ni kwamba Mbunge litahusika kutengeneza sheria inayo husu haki hizo ili kusiwe na mfurugano ambayo hauna mwelekeo. Sijui kama mwaniifahamu? Lakini sheria iliyotunguwa haiwezi kuvunja haki hii inayopewa na Katiba.

Halafu Andrew Mulango kuhusu Insurance. If you look at the section of Public Finance, hatuwezi ku-include haki za watu kuhusu mawakili ambayo wanawakilisha watu halafu huvunja haki yao. Kitu tumefanya tumezungumzia kuhusu Legal Profession na pia watakuwa na Code of Conduct nilisahau kwambia kwamba pia katika kuweka mahakama pia kuna Judicial Service Commission na pia kutakuwa na njia kuadhibu Mwakili ambayo unapita mipaka. Kwa hivyo mwananchi anaweza kwenda mpaka kwa Tume ya haki za wananchi. Tume ya haki ambayo tumeitunga. Uende useme Wakili fulani ameninyaganya haki yangu. Na Tume itakuwa na haki ya kuchukuza jambo hilo na kupendekeza jambo ambalo litakuondolea taabu zako na ikiwa amevunja sheria huyu bwana atachukuliwa hatua au bibi.

Pendekezo kuhusu kipindi cha elimu ya raia kinacho tengenezwa na Tume ya Kurekebisha Katiba. Tumekusikia maoni yako tutajaribu kutimiza haja zako lakini tutakuelezea ya kwamba ni vikumu sana hasa unapo fanya kazi na shirika la ki-taifa. Wana mipango yao, wana vipindi vyao kuondoa vipindi fulani saa fulani itakuwa ni ngumu. Lakini tumejaribu kwa uwezo wetu. Nakumbuka wakati tulikuwa tukifanya saa tatu asubuhi watu wakatwambia saa tatu asubuhi watu wako kwenye ibada tutajaribu kukibadilisha tukashindwa mpaka tukafikia saa sita sasa lakini sasa kitakuwa kikirundiwa saa tisa ili ukiwa ume kosa kile cha asubuhi kwa sababu ya ibada upate cha jioni. Ukikosa cha jioni upate ya asubuhi lakini haina maana ya kwamba hatuwezi kukirundia kipindi. Labda tutajaribu vile tunavyo weza kufanya msikilize.

Kuhusu Judge na anasa. Anasa hizo pia zitakuwa zinachunguzwa. Kutakuwa na Judicial Service Commission itakuwa inachunguza pia anasa hizo na Judge akiwa na karti ya hizo pia atachukuliwa hatua.

Halafu mzee…… kuhusu copral punishement na death peanulty tumesikia maoni yako na ya Wakenya wengine ambayo walikuwa wanasema pia let us abolish death peanulty and do not abolishi copral punishement but the majority of those who contributed in these issues walisema kwa ajili Mwenyezi Mungu ndiyo ametoa uhai usinyaganyi mtu uhai wake wengi walisema hivo. Lakini tumesikia maoni yako na uwambiye wale washiriki wa wilaya wanakwenda katika mkutano wa kitaifa wanaweza kupeleka maoni ya aina hiyo.

Timothy kuhusu … of election. Jambo hili tuliliangalia kwa maakini sana… lakini tukapata tatizo moja kwamba ikiwa tutakuwa na haki na Bunge kupiga kura kutokuwa na imani na Waziri Mkuu halafu Waziri huyo akiondolewa haina maana kuwa na uchagunzi. Rais atakuwa na nafasi tatu sa kujaribu tena kupata mtu ambaye watu watakayo mu-support wengi katika Bunge. Lakini katika njia hizo mara tatu akijaribu akishindwa itakuwa haina bundi isipokuwa watu waende kwa uchagunzi. Kwa hivo ikiwa Bunge halitavunjika tarehe yake itajulikana. From the date iliwekwa mpaka Serikali iwe from the day siku yake itaisha. Huenda likavunjwa only ikiwa Waziri Mkuu hana support ya wa Bunge katika Bunge na pia Rais atashindwa kutafuta mtu mwingine katika Bunge apawe atapata support hiyo ya Wabunge.

Halafu kitu kingine pengine niligusia kuhusu jambo hilo sababu ingine ya kuwa na kundi mbili za Bunge. Kumekuwa na…Katiba ya kisheria Kenya kwamba katika muda fulani wakati kura zinapo pigwa ama Bunge linapovunjwa kuwa nchi yetu hakuna tasisi ambayo inaweza kutengeneza sheria na ni jambo lakutisha hii iwapo kutatokea vita wakati wowote kutafanyika nini? Kwa hivyo sasa imetengwa hakuna wakati kutapokuwa hakuna tasisi ya kutengeneza sheria.

Miaka ya wabunge ya wakilishi katika Bunge la chini Lower House ni miaka mitano. Ya juu ni miaka minne tulifanya hivo kusudi ndiyo wakati wowote kutakwako na tasisi ya kufanya sheria katika nchi.

Halafu lingine ni la Victoria. Pendekezo lako pia linafaa kwanda katika mkutano wa kitaifa lakini juu ya hayo Bunge linaweza kuwa na haki ya kuongeza siku zingine lakini siku hizi ndizo tulipewa na wanakenya wasiweke siku zao.

Elijah amezungumza mambo yake. Nadhani Bwana Elijah kwanza Wakenya wengine walituambia kwamba wanataka haki ya kutekeleza mambo yao ya na walimu mambo hayo ni ya Seikali ya wilaya. Mimi sitaamua mambo hayo nyinyi wenyewe mta jiamulia mambo yenu. Kijiji kama kijiji mtajiamuria kijiji chenyo munataka kufanya mambo haya vipi lakini tumesema hivi kwamba ukishikwa na Police una haki ya kupewa police bure ukiwa uhatarishi maisha ya watu wengine. Una haki hiyo. Na ukipelekwa mahakamani. Watu wengi walikuja kwetu wakatuambia hayo makosa madogo madogo maaana Katiba mnaweka vitu makosa madogo mengine yafaa kuondolewa kabisa na mengine ikiwa utasitakiwa uwe unapata huduma za mahakama mpaka kesi itakapo isha.

Wengine wanakubali mashtaka sio kwamba umefanya makosa ni ile vurugo ya kuambia kwamba utawekwa ndani mpaka kesi itakapo zikilizwa nidyo ina wasumbua. Tumesema kwamba … ile….. ikiwa umeshtakiwa kwa jambo ambalo halina suruhisho ama utafungwa zaidi ya miezi sita au mahakama ikupe bondi.

Halafu Harman anazungumzia lease ya ardhi anasema iwe ni miaka moja nadhani hiyo itakuwa pia ni kuwaonea hawa watu sababu uwanyaganye ardhi apawo ilikuwa ni free hold usha sema Wakenya ndiyo watakuwa wanamiliki ardhi. Tuwanyaganyi kutoka free hold tufanyi lease kwa mwaka moja.

Bwana Michael anauliza je huyu mtu amabye hakuwa Mkenya akioa Mkenya atapata Ukenya kwa sababu ya ndoa hiyo watakapo achana nini itakayo tokea. Hakuna litakalo tokea hasa kuwa Mkenya. Ukisha mpa Ukenya, kisha mwataka kumnyaganya tena maanake wale watakao kuwa wakivunga ndoa na wageni lazima wa pime na kuwafikiri kwa muda mrefu kabla hawajafunga ndoa. Au sio hivyo lakini ukisha mpa hiyo amekuwa Mkenya na hivyo hutamunyaganya.

**Interjection**: Comments.

**Abubakar Zein Abubakar:** Anasema ikiwa utamnyaganya uraia kwa sababu hiyo basi atao mwingine. Mzee Onesmas kuhusu yatima ni fikira nzuri lakini tulisema kwa sababu ya hali yetu ya kuichumi tuazi na nini? Na elimu ya msingi. Lakini Serikali kuanzia chini inaweza kufanya mambo kama haya maanake Serikali ya Wilaya pia inasimamia elimu. Kwa hivyo mtajiamria wenyewe hapa. Mtasidia watu walio yatima au hamutawasaidia.

Wazo la Bwana Godfrey, mambo ya wilaya yameandikwa kabisa clearly na usome the relevant chapters za devolution pamoja na provisions zinazo wekwa kwenye schedule. Tumeweka wazi wazi tusilete tofauti wazi wazi Serikali ya taifa inamajukumu gani? Na Serikali za wilaya na Serikali zingine na moja haiwezi kuingilia ingeni na ikiwa kuna tofauti karti ya Serikali ya Taifa na Wilaya either Serikali ya Taifa au ya Wilaya ina haki ya kupeleka jambo hili moja kwa moja mpaka Supreme Court iamue katika tatizo hilo.

Halafu Bwana Mohamed kuhusu ignorance, mnajua ya kwamba tumetengeneza Tume ya Katiba katika mswada huu. Tume hiyo ya Katiba haitakuwa tu, na mamulaka auo jukumu la ku-implement Katiba lakini itakuwa na haki ya kueneza habari ya Katiba na ukiangalia pale tukizungumzia majukum ya raia tunasema jukumu ya raia moja ni kwamba unajua Katiba yako. Na Katiba itafunzwa shuleni. Eh tuko pamoja? Lakini mtu hawezi kujicha mwingine akasema ati mimi sijui kujicha mtu ni vibaya kwa hivyo unisamehe. La wazekana hivo.

Mzee wa National Parks ni mejibu na mahakama nimejibu sijui kama kuna swali limebaki.

**Interjection:** Liko.

**Com. Abubakar Zein Abubakar**: Kwa vile mama hujauliza lako. Tuaze na lake la mama nadhani hataudhika kuheshimu mama kwa umri wake aulenze swali halafu tuendelee na nyinyi mulio panga line.

**Speaker**: Nashukuru sana kusikia maneno matamu. Jina langu ni (Inaudible … mimi nauliza sisi hapa Voi tumekuwa masikini wa mashamba hakuna pahali pa kulima. Mboga, matunda tunapata kutoka nje zamani sisi tulikuwa na mashamba mimi mwenyewe ni mzaliwa wa hapa. (Inaudible …Mashamba yetu yalikuwa huko chini ndiko kunacho kuzwa mbego. Huko chini. Tukaja tunganyaganwa kabisa haya mashamba na mzungu. Mzungu alipo enda tena tukarundi tukapokonywa na mwenye nguvu

akachukua kwa kifua. Sasa sisi hatuna mashamba hatulimi twaishi kwa maduka. Sina mahala pa kwenda. Yale mashamba yetu tungerundishiwa aje?

**Fatuma Hezra**: Majina ni Hezra kutoka… Swali langu ni kama katika draft ya leo kuna kipengele mliki sahau. Kitengele hicho kinahusiana mambo ya Councils wards juu ya watakao gombea hizo viti kwa sababu… nasisi tulikuwa tumependekza katika draft ama katika maoni wakati wa kutoa maoni kwamba viti vya Town Council, ata za Urban vigombewe na wazaliwa wa pale ampabo jambo hili lilisahauliwa sijui ni utaalamu gani nyinyi muliutumia labda utatueleza tukaweza kujua ni utalamu gani muliutumia.

Halafu sijui ni umilikaji wa ardhi. Nafikiri desturi ya Mtaita si mtu wakutanga tanga na ninafikiri wakati wa kutoa maono ama katika draft ambayo umetupatia sijaipitea sana ni kwamba popote mwananchi anaweza ishi ama anaweza kaa kama Mkenya lakini kwa desturi ya Wataita kama ni wa Voi utamakuta amekaa Voi hutamkuta amenda Undanyi atakaa hapa hapa. Lakini kunao watu wanatoka labda Mombasa. Mombasa ako na shambo liko na Title Deed. Ukienda Kilifi vile vile, anakuja hapa Taita kwa sababu hayajalazwa akija twamkarebisha mwingine na mwingine anakuwa ni mkuaje. Kule aliko toka Mombasa anakodesha shamba kwa sababu sheria inasema una weza ishi pahali popote. Sasa tungependa kwa upande wa land sale na ownership muweke vipengele vinafo eleza umilikaji wa ardhai kuhusu mtu anaruhusiwa kuwa na mashamba mangapi? Ndi posa tunakuta labda kule anakodisha shamba na huko kwa sababu tuko under zones hakuna njia yote ya kupata mapato wengi walisha grab. Hakuna ardhi ya kulisha kwa sababu tumekaribisha watu na kusema kila Mkenya aweza ishi pahali popote. Kwa hivo tungependa kuwa hiyo kitu ya ardhi ipelelezwe katika draft Constitution. Asante.

**Jefferson Kanyi Mwakiji:** Majina yangu ninaitwa Jefferson Kanyi Mwakichi. Na nashukuru sana Ma-commissioners wa hii Committee ya Constitution.

Jambo ambalo mimi nilikuwa nitaka kupendekeza ni hili. Taifa letu hili la Kenya, ni Taifa tunalotaka liwe moja. Na Taifa hili la Kenya kwa upande wa vyama vya kisiasa, tunataka vyama vya kisiasa visiwe vya Kikabila, na viwe katika Draft ya Constituion. Mimi ninapendekeza kivyangu, nasema ya kwamba ile committee ya Constitution iweke limit ya vyama. Kama ni vitatu viwe passed, siyo tu vyama vingi vya ukabila . Mapendekezo yangu ni kama hayo.

**Salim Husein Mwamkanga:** Asanteni wageni wetu. Mimi kwa jina ninaitwa Salim Husein Mwamkanga, mkombozi wa Taita Taveta District. Mimi kile naomba, Katiba hii ya sasa iwe na imani na wananchi. Isiwe kama ile katiba ya sasa. Nikisema hivyo ninamaanisha watu tulipatiwa makao huko porini, na baadala ya kutupatia makao mtu porini, ni kwanza utangulize maji kliniki ndio uai wa mwanadamu. Lakini sisi wajua maji hakuna Naomba Katiba hii mpya kabla haijaamisha watu kutoka town kwenda porini, waweke hivyo vitu tayari, wananchi wakute maji, Kliniki ndio uhai wa wananchi. Asanteni.

**Speaker**: Bwana Commissioner na wananchi Bwana asifiwe.

**Audience**: Amina.

**Mwalunda:** Mnisamehe nilichelewa kwa ajili ya shughuli na uenda nikauliza maswali ambayo yameulizwa ndungu yangu utanisamehe. La kwanza nimeudhika sana na ile sehemu ya dual citizenship. Kama mwananchi, naogopa ogopa mtu kuwa na citizenship mara mbili, hawezi kuhatarisha maisha yetu maana anaweza kukaa huko kumbe anakaa hapa akiwa na madhumuni fulani. Sasa hiyo inanitia wasiwasi hiyo dual citizenship ukitueleza itatusaidia sana.

Na hiyo sehemu ya kubadilisha ya kusema kwamba, ukibadilisha chama wakati umekuwa Bunge, halafu unapoteza. Ninaona kama kwamba unakongana na ule uhuru wa kuendelea ku-associate. Ninaona kama mtu huyu akaona kwamba njia moja ya ku-express shida ambazo simepatika na chama chake ni kuwajisha kazi ili kusema kitu. Sasa kama punishment itakuwa kuwa namna hiyo, uenda uhuru wa kuwasilisha mambo ukawa curtailed, sasa pengine hilo tunaweza kusaidiana.

Kama kiongozi wa dini, basi pengine hivi ni either umesema mengine ni local Government na kadhalika. Nashukuru kwamba, kuna uhuru wa kuabudu na makasema pale kwamba kila region ni sawa. Niliuliza wenzangu hapo, tayari niulize ile ya devil worship, nikaambiwa ulitaja mapema kwamba haiwezekani. Lakini kuna zingine ambazo, sinafuatana fuatana, kwa mfano kuna shida na ile Muingiki na mambo kama hayo. Wengine wanasema kwamba ni region. Sasa tuseme kama ikiwa hivyo kutakuwa namna gani?

Na pia mimi kama mhubiri, huenda nikajaribu kueneza injili yangu na mwenzangu next door huenda ana mtoto huenda shule anataka kusoma na mimi neighbour hapo napiga ngoma usiku mchana na kadhalika, hiyo si appreiation, tunaweza ku-practise namna gani ili uhuru uweko na tena zile haki za binafusi sitimiliki. Yaani yule ambaye ana excercise awe ana furaha yake yakufurahia ijili yake na haki yake, lakini huyu ambaye anasikia kwamba pengine nina hubili hapa na ninataka wageni wapumusika, nina mtoto wa shule anataka kusoma, how do you deal with that ili kila mtu yeyote apate haki yake katika mambo kama hayo. Asante ndugu yangu nisamehe kama nimerudia lolote. Naitwa Malunda.

**Speaker;** Swali langu nimerudi tena, kama vile Bwana Commissioner umetueleza kuhusiana na Draft hii ya Katiba, kwamba lengo na madhumuni na msingi, ni iwe na National out look, yaani ambayo imekusanya mahadili,mipango inayousisha kila mwananchi wa Kenya kama Mkenya. Nasikitika kwamba, kwa ufahamu wangu, sijui ni wangu pekee lakini kwa ufahamu wangu ni kwamba Katiba yetu inataka kuondoa ukabila ule ambayo toko nayo leo, draft. Hapo nyuma tukisoma wakati wetu ambao tulisoma ile system ya zamani, ni kwamba system ile ilikuweko imeondoa ukabila.

Na mimi nina imani sana, ukabila umeingia ndani ya nchi ya Kenya hivi sasa umeletwa na the current Education Sytem ya 8-4-4. Sasa sijui kuna provision gani katika draft hii ya education kwa sababu sikuli siku hizi unakuta kwa mfano, Kenyatta High School Mwatate, wanaosoma pale watakuweko 80% ni Wataita, kwa hivyo hawana hata nafasi ya ku-interact na any other

tribe ya kutoka nje ya province. Ikiwa ni provincial schools mwisho wake ni Mombasa, Kwale or Coast Province.

Wakati wa zamani, when we were in those schools, ulikuta interaction yetu, tunakia na Wakisii, Wasomali, Waturukana, Wanandi na Wakikuyu. Kwa hivyo mimi ninaona kwa upande wangu, education system ime-propergate tribelisim in Kenya. Zifunguliwe kuwe hakuna story ya Provincial schools, Nationa Schools sifunguliwe kila kabila ama kila Province mtoto wanaoweza kuja a-apply. Akiwa kisumu apply school in Lamu. Bora ni matokeo yake ndiyo ya itamwingiza katika shule ile. Lakini inaonyesha kwa system tulioko nayo, Kuna descrimination na segragation. Kwa hivyo mtu saa ingine anaenda kupata elimu mahali ambapo hajaridhika. Kuna mtu hamu yake ni kwenda Nairobi University. Kwa hivyo asante kwa hayo.

Mambo ya hosipitali mimi ninaona …(inudible)

**Aisha Kaddho Makomba:** Commissioners na wezangu, asalam alekum

**Audience**: Aleku msalam

**Aisha Kadho Makomba:** Mimi kwa majina na Aisha Kadho Makomba. Mimi yangu ni kwa Bwana Commissioner kifungo kile ilichokisoma cha Kadhi, kama mama wa kislamu, yangu sijui itakuwa ni maoni maanake siwezi kusema labda ni swali. Kwa sababu kifungu hicho kama ulivyosema ofisi hii ya kweli ina nguvu lakini upande mwingine twasema ni kama nguvu zake kidogo tungependa siongoswe simekaza kidogo. Sababu mama huyu ama inapokuwa order imetoka haifalizwi na kadhi, inakuwa sasa inarudi kortini mama yule anayumbishwe yumbiswhe kiasi kwamba kama ilikuwa ni masilahi ya hawa watoto nyuma wanaendelea kuteseka. Sasa hapo mimi ningalipenda hicho kifungu ama hiyo ofisi kulingana na Katiba ya sasa iongezwe nguvu kumsaidia huyu mama wa kislamu. Anapata taabu kwa kweli. Akipata yeye pia hawa watoto wanapata taabu. Tumeona na tumeshukuru kuwa katika nafasi hii ili kusudi tusaidie akina mama wa wakislamu.

**Speaker:** Bwana Commissioner, kuna swali ambalo linakera watu, hivi juzi tulisikia mtu mkubwa sana muheshimiwa akisema kwamba hii Provincial Admsinistration ikiondoka kutakuwa na anarchy kutakuwa na hali ambayo hawezi kuendeshwa vizuri, na hakutakuwa na amani. Sasa hiyo hata mimi mwenye sielewi. Lakini kitu kingine kinacholkera watu ni wale Provincial Administration watakao futua kazi, au watakao ondoka wataenda wapi? Hilo ndilo swali, asante.

**Cosma Nyamu**: Bwana Commissioner, mimi kwa majina ni Cosmas Nyamu, nangependa ku-react kwa jambo ambalo nilisoma katika hii Draft ambayo tumeiona, kuhusu protection ya Rais akiwa katika uongozi. Nili-note kwamba, inasema kwamba Rais akiwa katika Uongozi, hakuna shtaka ambalo linaweza kuwakilishwa juu yake. Hata kama lilikuwa noticed haliwezi kuakilishwa. Sasa hatuelezi alternative ya hilo kosa,na hilo kama ni kosa ambalo limeonekana, litawakilishwa wakati gani.

Halafu swali lingine ambalo ningeuliza ni kuhusu hii nafasi ya tajiri na masikini. Kwa kipindi hiki tunaona kwamba kuna tofauti kubwa sana. Tunavyosikia per month kuna mtu ambaye ana-earn more than four hundred thousand na katika nchi yetu pia kuna mwingine ambayo ana earn less than two thousand. Sasa hiyo kitu inaendelea mpaka inakuwa pengo kati ya tajiri na masikini ni kubwa mno, kiasi ya kwamba hatuelewi.

Lingine la mwisho, ni kuhusu mtu akishitakiwa akiwa na kosa, kuhusu kuchochewa. Tunaona kwamba mtu ambaye hana uwezo akifanya kosa, hana uwezo wa ku-hire a lawyer. Lakini yule mwenye uwezo ana-hire lawyer. Sasa unakuta ya kwamba huyu kwa sababu ako na lawyer, chances zake za ku-win hata kama ako na haki ni kidogo sana. Sasa katika Katiba yetu, ni huyu mtu atatetewa kivipi? Yangu ni hayo.

**Gabriel Mwachie Mganga:** Asante sana Bwana Commissioner na viongozi wenzangu. Kwa majina ninaitwa Gasbriel Mwachie Mganga. Swali langu linahusu zile harassment ambayo watu hufanyiwa wakati wanapokunywa pombe ya kienyeji. Wanaambiwa kwamba iko illicit. Na yenyewe kuitwa illicit ni kwa sababu ilitokana from an African Technology. Lakini hii beer kwa sababu imetoka from a white technology inaitwa legal. Na utaona watu wakigandamiswa sana katika hiyo hali. Na kati ya hizo pombezote mbili hakuna ambayo imehalalishwa na ndani ya Korani tukufu ama ndani ya Bibilia. Kwa nini ingine sasa inaitwa illicit?

Swali la pili ni kuhusu haki za watoto. Tulienda katika seminar ya haki za watoto tukaambiwa kwamba mtoto anayezaliwa nje ya ndoa inaitwa mtoto wa mama. Mara nyingi tunapoona, sheria ikipitishwa hivyo, utaona hali ya uchumi katika ile nyumba mtoto amezaliwa inazidi kuharibika kwa sababu majukumu ya kulea yule mtoto itawajiwa mazazi mmoja. Mbeleni kulikuwa na ile iliyokuwa inaitwa ……..Act. Tungaliona kwamba kama hii ingarundishwa haki ya mtoto ingalipatikana zaidi kuliko vile ilivyoko.

Halafu, swali langu la tatu na la mwisho ni kuhusu haki za akina mama. Mara nyingi katika traditions, utaona huyo mama aliyezaa musichana, amafikia wakati wa kuolewa, na anapo fikia wakati wa kuolewa huo mama hausishwi kakika kushudia matumizi ya mahari. Inakuwa ni jukumu la baba. Baba yule naye baadala ya kuaangalia kwamba huyu mama ndiye alibeba mimba na akamulea huyu mtoto mpaka amekuja kuolewa, sasa ndiyo huyu mtoto anatolewa mahari, yule mzee anachukua pesa na anaenda kuongeza bibi wa pili. Kwa hivyo ningalipenda mfahamu akina mama. Hayo ni yangu yamekwisha. Asante.

**Juma Shapan Nyau:** Okay, asante sana kwa majina niaitwa Juma Shapan Nyau kutoka ofisi ya Serikali, nigalitaka kujua kwa ukweli yaani, haswa kwa mababu zetu yale mashamba ambayo wamenyanganywa na wale waliokuwa wakitutakia mkuu na wakati huu wamiliki, jee Katiba hii ambayo tunaendelea nayo wakati itakapokuwa imekamilika na inatumika, tutaweza kuwa itaturuhusu sisi kusimamia na kutetea mashamba yetu yote yaliyo chukuliwa na tukarudishiwa wenyewe. Swali langu ndilo hilo.

**James Nyale:** Mimi kwa majina ni James Nyale, swali langu nilikuwa nataka kuuliza kwa sababu Kenya hii tangu nizaliwe na

Mwenyezi Mungu wakati tunapata uhuru, tulikuwa watu elfu saba, na tangu wakati huu, na saa tuko zaidi ya mililion thelathini. Sasa vile nilikuwa ninazungumzia kuhusu habari ya poverty, nilikuwa ninataka kusema hivi, katika hii Katiba yetu ambayo ni mpya, ingawaje Serikali Katiba ya zamani ilikuwa infanya mambo ya family planning na nini na nini. Lakini bado haikuweza kufaulu, je kuna sheria yeyote pengine hapo imewekwa ili kuzuia watu wasizaane kwa wingi? Kwa hivyo hiyo ndiyo inaleta umasikini, kwa sababu mtu moja anaweza kuwa amezaa watoto ishirini na wengine kumi. Sasa utakuta kwamba umasikini unazidi kwa sababu hakuna sheria zozote ambazo simewekwa. Mimi sina kazi na ninazaa tu kwa hivyo je katika ile katiba, kuna mahali ambapo tunaweza kukawa na sheria ya kusema kwamb Wanakenya kuwa na watoto watano, na ikifika hapo ukome ili uzidishe masikini. Asante sana.

**Com. Abubakar Zein Abubakar**: Asante sana. Ngoga ngoja… Tulisema hakuna mtu atakayepikwa kwa maoni yake. Aaa mzee wangu apana. Hata kama atapotoka haki yake anayo.

Kwanza kabisa ningapenda kusema hivi, kwa sababu tunaanza kuuliza maswali ya mambo ambayo nilikuwa nimeshazungumzia, inamaana kuna watu wamechelewa. Isipokuwa zile za Bishop ambaye ametueleza kwamba pengine nitauliza jambo ambalo pengine mshataja, wengine pia wamegusa mambo amabyo nishataja. La Patrick nilimaliza . Tuanze na Fatuma. Mama fatuma nilikuwa nimesema kwamba kulingana na mapendekezo ya Katiba Mpya, tumetaja mikoa mitatu na tukasema pengine baadaya mikoa hii mitatu kuna sehemu zingine, ambazo kutokana na Historia wamenyanganywa haki zao za aridhi. Na tumetaja pwani kama mkoa moja, kwa sababu ya maoni hayo mlitoa kuhusu watu na aridhi yao. Na tukasema Katiba hii ikianza kutumika, Serikali inalasimika kuweka njia ya kufanya ujunguzi kuhusu madai haya ya Kihistoria na madai haya pengine ya kuonewa ili, haku ifanyike na kuweko na amaani katika kufanyika haki hiyo na usawa. Kwa hivyo tumetia kwenye Katiba njia ya kutatua tatizo lako.

**Interjectio: Fatuma :** Kuanzia kwa Chief, nikafungiwa waya.

**Com. Abubakar Zein Abubakar:** Hayo yamekwisha, tumeshasikia mama, na tumeweka njia ambayo itatumika uende mahali njia hiyo ili hali haki ijulikane iko wapi. Bwa Esira mambo kuhusu mambo yako ya aridhi pia yanahusiana na ya mama Fatuma. Kwa hivyo sehemu ya swali lako litajibika hivyo. Lakini sehemu nyingine unapozunguza kuhusu malisho, sijui hukukuweko kutoka mwanzo niliposema kwamba tumegawanya ardhi katika sehemu za umilikiji wa aina tatu. Unamiliki aridhi kama mtu binafusi kuna kumiliki aridhi kwa umma na kuna umaa jamii, yaani the commons. The Commons uyatekelezayo, it is the pieces of land which is used by the community or a group of people. Ikiwa ni kwa malisho au kwa njia fulani. Na tutatunga sheria, tumeseme Bunge lazima litunge sheria katika kufahamu watu wa sehemu hizo zote tatu. So this issue will have its own Act of Parliament. Lakini ni mhimu kufahamu kwamba si kila jambo tunaweza kuliweka katika katiba, tunaweka Katiba nguzo, msingi wa mahadili na njia. Halafu sheria sitatungwa ili kutekeleza mambo haya.

Vyama visiwe vya kikabila nindhani nilikuwa nimezungumzia hilo, sijui ambalo hatukuzungumzia kuhusu vyama, ni kwamba,

wajui tumeweka very tough conditions for registration. Kutakuwa si vyama vingi ambavyo vitafuka mipaka ya kuregister. Halafu, tumesema kwamba vyama vitapewa pesa na umma kupitia Serikali. Kulingana na kura wanazopata katika uchaguzi. Chama chochote kitakacho pata asili mia tano ya kura za inchi nzima wanaweza kuepwa pesa kulingana na asilimiazao. Ukipata chini ya hapo hupati chochote. Bwana Kare ndilo swali lako hilo.

Bwana Hussein, watu wasihamishwe kabla ya kupewa huduma, nadhani mambo hayo yatatatuliwa katika kiwango cha Serikali ya wilaya. Mtajiamuliwa wenyewe mnataka kufanya vipi mambo yenu. Msitoke Kenya baada ya kudai kwamba mnataka kupewe haki za Serikali ya Wilaya, halafu msema tena taifa iamue. Haiwezi kutiawa kwenye Katiba namna hivyo. Kuhusu maswali yako matatu, dual citizenship, kwanza hiyo mambo ya dual citizenship, kutatungwa sheria ya Bunge itakayo isimamia mambo ya dual citizenship. Na mtu ambaye anaruhusiwa kuwa dual citizen, ni Mkenya kwanza, sijui kama mnanielewa, kwanza uwe mkenya halafu ndio utaruhusiwa kuwa mwananchi wa nchi ingine. Sijui kama unanielewa. Si kwamba wewe ni mmarikani halafu uwe Mkenya, Sijui kama tunaelewana, halafu nilisema kwamba nilipoanza hakuna ofisi tunayoiweka bila kuiwekea mipaka. Hakuna haki tuliyotoa bila kuiwekea mipaka bila uwahajibikaji. So, kumetengwa mipaka ili koti kama uliyo nayo wewe isije ikatumiwa vibaya kama pengo la kuleta nchi ikaangamia au watu ambao hawafai nchi ingine wakimbilie Kenya. Tunafahamu hayo na yako katika uongozi.

Halafu kuhusu defection of an MP, swali lako lingekuwa nzuri ikiwa hatukumpa mtu haki ya kusisima kama independent person Katika Katiba mpya mapendekezo yanasema somebody has a right to run as an independent person. Utaki kuingiliwa na chama chochote, run as an independent candidate. Ukiingia Bunge wewe you are independent. Lakini ukitumia mamlaka ya chama kusimama, hiyo chama tu kinawajibu kwako, lakini siyo wewe tu una wajibu kwa chama. Siju kama linafahamika hilo?

Kuhusu religious rights, juu nilikuwa ninajibu wanaosema kila rights ina obligation, lina jukumu na ina mipaka. Na some of this rights tumesema kwmba ikiwa kuna sababu za kutosha sinaweza kupunguzwa au ikazuiwa, ikiwa mtu anatumia vibaya haki hiyo, na kutatumika na sheria ambayo itaundwa kusimamia mambo hayo. Wakenya wengi wametwambia kusajili dini na mashirika ya kidini lazima waangaliwe kwa uangalifu, ili isipite mipaka. Kwa hivyo ombi lako litatiliwa maanani katika njia hizo.

Elimu na kuhusu National Intergrity, ikiwa tumeipa District haki ya kusimamia elimu mpaka Secondary, lazima nyinyi mujukue majukumu kama District kuhusu sera za elimu Sijui kama mnanielewa. Mnanielewa, mkipewa mamlaka myatumie vizuri.

Bi Esther kuhusu nguvu za kazi. Tafadhali uende usome sana kitengo hicho kinacho husu nguvu za kazi. Tuzungumze juu ya vyama vingi kabla sijaondoka. Nime ongezewa nguvu na wanawake waliokuwa wakisema ya kwamba wanapata matatizo ikiwa bwana yake amekufa. Angalia nguvu zilizo ongezwa uone kama sina faa ama hasifaye.

Halafu bwana Nyambo anauliza kuhusu kuleta vujo sidhani ningependa kuzungumzia sana kuhusu mambo haya ya fujo. Lakini

ukiangalia the transition mechanism sera za mvito na mambo tuliotoa kuhusu mvito transition eh… yanazungumzia haya mambo kwa uwangalifu na ubali zaidi.

Kuhusu Provincial Administration. Mwalimu wangu ningependa kukueleza hivi, kila pahali tulipo enda walisema …

**Com. Abubakar Zein Abubakar:** Msiweke kwa mambo yaliyotendeka kwa mambo yaliyo tendeka kabla ya sheria hiyo haijatungwa. Huo ni msingi mmoja ntunao tunao tumia hapa, lakini twasema hivi, ikiwa Rais atakosa, kuwe na njia ya kumuadhibu. Sijui kama mtanielewa, kuna njia za kmtoa Raisi kama kama amefanya makosa, Hapo akishatolewa sheria itafanya kazi yake.

Halafu tofauto kati ya matajiri na Makini. Na kitu kingingine ambacho ningefurahi kuwaambia ni swala ambalo lingefurahisha nyinyi ni kwamba tumeunda Tume ya mishahara ya Kenya. Tume hii itakuwa na kazi ya kilinganisha na kuweka mishahara na maruburubu yanayolipwa wafanya kazi wote wa umma. Kutokea kwa Rais mpaka kwa mfakiaji, kwa kuweka kwa viwango. Ndio kusiwe kuna tofauti hizo kubwa na nyinyi wenyewe mmetwambia hamtaki wabunge wajiwekee mishahara, Wabunge hawana tena kazxi hiyo ya kujiwekea mishara. Tume hii huru ya kuweka mishahara ndio itakayo angalia mambo hayo ya Wafanyi kazi wa umma wote.

Halafu nauliza je, nadhani pia Bwana Kijana huyu Nyambo alikuwa amekuja amechelewa kwa sababu nilizungumza kuhusu office ya public defender, hiyo nilizungumza?

**Aundience:** Ndiyo

**Com. Abubakar Zein Abubakar:** Kwa sababu tumeweka Public prosecutor na kutakuwa pia na Public Defender. Huyu public defender ndiye atakuwa na kazi ya kulinda haki za Wakenya, ikiwa una mashitaka magumu unaweza kwenda kwake upate usaidizi na tumesema kwamba huwesi kushitakiwa kwa kosa kubwa ambalo linaweza kufanya wewe ukafungwe maisha bila kupewa wakili wenye kutumia pesa za Serikali.

Halafu kuna swali la Gabriel kuhuzu traditional beer, sijui hamnisikizi nyinyi, si nilijibu swali la huyu ndungu yangu hapa kuhuzu mambo hayo?

**Audience:** Ndiyo

**Com. Abubakar Zein Abubakar**: Na si kitambo sana? Nilijibu tena?

**Audience**: No

**Com. Abubakar Zein Abubakar:** Basi ndugu yangu Gabriel mshike huyu ndungu mwingine. Haki za watoto na haki za wanawake, nasema ndugu yangu ukifungua chapter five, hilo swali uliuliza wewe Gengo, namba thelathini na saba, sehemu ya nne inasema, la child's mother and father whether married to each other or not, have an equal duty to protect and provide for the child. Nishajibu?

**Aundince**: Ndio.

**Com. Abubakar Zein Abubakar:** Kuhusu haki za wanawake ningependa angalie sehemu ya wanawake, tumeitaja vizuri. Juma anazungumzia mashamba yaliyo nyanganywa yanarudi kwa ipi? Jibu la mama Fatuma. Halafu Nyefu anazungumzia kuhuzu kuongezeka kwa watu. Ndugu Nyefu, hayo maoni ya namna hiyo ungeyafuata vile tulikuwa tukikusanya maoni kutengeneza Katiba. Wengi wa Wakenya walisema tuwawekea watu limit ya watoto. Lakini kwa mfano Serikali ya Wilaya, muamue kwamba watoto wa secondary watakuwa wakipewa usaidizi fulani wa kufanya masomo yao. Yet, mzazi mwenye watoto mia utampa uzaidizi sawa na mazazi wa watoto wawili? Ni jibu ambalo mtaamua nyinyi wenyewe kama Serikali ya Wilaya. Sababu tutaanza kuzoea ya kwamba tutapewa madaraka na madaraka tunayatumia. Kwa hivyo hilo ndilo lilikuwa swali la mwisho, na ikiwa kuna swali lingine ambalo sikulijibu mtu anaweza kuniambia, au tusianze kufanye line ingine.

Swali lingine labda litakufanya wewe ushindwe kulala, lakini jambo hili, ni hayo mambo mhimu tuliyoanza, huu ni mwanzo wa kujadiliana, na ni muhimu sana tutakapoondoka vile msianze kujadiliana. Ukae chini ujadiline, usome kifungu hati kifungu, haya kwa haya, hili ikifika wakati wa zile siku thelathini kumalisika tuanze mkutano wa kitaifa, mtakuwa mshawaambia waakilishi wenu wanao kwenda katika mkutano wa kitafa kuhuzu mawazo yenu na kila jambo linali jitokeza katika mapendekezo haya. Kama nilivyo sema mwanzo,sisi hatusemi kwamba mapendekezo haya hana dosari. Tunasema kwamba mwenyezi Mungu pekee yake ndiye hana dosari, lakini binadamu anaweza kuwa na ukosefu wa hapa na hapa na mtuonyeshe mahali ambapo tumekosea. Na pia ikiwa kuna mambo ya kuongezea, mtupe tuyaongezee. Mimi ningalipenda kuchukua niaba hii kwa vile sikuona mtu ambaye anasema hawezi kulala kumkabidhi Bishop.

**Speaker:** Twashukuru sana Bwana Commissioner, mpango huu tumekuwa tukiuombea sana. Ndiposa nasimama, lile ambalo pengine linanifanya nikose kulala vizuri, ni kiongozi wa nchi, kusimama na kusema, Katiba inamambo fulani ambayo hayaambatani na hata na msingi yetu ya Kiafrika. Na mimi nimeendelea kusoma kupitia gazeti na ninataka nakala yangu kama iko, mnamuelewa ni kitu gani kinamkera mpaka dismiss hii kitu namna hii, ili nisipate kulala?

**Speaker:** Swali langu ni kuhusu mipaka ya wilaya. Hasa nikiwa mdogo, kama kwa mfano wilaya ya Taita Taveta, mpaka niliojua ulikuwa Makandoni, Mpaka Mtitu Wandei karibu na …………………..(inaudible)

**Joseph Mwamburi:** Mimi nanaitwa Joseph Mwamburi, swali langu ni hili, kuna mababu ambao wanalipikania uhuru, mbona

katika Katiba hii, mababu walio pikania uhuru hawaja jaliwa ama kufikiriwa?

**Com. Abubakar Zein Abubakar:** Nadhani jambo la kwanza ningelianza nalo ni swali uliliuliza kuhuzu his Excellence the President of the Republics of Kenya. Nilisema mimi mwanzo kwamba singependa kufanya siasa, lakini ningelipenda kusema hivi, kuna siri, kuna mbaathi yetu sisi Ma-commissioner tusingependa kumkosoa Mweshimiwa Rais, kuna badhi yetu sisi ma-commissioner, tumo mwetu sisi ndani yetu, wanasema waswahili kikulacho?

**Audience:** Kiko nguoni mwako.

**Com. Abubakar Zein Abubakar:** Kuna baadhi yetu Ma-commissioner na singalipenda kusema haya, isipokuwa Bishop ameniuliza, imebidi, nasifunje upendo, ambao hawako na sisi na wala hawako na wakenya. Wako na mabwana zao wanaowapa zenti ili kuharibu mvumo wa kurekebisha Katiba na hawala si siri, sasa wamekuwa wakisema uwongo na unafiki mwingi sana. Kwa mfano kitu, kwa Rais, na wala sitaki kusema maneno yanayomhusu Rais, lakini watu hawa wamekuwa wakizunguka Kenya wakisema, ule mswada unaotayarishwa, unaruhusu wanaumme kuoa wanaumme na wanawake kuoa wanawake. Unaona jambo kama hilo, na jambo kama hilo haliruhusiwi na Katiba hii, lakini waswahili wanasema akuchukiyaye, hakuchaguhii tu, hawatajakua tu hili kisitu si nilijepesi, nilibaya hili nzuri wamejaribu kuchochea wanasiasa ili mswada huu ukataliwe,sio kwa sababu ya mambo yaliyomo humo ndani, ili mabwana zao ambao waliwapa fedha kuaribu mvumo huu, wapate walichokuwa wakikitaka,.ambacho ni nini? Kukazaliwa kwa mapendekezo yaliyotolewa. Na uongo wao umemea mzizi kutoka njini mpaka juu kabisa. Na sisi tunatunachowaomba Wakenya ni wasome jamani. Someni jamani, msisikize hii minongono ati tumeona kitu kibaya, ma-lawyer wengine walisema hata kama ni lawyer ambaye anasema kuna kitu kibaya na takimbia mahakamani kusema Wakenya wasuiwe wasizungumzie mahakama. Kwa hivyo wataka nani lawyer? Akitwambia kuna kitu kibaya, mwambie nionyeshe kitu kibaya na mimi nikione kiko wapi hicho kibaya. Ndio kila mtu ajue, siyo?

**Audience:** Ndiyo

**Com. Abubakar Zein Abubakar**: Haya siyo mambo ya siri Bwana. Na hawa naogopa pengine wengine wenu mtaanza kuniuliza jamani, hao wanao waaribia kazi humo humo ndani mtawafanya nini? Kazi hiyo tuwajeni tu, hawajatushida mpaka sasa, wamejearibu wawezavyo kutuaribia kazi na imeshindikana. Na hivi sasa wana taabu kwa sababu gani? Kila wakipewa fedha wakitumwa kufanya jambo halifanyiki, sio?

**Audience:** Ndiyo

**Com. Abubakar Zein Abubakar:** Na kama Bishop alivyo sema wakenya wanaomba kila siku, wewe una nguvu aina gani, itashinda Mungu?

**Audience:** Hapana.

**Com. Abubakar Zein Abubakar:** Sasa taabu yao ni kwamba wanauliswa nyinyi mlisema report haitatoka, mbona imetoka, mlisema watu hawataka kujukua maoni, mbona wamejukua? Umlisema Mswada hautatoka mbona umetoka. Ndiyo maswali matatizo walio nayo. Na sisi tungeomba watu wote akiwemo mweshimiwa Rais, his Excellency the President of this Republic to read this document, and we are not saying that we don't want to critized. Any person who reads it, let them tell us what in the problem they have with any Act that is been proposed. Sijui kama ni sawa hivyo.

**Audience:** Ni sawa

**Com. Abubakar Zein Abubakar:** Mpaka ya wilaya tumesema kwa sababu jambo hilo ni nyeti sana, na Tume yetu hakuzunguka kwa ku-deal na mambo ya mipaka pekee yake, kutaundwa Tume ya ardhi ambayo itakuwa huru kusimamia ardhi, na wila pia mtaunda Tume yenu hapa na pia tutaunda Tume ya kushughulikia mipaka ya wilaya, ya tarafa na mikoa. Ili kila kitu kishughulikiwe vinavyotakikana. Na wapiganiaji uhuru, ukiangalia katika report yetu utaona tumezunguzia kuhuzu wapikaniaji huru. Lakini kama tulivyo sema, si kila jambo linaweza kutiwa ndani ya Katiba. Na wapikaniaji uhuru walioko sasa, ambao wanaishi katika hali mbaya, watakuwa na uwezo wa kuja katika Tume mbali mbali na kudai ridhaa. Sijui kama mnanifahamu?

**Audience**: Ndiyo.

**Com. Abubakar Zein Abubakar:** Na hakiwa ni mzee haki za wazee sinatumika. Ukifika miaka sitini na tano, jukumu la familia yako na Serikali, mambo mawili. Familia yako na Serikali kukuangalia wewe. Mzee asipate taabu akasema mtu mzee kafa njaa. Kama mama Fatuma anasema hata kupata mlo inakuwa ni shida kwa sababu tumenyanganywa mashamba yetu. Ni mzigo wa Serikali. …interjection (Inaudible).
Nafahamu mama ndio nikakujibu

**Mama Fatuma**:…………………….(Inaudible)

**Com.Abubakar Zein Abubakar:** Nafahamu mama ndivyo ninasema hivyo. Ninafahamu ndio nikakutaja, mama anahaki zake. Lakini mimi ningalipenda kwa sababu hakuna maswali mengine, ningalipenda kusema hivi, kwa kumalizia, najua nimekaa mda mrefu, nawashukuru sana kwa kufika hapa, nawashukuru kwa niya zenu nzuri na njema na ninawaomba msije kutuombea. Tutakapokuwa safarini mwetu na katika kupadilisha Katiba.

Na nigaliwaomba pia, sisi sasa kama Tume hakuna tena kura.

**Audience:** Tutawaombea tu.

**Com. Abubakar Zein Abubakar:** Asante mzee wangu, tutakuwa katika mkutano wa Kitaifa lakini mimi sitapika kura, atakayepika kura ni mwakilishi wako katika wilaya. Umwambie untaka mambo gani ayapikie kura. Halafu na zaidi msiwase, msiamke asubuhi kufikiria Katiba imefika wapi, kabla ya kwenda ufikirie Katiba imefika wapi, sawa?

**Audince:** Ndiyo.

**Com. Abubakar Zein Abubakar:** Halafu la mwisho kabisa, mimi siwesi kuwa na maneno ambayo yanaweza kutosha kueleza ukarimu na mapenzi walionionyesha watu wa voi na watu wa Taita kwa jumla. Nina washukuru sana, namshukuru mwenye kiti, namshukuru msaidi Mayor na ningependa kusema hadharani hapa kwamba tukipata furusa ya kwenda moja kwa moja, ni hata desturi, mila na nidhamu inataisishwa tukifika hapa twende tukamsalamie mayor, tumwambie mzee tumefika, tukubalie tuingie hapa kwako. Leo haikufanyika hivyo kwa sababu tulikuwa na matatizo ya kupokea mzigo kutoka Nairobi. Na nimeshamwomba radhi na amekubali lakini ningeomba pia mimi radhi kwa sababu si niya yetu kuwasalalisha viongozi wetu. Tunawaheshimu, na nitakuja nikuone tena mayor, asante sana, na tunawashukuru watu wote waliousika katika kutayarisha mkutano huu na hasa Bi. Mwadime ambaye unipaka mafuta siku zote, ningeomba pia tumpikie makofi yeye. Kama aliseme yule Bwana habari ya mvua, unayo habari Bwana, tuanze na manyunyu…………

**Audience:** Clapping. …………

**Com. Abubakar Zein Abubakar**: Asanteni sana

**Speaker**: Wananchi nafikiri tumefika mwisho wa Mkutano wetu. Tunamshukuru sana Bwana Abubakar…………

**Speaker:** Bwana Commissioner, coordinator wa Taita Taveta District, Askofu na viongozi wote ambao wamefika hapa kusikiza ama kujionea na kuzungumza juu ya draft Constituion, ambayo imechukua mda mrefu kurekebishwa katika nchi hii yetu ya Kenya. Nafikiri langu ni kuwashuru nyinyi nyote ambao mlikuja hapa. Kwa sababu mambo haya yote au kikao hiki cha leo hakingefanyika kama si yale maoni yenu ambayo mlikuja kutoa hapa. Na kitu ambacho ningaliuliza bwana Commissioner ni kwamba, yale yote ambayo yamezungumzwa hapa kama kuna mageuzi yeyote, yafanyike bila masharti yoyote, kama kuna katika hii Constituion. Na twakutakia heri Bwana Abubakar Commissioner wetu najua kesho utakwenda Taveta, na twazidi kukuombea Mungu na Baba askofu atakuombea, kama kwa kawaida yeye huwa anawaweka mbele ya mwenyezi Mweyezi Mungu kila wakati. Kwa hivyo, nakutakia heri na Commission hii tunazidi kuiombea na tunapenda kazi yenu. Kwa hayo machache, wale ambao wako hapa, mnapokwenda nyumbani, mwende salama na msichoke, uketi na kuzungumzia pahali unaona kuna hitilafu au kuna shida ya kusahihisha,vile vile mambo haya yazungumzwe katika Commission ili yarekebishwe. Asanteni kwa hayo machache.

**Speaker:** Wananchi na bwana Commissioner tunakushukuru sana kwa hotuba ndefu na mwelekeo mzuri ambao umefundisha. Katika hii draft, umetueleza mambo mengi ambayo sisi tuliyatoa vile mlikuwa mnaenda round katika nchi yote. Thank you very much. Na pia ningetaka kusema kama nilivyosema mbeleni, kwamba Katiba ile ya kwanza, ya majimbo iliundwa kimya kimya bila wananchi kujua. Tusipokuwa na cho chochote……… tukifunga macho yetu hii nayo yanafutwa kivingine na watu hawatumii democracy. Mimi ninashangaa Katika hii draft ambayo wakenya wote wanaipenda na wameisoma. Inasemakena ati ni Katiba ya Ulaya. Hayo mambo tumeyasoma katika magazeti, na yamesemwa na watu wakubwa, hata hatuwezi kuwafikia, hata kidogo. Sasa ni wajibu wetu WaKenya, sisi Wakenya kuna watu ambao wanapenda nchi yetu kabisa. Viongozi wetu wanapenda nchi hii lakini, kuna viongozi wengine, mimi………….the draft. Ninaandika na kijana mmoja tulikuwa pamoja, akaniambia hii Bwana …….uko kwenu mmeanza mahezo wa golf, huku kwenu tunasikia na tunaona mchezo wa golf unafanywa huko, aaa nimeshangaa, sisi Wakenya hatuna haki. Tunachekwa na watu wa nje. Na sasa jameni tujue kuna watu ambao wako tayari uongoza nchi hii kwa moyo wao wote.

Nakumbuka Bwana Bishop siku moja hapa tukifungua mkutano, alisema, Katiba hii mpya ni ya kutibu magonjwa ya Kenya. Na ndivyo tunavyo amini hivyo, likini leo tunaambiwa Katiba hii ni ya Wingereza, ya ulaya. Sasa tuwe macho ndugu zangu. Sisi Wakenya tusiwe watu wa kuchekwa chekwa. Tuna akili ya kufikiria, kwa hivyo tutakuwa na mikutano ya kwenda katika tarafa, kueneza ijili ya hii draft. Tunaomba mtoke kwa wingi. Tuzungumze na hawa wajumbe wetu watatu, tukiwapata, tuwapatie mambo yote yaloyotoka katika mjadala wetu. Tunataka uhuru kamili, siyo mambo tunayoyaona siku hizi. Hasa hii ni election ya mwaka huu. Tunaona mambo ambayo ni kama watu hawajui democracy democrazy ile ya zamani, imepitwa na wakati, democrazy sisi tumefundishwa na waingizereza ni ile ni self-explanatory. Leo tunaambiwa ndio huyo huyo, kitaita ni mwone,ni sakala ni mweni, sasa hiyo democrazy ya babu sisi, tuliyosoma sisi ile ya secret ballot. Ikinishinda hata juzi tulikuwa hata tarehe kumi na saba, tulipika secret ballot, nilitosheka kwa sababu ilikuwa secret. Hata ingawa hakukuwa na transparent lakini niliamini. Siwezi kusema ati hawa watu wamenionea nini na nini, aaa, ilikuwa secret ballot. Hiyo ndiyo wakenya tunataka.

Hata katika vyama tunashukuru, katika vyama vya kisiasa. Chama cha kisiasa kama hakina secret ballot katika kuchagua viongozi wao, hicho chama si cha haki. Maana mkikubali chama kinatumia mlolongo, chama kinatumia acclamation kitachukua demokrasia hiyo katika Serikali na mtaharibikiwa na Serikali.

Nashukuru tumekaa tukasikiza yote kutoka kwa Commissioner, twende na injili ya kusoma Draft Constitution ili itakapo andikwa ile kamili, iwe imetoka kwa wakenya wenyewe. Asanteni sana.

**Speaker:** Asante, basi twashukuru sana kwa yote ambayo tumenena. Tunamwita baba askofu aje atufungie kwa maombi. Katiba hii na iwe ni Katiba ya nchi ya Kenya. Asante sana.

**Bishop (Prayer):** Kabla ya kuomba, kwanza Katiba hiyo itaandikwa kwa makaratasi lakini ni maombi yangu tuyaandike kwa maisha yetu, na mioyo yetu na hata ikiwezekana, moyo wa Katiba hii uanze kufanya kazi hapa Voi. To be specific in this community. Na tuombe.

Mungu wetu, tumekuja hapa kwa nia moja ya kukuomba ya kwamba utusaidie katika Katiba ambayo itakuwa Rasilimali kubwa kwetu na kizazi kinachokuja na vingine. Tunakushukuru kwa Commissioner wetu ambaye umemleta na akiwa na lugha ya kueleweka kabisa, tunawaombea hata na team iliyoko hapa Taita ya kuongoza shughuli hizi, Bwana watakapoenda katika mashinani uwe pamoja nao kuwasaidia katika kila jambo, kazi zote watakazoendelea kuzifanya, uwe mlinzi wao na twaomba Bwana uwe mshindi kututetea katika Katiba hii. Ili mwisho yote, tuyaone yakifanya kazi na ukitubariki.

Tunaomba haya yote tukiamini umetusikia katika jina kuu la Yesu Kristo mwokozi wetu.

Audience: **Amina.**

Meeting ended at 4.30 p.m.

**&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&**